# Nipashe

Alhamisi Januari 16, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580129

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Lukuvi aanika ofisa mikopo benki alivyopata nyumba 5 kwa dhuluma

UKURASA 3




UKURASA 13

# Wingu zito latanda usajili laini za simu

**IDADI** walio bado yatisha, wengi wahaha kutafuta namba, Nida yazidi kulaumiwa...*Endelea ukurasa wa 2*







Umati wa wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, mkoani Arusha, wakiwa kwenye foleni kwa ajili ya kuandikisha kupata vitambulisho vya Taifa, katika makao makuu ya ofisi za NIDA, wilayani humo wiki hii. Picha ndogo: Wakazi wa mikoa ya Dodoma na Shinyanga, wakiwa kwenye msururu mrefu kwa ajili hiyo. **PICHA: WAPIGAPICHA WETU**

## MBUNGE WA CCM AFARIKI DUNIA

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


# OCD, ofisa ushirika waingia matatani fedha za wakulima

UKURASA 2


**MICHEZO** MOLINGA, BALINYA WATEMWA RASMI, MORISSON KIMEELEWEKA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Waziri akemea siasa za ubaguzi

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amekemea siasa zinazoashiria ubaguzi visiwani Zanzibar na kuvitaka vyama vya siasa kuwaacha wananchi wafanye kazi.

Masauni aliyasema hayo jana visiwani humo wakati wa kikao cha ndani na wanachama na wapenzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichofanyika katika ofisi za tawi la Mwembeladu visiwani humo.

"Tunataka baada ya uchaguzi watu wafanye kazi, siyo kupumbazana kila siku na kuwafanya wananchi wa nchi hii kama mazezeta. Huwezi kutengeneza misingi ya ubaguzi, ukategemea kuwa Rais katika nchi hii," alionya.

Masauni alisema miradi mingi imezinduliwa katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano na uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, huku vita dhidi ya wezi na mafisadi waliokuwa ndani na nje ya CCM ikiendelea.

Masauni aliongoza upachikaji wa bendera kwa mabalozi ishirini wa Shehia ya Mwembeladu kwa lengo la kuwaweka tayari kwa maandalizi ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

# Wingu latanda usajili laini za simu

**Na Waandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku nne kabla ya kumalizika kwa siku 20 zilizoongezwa na Rais John Magufuli kwa wananchi kusajili laini zao za simu kwa alama za vidole, wingu limezidi kutanda usajili huo kutokana na baadhi yao kushindwa kupata namba za utambulisho wa taifa.

Katika udadisi wake, Nipashe jana ilishuhudia katika maeneo mbalimbali nchini kukiwa na msongamano wa wananchi kwenye ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), wakisaka namba za utambulisho wa taifa.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, waliomba serikali kuongeza muda zaidi kwa ajili ya usajili huo, wakitoa hadhari kuwa wengi wataachwa bila mawasiliano baada ya kuzimwa kwa laini sizizosajiliwa kwa alama za vidole usiku wa kuamkia Januari 21 mwaka huu.

Wananchi hao waliitupia lawama Nida kuwa ndiyo kikwazo kwa wengi wao kujisajili kutokana na kutowapa kwa wakati namba za utambulisho wa taifa zinazotumika katika usajili huo.

Mkoani Kilimanjaro nako bado kuna idadi kubwa ya wananchi katika wilaya za Hai, Siha na Moshi ambao bado wanasotea usajili wa laini zao za simu kwa alama za vidole, huku baadhi ya mawakala wa kampuni za simu waliopewa dhamana ya kufanya usajili mitaani, wakilalamikiwa kugeuza zoezi hilo kuwa dili la kujipatia fedha.

Jana, Nipashe ilishuhudia katika maeneo ya Bomambuzi, Njoro na Kiborloni ambayo yana idadi kubwa ya wananchi katika Manispaa ya Moshi, yakiwa na msongamano wa wananchi wanaokamilisha taratibu za kusajili laini zao kwa alama za vidole, wengi wao wakilalamikia ucheleweshaji wa namba za vitambulisho vya taifa.

Shihisa Swai, mkazi wa Pasua mjini Moshi, alidai hawajui hatima yao kwa kuwa hawana uhakika wa kukamilisha usajili wa laini zao ndani ya siku nne zilizobaki.

Grace Jacob, mkazi wa Hai, aliishauri serikali kuangalia mchakato huo wa usajili huo, akisisitiza kuwa kuna watu wengi hadi sasa hawajapata namba za utambulisho wa kitaifa ilhali walijaza fomu za usajili mara kadhaa.

"Wananchi walio wengi bado hawajatimiza matakwa ya kisheria ya kusajili laini zao za simu kwa mfumo wa alama za vidole, lakini wengine wana watoto wachanga, wanapanga foleni na wanalalamika kwamba hawajapata namba za Nida, ndiyo maana kila mahali ni msongamano," Kaika Laizer, mkazi wa Gararagua, wilayani Siha, alilalamika.

Kutokana na hali hiyo, wananchi ambao bado hawajasajili laini zao, waliomba serikali kuongeza muda zaidi wa usajili huo ili kuepuka athari za kiuchumi na kijamii zitakazotokana na

INAENDELEA UK.8



Wafanyausafi wakisafisha mtaro wa maji ya mvua ili kuondoa mchanga, kando ya Barabara ya Nelson Mandela, eneo la River Side, Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**


**MAJEMBE AUCTION MART LTD**
**(VIJANA WA KAZI)**

**MNADA WA HADHARA**

KWA NIABA YA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (NHC) S.L.P 391 DODOMA TUTAUZA MALI ZA WADAIWA ZILIZOCHUKULIWA WAKATI WANAONDOLEWA KWENYE MAJENGO YA SHIRIKA LA NYUMBA BAADA YA KUSHINDWA KULIPA KODI YA PANGO.

MNADA UTAFANYIKA SIKU YA IJUMAA TAREHE 31/1/2020 SAA 3.00 ASUBUHI KWENYE ENEO LA CCM MKOA KARIBU NA SHULE YA SEKONDARI VIWANDANI.

| NA. | JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI |
|---|---|---|
| 1. | GEOFREY A. MKOLONGO | SOFA, FRIDGE, MEZA, KITANDA, GODORO, DISH |
| 2. | LUCY MICHAEL MWITA | KOCHI ZA MBAO, KING'AMUZI, VITANDA/GODORO, TV, KABATI ZA MBAO |
| 3. | CHRISTOPHER MKANDE | TV, DECL., FRIDGE, TV, MITO YA MAKOCHI NA KADHALIKA |

**MASHARTI YA MNADA:**
MALIPO NI TASLIMU NA MALI ITAONDOLEWA SIKU HIYO HIYO. KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA NAMBA 0754 301830, 0715 868000, NA 0752 858585, 0715 311067, 0783 553819


# OCD, ofisa ushirika waingia matatani fedha za wakulima

**Na Happy Severine,** MEATU

MKUU wa Polisi Wilaya (OCD) ya Meatu, Elsante Olomi, na Ofisa Ushirika wa Wilaya hiyo, George Budodi, wanadaiwa kurejesha Sh. milioni mbili zilizotolewa katika mazingira yaliyodaiwa kuwa na viashiria vya rushwa.

Imedaiwa na uongozi wa wilaya hiyo kuwa watuhumiwa hao wamerejesha kiasi hicho cha fedha hizo baada ya kubanwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Mkuu wa Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, Dk. Joseph Chilongani, aliiagiza Takukuru kuwachunguza watumishi hao wa serikali kutokana na utata ulioibuka katika kutolewa kwa fedha hizo zilizokuwa zitumike kuwalipa wakulima wa pamba katika Kijiji cha Mbushi wilayani huko.

Kwa mujibu wa Dk. Chilongani, Desemba 31 mwaka jana, OCD na ofisa ushirika huyo wanadaiwa kumtuma Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Salum Malongo, kuwashinikiza viongozi wa ushirika huo, watoe kiasi hicho kutoka kwenye fungu la Sh. milioni tano za malipo kwa wakulima, ili wasiwapeleke mahakamani.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa wilaya alidai baadhi ya viongozi wa ushirika walikubali kutoa rushwa hiyo, huku wengine wakigoma na kuamua kwenda kutoka taarifa kwake (Mkuu wa Wilaya) juu ya jambo hilo.

Katika kikao cha Kamati ya Mazao cha

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA




Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (wa pili kulia) na Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna wakionyesha mchoro wa nyumba wakati wa uzinduzi wa mikopo ya ujenzi wa nyumba, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Mkuu wa wateja wadogo, wafanyabiashara wadogo na wakati wa benki hiyo, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge CCM afariki dunia

**Na Anaeli Mbise**

MBUNGE wa Newala Vijijini, Rashid Akibar (CCM), amefariki dunia akiwa eneo la Mingoyo Mnazi Mmoja mkoani Lindi.

Taarifa iliyotolewa jana jioni na Katibu wa Siasa na Uenezi Mkoa wa Mtwara wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Selemani Sankwa, ilieleza kuwa wameshtushwa na kifo cha mbunge huyo kilichotokea jana.

Alisema CCM inatambua mchango mkubwa wa mbunge huyo enzi za uhai wake katika kuwatumikia wananchi wa Newala Vijijini na kukijenga chama hicho.

Alisema taarifa hiyo taratibu za mazishi zitatolewa baada ya makubaliano ya familia na Ofisi ya Bunge.

**SPIKA AMLILIA**

Jana jioni, Ofisi ya Bunge ilitoa taarifa kwa vyombo vya habari ikieleza kuwa Spika wa Bunge Job Ndugai, amesikitishwa na msiba huo.

"Natoa pole kwa wafiwa wote wakiwamo familia ya marehemu, waheshimiwa wabunge, ndugu, jamaa na marafiki. Mungu awape uvumilivu katika kipindi hiki kigumu," ilielezwa katika taarifa hiyo iliyomnukuu Spika Ndugai.

Akibar, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 58. Aliwahi kuwa mjumbe wa Kamati ya Maadili ya CCM kuanzia mwaka 2005 hadi 2010 na alishinda kiti cha ubunge mwaka 2015.

# Lukuvi aanika dhuluma maofisa mikopo benki

**Na Moshi Lusonzo**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Willium Lukuvi, amefichua namna maofisa mikopo wa benki wanavyodhulumu wateja wa mikopo ya nyumba.

Waziri huyo ameeleza jinsi ofisa mikopo wa benki moja jijini Dar es Salaam, alivyojipatia nyumba tano kutokana na kudhulumu wateja.

Alikuwa akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi huduma ya utoaji mikopo ya muda mrefu ya ujenzi wa nyumba inayoitwa 'Nyanyua Mjengo, inayotolewa na benki ya NMB.

Alisema kuna baadhi ya benki kwa kushirikiana na madalali matapeli wanawaibia wananchi na kuuza nyumba zao kwa mnada pasipo kufuata taratibu.

"Kuna ofisa mmoja wa benki ambaye anamiliki nyumba tano, zote amezipata kwa njia ya udanganyifu kwa kuwapora watu kwa kigezo cha wamiliki wake kushindwa kulipa," alisema. Alisema maofisa hao wanapotoa mikopo kwa wateja wao, wanasubiri ndani ya mwaka mmoja kisha wanafuata madalali ambao wanakwenda kupiga mnada mali iliyowekwa dhamana kwa madai ya kushindwa kulipa deni.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, serikali imegundua jambo hilo na kuwaonya watu wanaondesha mtandao huo kuacha mara moja.

"Watu hawa maskini wanakopa kwa ajili ya kuhakikisha wanapata angalau nyumba za kuishi, inapotumika hila ili kumfilisi kwa kuchukua nyumba yake haikubaliki kamwe," alisema.

Aliipongeza uongozi wa benki ya NMB kwa kubuni na kuanzisha huduma hiyo ambayo alielezea ni mwarobaini wa wananchi wa ngazi zote kupata nyumba zenye ubora.

Alisema kuna watu zaidi ya milioni moja ambao wanamiliki hati ya viwanja, na kama NMB itaweza kuwafikia kutaleta mabadiliko katika upangaji na uboreshaji wa miji nchini.

"NMB ndiyo benki pekee nchini ambayo imeanza kutoa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, nashauri kuongeza juhudi ni mikakati ya kuwafikia watu wengi zaidi ili kuwapo na nyumba nyingi zenye ubora," aliongeza.

Awali, Ofisa Mkuu wa Mteja Binafsi, Biashara ndogo na kati, Filbert Mponzi, alisema kwa kushirikiana na Taasisi ya Mikopo ya Nyumba Tanzania (TMRC), benki yake itatoa mikopo yenye riba ya asilimia 17 kwa watu watakaotaka kujenga nyumba za kisasa.

Alisema mkopo huo utaanzia Sh. milioni 10 hadi 200, na kuwa itawalenga wafanyakazi wa serikali na wajasiriamali wenye hati ya viwanja na wameshindwa kujenga makazi yao.

"Huduma hii itampa nafasi mteja kulipa deni kwa unafuu zaidi wakati anaendelea kuishi ndani ya nyumba yake na kuendesha shughuli zake bila hofu," alifafanua Mponzi.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa NMB, Ruth Zaipuna, aliahidi benki hiyo yake itaendelea kushirikiana na serikali katika utoaji wa huduma hiyo mpaka idadi kubwa ya Watanzania watakapomiliki makazi yao.

FARM AFRICA

TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Farm Africa limekuwa likifanya kazi nchini Tanzania tangu 1990 kama Asasi isiyo ya Serikali (NGO) chini ya Sheria ya NGO na ikiwa na cheti cha usajili no. I-NGO / 0008750. Madhumuni ya muda mrefu ni kusaidia kupunguza umasikini kwa kuendeleza njia zenye msingi wa jamii za kuboresha uzalishaji wa kilimo na matumizi endelevu ya ardhi nchini Tanzania.

Farm Africa ni shirika la kimataifa lenye ubunifu ambao hupunguza umasikini vijijini mashariki mwa Afrika kwa kusaidia wakulima kukuza uzalishaji Zaidi na zaidi: kunasaidia wakulima sio tu kuongeza mavuno, lakini pia kupata na kufikia masoko, na kuongeza thamani ya mazao. Tunaweka kipaumbele cha juu katika uendelevu wa mazingira na tunakuza njia zinazosaidia wakulima kuboresha mavuno yao na mapato bila kuharibu rasilimali zao asili.

Farm Africa inafanya kazi chini ya Mpango Mkakati wake wa kimataifa wa kipindi cha 2016-2020 wa dhamira ya Kuendesha Ustawi kupitia Kilimo

Mnamo tarehe 3 Januari 2020, Farm Africa ilisaini makubaliano na taasisi ya Mpango wa Chakula Duniani (WFP) wenye thamani ya shilling 1,407,750,726 / = kama ruzuku ya kutekeleza mradi wa miezi kumi na nane (18) ambao utazingatia mnyororo wa thamani ya mtama mkoani Dodoma. Mradi huo unakusudia kuhakikisha kwamba "walengwa wadogo katika wilaya zilizopewa kipaumbele watakuwa wameongeza upatikanaji wa masoko ya kilimo ifikapo 2030, kuboresha usalama wa chakula na lishe kupitia uzalishaji bora na mapato (lengo la SDG 2.3)."

**Mradi huo utalenga kufanikisha matokeo yafuatayo:**

1. Wakulima walengwa wanafaidika na msaada wa mnyororo wa thamani wa WFP ili kuboresha upatikanaji wa masoko yenye faida na kuongeza mapato yao.
2. Wakulima wadogo walengwa wananufaika kutokana na upatikanaji bora wa huduma na bodha za kilimo himilivu ili kuongeza uzalishaji na mapato na kupunguza athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi.
3. Wakulima wadogo walengwa wananufaika kutokana na upatikanaji mkubwa wa miundombinu ya uhifadhi katika kaya na jamii ili kupunguza upotevu wa mavuno baada ya kuvuna na kuboresha ubora wa mazao yaliyovunwa.
4. Kuongeza usawa wa kijinsia na ushiriki wa vijana katika kufanya maamuzi yanayohusiana na uzalishaji wa kilimo na shughuli za uuzaji

Mradi huu utatekelezwa katika mkoa wa Dodoma (Wilaya ya Mpwapwa, Kondoa, Bahi, Chamwino). Ilani hii ni katika kufuata kanuni ya mashirika yasiyo ya kirikali (Marekebisho), 2018 GN609 ya 19 Oktoba 2018.

*Kupata habari zaidi tafadhali tuma barua pepe kwenda infotanzania@farmafrica.org*

215587002

HABARI KITAIFA

# Bil.240/- sasa kuboresha elimu

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imeingia mkataba na Sweden kupitia Mfuko wa Ushirikiano wa Elimu Duniani (GEP), kupatiwa Dola za Marekani milioni 90 (Sh. bilioni 240.95) zitakazotumika kugharamia miradi miwili ya elimu.

Mkataba huo ulitiwa saini jana jijini Dar es Salaam kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James na Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjöberg.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini baada ya kutiwa saini kwa mkataba huo, James alisema fedha hizo zimetolewa bure na Serikali ya Sweden na siyo mkopo, na zitatumika kuendeleza sekta ya elimu nchini.

Alisema Dola za Marekeni milioni 38.89 zitatumika kugharamia Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (ESDP) kwa mwaka 2016/17-2020/2021, katika sekta tatu ndogo za programu ambazo ni elimu ya msingi, elimu jumuishi na elimu ya watu wazima.

Alisema Dola za Marekani milioni 51.11 zitaongeza mchango wa Serikali ya Sweden katika Programu ya Elimu kwa Matokeo (EPforR).

"Malengo ya EPforR ni kuwezesha Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) 2016/17-2021/22, hususani kuwezesha ubora na usawa katika matokeo ya elimu ya msingi na sekondari," alisema.

James alisema mkataba wa msaada huo unatokana na mfuko ambao unachangiwa na washirika wa maendeleo wengine ambao ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (Unicef), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco), Benki ya Dunia (WB), Umoja wa Ulaya (EU), Australia, Canada, Denmark, Ufaransa, Korea, Uholanzi, Norway, Hispania, Uswisi, Marekani na Uingereza.

Alisema serikali ya Sweden imekuwa ikitoa misaada kwa Serikali ya Tanzania katika sekta mbalimbali zikiwamo nishati, Mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma (PER), utafiti, maliasili na hifadhi ya jamii.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alisema kuanzishwa kwa mfumo wa elimu bure nchini kumeongeza uandikishwaji wa wanafunzi shule ya msingi kutoka milioni 1.1 hadi milioni 1.9 kwa mwaka.

Balozi wa Sweden, Sjöberg alisema GPE inasaidia nchi zipatazo 60, Tanzania ikiwa ni ni mojawapo wa wanachama.

Alisema mkataba huo wa miaka minne utaiwezesha Tanzania kupiga hatua katika sekta ya elimu na kuongeza idadi ya wanafunzi ifikapo mwaka 2030.

Aliongeza kuwa Serikali ya Sweden na Tanzania zimekuwa zikishirikiana kwa miaka mingi, hivyo ushirikiano huo utaendelea kuimarika zaidi.

# DC awaonya viongozi wachochezi

**Na Zanura Mollel,**
LONGIDO

MKUU wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, amekemea tabia ya baadhi ya viongozi kuchochea migogoro ndani ya jamii na kuwataka kutangaza amani na kutambua wajibu wao katika kushughulikia kero zinazowakabili wananchi.

Alisema hayo juzi wakati wa mkutano wa wenyeviti na watendaji wa vijiji vilivyoko mpakani wilayani hapa, ulioandaliwa na Mbunge wa Longido, Dk. Steven Karuswa, kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao.

"Mkichochea migogoro mnasababisha chuki baina ya wananchi, serikali na hata chama kilichokupa dhamana ya kuongoza na si chama kingine bali ni Chama Cha Mapinduzi (CCM)," alisema.

Alimpongeza Dk. Kiruswa kwa kushirikiana na halmashauri kuandaa mafunzo kwa viongozi, ambayo yatawasaidia kujifunza zaidi wajibu wao na mipaka yao ya kazi.

"Kuna maamuzi (uamuzi) mnayatoa (mnatoa) wakati mwingine si jukumu lako lakini leo (juzi) mtafahamu mipaka yenu ni ipi katika utendaji," alisema Mwaisumbe.

Akitolea mfano sakata la kitalu cha uwindaji cha Green Miles, alisema awali aliamuriwa kuondoka kutokana na kuonekana kuwa msumbufu ndani ya jamii, lakini mmiliki wa kitalu hicho alikwenda wizarani kuomba kwa kuwa tayari alikuwa na wageni wake.

Serikali kupitia Waziri wa Maliasili na Utalii, alisema ilimwongezea muda ambao alitakiwa kuondoka Desemba 16 lakini hadi sasa hajaondoka, hivyo watakutana na wahusika ambao kitalu kipo maeneo yao ili waweke azimio la pamoja.

"Green Miles alinipeleka mahakamani, Rais (John) Magufuli akanambia hata kama amekushtaki wewe kama wewe na si kama Mkuu wa Wilaya, kesi hiyo atasimama mwanasheria wa serikali kwa kuwa ulikuwa unatetea maslahi ya wananchi," alisema.

Green Mile Safari Limited inadaiwa na vijiji 23 zaidi ya Sh. milioni 329.



Mwonekano wa jengo la soko jipya la kisasa la Magomeni, litakalokuwa na ghorofa tatu, linaloendelea kujengwa na Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mashahidi 60, vielelezo 200 kujenga kesi ya vigogo Nida

**Na Hellen Mwango**

MASHAHIDI 60 wanatarajiwa kuitwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dickson Maimu na wenzake wanne.

Kadhalika, katika kesi hiyo ambayo mashahidi wa upande wa Jamhuri wataanza kutia ushahidi Januari 27, mwaka huu, vielelezo 200 vitawasilishwa. Mahakama hiyo imepanga kuanza kusikiliza shahidi wa kwanza wa Jamhuri Januari 27, mwaka huu dhidi ya kesi hiyo ya uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.

Upande wa Jamhuri ulidai jana kwamba unatarajia kuita mashahidi hao na kuwasilisha vielelezo hivyo kuthibitisha mashtaka dhidi ya vigogo hao wa zamani wa Nida.

Kesi hiyo ilipangwa kuanza kusikilizwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salumu Ally aliyepangiwa, kusikiliza kesi hiyo.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali Mkuu, Zacharia Ndaskoi, alidai upande wa Jamhuri umeshindwa kumpata shahidi wa kwanza, hivyo aliomba tarehe nyingine ya kusikiliza.

"Mheshimiwa hakimu, leo (jana) tulitarajia kuwa na shahidi mmoja, lakini tumeshindwa kumpata, tunaomba mahakama yako ipange tarehe nyingine ya kusikiliza ushahidi wa Jamhuri," alisema Ndaskoi.

Wakili wa utetezi, Joseph Ndunguru, alidai upande wa utetezi hauna pingamizi na ombi hilo, lakini kwa kuwa waliambiwa kesi hiyo ina mashahidi 60 na vielelezo 200, Jamhuri waite mashahidi wengi siku itakayopangwa kusikilizwa kesi hiyo.

Hakimu Ally alisema kesi hiyo itaanza kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Januari 27, mwaka huu.

Mbali na Maimu, wengine ni, Meneja Biashara wa Nida, Avelin Momburi; Ofisa Usafirishaji, George Ntalima; Xavery Silverius maarufu kama Silverius Kayombo na Mkurugenzi wa Sheria Nida, Sabina Raymond. Maimu na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 55 yakiwamo ya kutakatisha fedha na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.

Kati ya mashtaka mapya 55 waliosomewa washtakiwa hao, yapo ya kuisabishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175; utakatishaji fedha, kughushi; kuwasilisha nyaraka za uongo ili kumdanganya mwajiri wao; kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu; matumizi mabaya ya madaraka na kuongoza genge la uhalifu.

Hata hivyo, Maimu, Ntalima na Silverius walirudishwa rumande kutokana na mashtaka ya kutakatisha fedha yanayowakabili kutokuwa na dhamana, huku Momburi na Raymond wakiwa nje kwa dhamana.

HABARI KITAIFA

# Waziri wa Maji Prof. Mbarawa aivunja bodi ya maji

**Na Mwandishi wetu**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amevunja Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Chalinze (Chaliwasa) na kuiunganisha na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Dawasa) tangu Januari 11, 2020, ili kuongeza ufanisi katika maeneo ya kihuduma.

Uamuzi huo wa Waziri Mbarawa ulitangazwa jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, baada ya kumaliza ziara ya kukagua miradi ya maji inayoendeshwa na Dawasa iliyopo maeno ya Bunju, Mabwepande, Salasala na Changanyikeni.

Prof. Mkumbo alisema mikoa ya Pwani na Dar es Salaam ilikuwa na mamlaka mbili za maji ambazo ni Dawasa kwa Dar es Salaam na Pwani na Chaliwasa ambayo ilikuwa na jukumu la hudumia maeneo ya Chalinze, lakini ilikuwa inakabiliwa na changamoto kubwa kiuendeshaji.

"Kutokana na taratibu za wizara za kuunganisha mamlaka za maji ili kuboresha uendeshaji na kuongeza tija, Waziri wa Maji Profesa Makame Mbarawa, amefanya uamuzi wa kuinganisha Mamlaka yetu ya Chalinze (Chaliwasa) na Dawasa tangu tarehe 11, Januari 2020 Mamlaka ya Chalinze hii ipo chini ya Dawasa," alisema Mkumbo na kuongeza."

"Kwa maana hiyo Mheshimiwa Waziri amevunja Bodi ya Mamlaka ya Maji Chaliwasa, na itaendeshwa na Bodi ya Dawasa iliyo chini ya Jenerali mstaafu Davis Mwamnyange, ambayo ni bodi makini na inafanya kazi yake ipasavyo." Aliongeza kuwa Chalinze wanakabiliwa na changamoto kubwa mbili; ya kwanza hawana uwezo wa kusimamia uendeshaji kwa maana ya kulipia umeme na ya pili ni kukosa uwezo wa kununua dawa za kusafishia maji, ambapo kwa kiasi kikubwa walikuwa wanategemea kutoka Dawasa.

"Dawasa ni mamlaka kubwa na inakusanya fedha nyingi ambazo zinawawezesha kujiendesha. Tegeta peke yake Dawasa inakusanya zaidi ya Sh. bilioni moja na ndio inaongoza kuliko mamlaka nyingi Tanzania, na kwa sasa nchi nzima tunakusanya zaidi ya Sh. bilioni 23 kwa mwezi... katika pesa hiyo Sh. bilioni 10 hadi 11 zinakusanywa na Dawasa peke yake," alisema na kuongeza:

"Kwa maana hiyo, nusu ya mapato ya Mamlaka za Zaji Tanzania yapo Dar es Salaam, kwa hiyo tunataka watumie "manguvu" yao haya wakatusaidie Chalinze kulipa umeme na gharama nyingine za uendeshaji ili serikali iweze kufanya mambo mengine makubwa," alisema Prof. Mkumbo.

Alisisitiza kuwa Dawasa inatekeleza miradi mingi katika maeneo ya Chalinze, hivyo baada ya kuiachia iliyokuwa Bodi ya Chaliwasa ifanye kazi hiyo, Waziri aliona ni bora kuiweka mamlaka hiyo chini ya Dawasa ili kutoa nafasi kwa serikali kufanya mambo mengine.

## Mwimbaji injili kortini tuhuma mauaji ya mke

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWIMBAJI wa nyimbo za injili, Moses Pallangyo (29), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha akikabiliwa na shtaka la kumuua mke wake, Mary Mushi, kwa shoka.

Akimsomea shtaka hilo juzi mbele ya Hakimu Nestory Baro, Wakili wa Serikali Ahmed Khatibu, alidai mshtakiwa alitenda kosa hilo Desemba mwaka jana katika kijiji cha Kilinga wilayani Arumeru.

Baada ya kusomewa shtaka hilo kukiwa na idadi kubwa ya ndugu wa pande zote mahakamani, Hakimu Baro alimtaka mshtakiwa huyo kutojibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

"Pamoja kusomewa shtaka lako hili, lakini hutakiwi kujibu chochote, kwa sababu mahakama hii haina uwezo wa kusikiliza kesi hii zaidi ya kutaja tu," alisema.

Hakimu Baro alisema mshtakiwa atakaa mahabusu katika Gereza Kuu la Kisongo mkoani hapa. Kesi hiyo itatajwa tena Januari 28 mwaka huu.

Mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo Desemba 25 mwaka huu katika Kijiji cha Kilinga wilayani Arumeru na alidaiwa kukimbia baada ya kulitenda, na baadaye kukamatwa na Jeshi la Polisi Desemba 28 mwaka jana majira ya saa 11:30 jioni katika Kijiji cha Ekibushing, Kata ya Oltrument wilayani humo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuendelee kuchukua hatua dhidi ya mvua

**MVUA** zinazoendelea kunyesha katika maeneo mengi nchini, zimeendelea kusababisha athari kwa wakazi wa maeneo husika.

Mvua hizo zilizoanza Septemba mwaka jana, zimekuwa zikiharibu miundombinu ya barabara na madaraja pamoja na majengo, vifo na kuwakosesha watu makazi kutokana na maji kuzingira nyumba na kuzibomoa.

Mvua ni neema na zinahitajika, lakini pale zinaponyesha na kusababisha madhara kwa binadamu inakuwa kinyume cha matarajio yake, kwa sababu matarajio ni kusaidia shughuli za uzalishaji wa chakula na mahitaji mengine ya maji yakiwamo matumizi ya nyumbani na katika taasisi.

Hatutataja matukio yote yaliyosababishwa na athari za mvua hizo, lakini matukio ya karibuni ni mvua kubwa ya mafuriko wilayani Mvomero, Mkoa wa Morogoro, ambayo ilisababisha maelfu ya watu kupoteza makazi, hivyo kwenda kuishi kwa ndugu, jamaa, majirani na marafiki. Mvua hiyo pia ilisomba makaburi takribani 14.

Wakazi kadhaa wa Wilaya ya Mvomero waliopoteza makazi wanaendelea kujihifadhi kwa ndugu, jamaa, marafiki na majirani, huku wakiomba kupatiwa makazi ya muda pamoja na misaada ya kibinadamu kutoka serikalini, wadau na wasamaria wema. Katika tukio lingine, zaidi ya watu 1,000 wameripotiwa kukosa makazi, baada ya nyumba 237 kubomolewa na mvua zinazoendelea kunyesha mkoani Dodoma.

Wakazi walioathirika kutokana na mvua hizo usiku za kuamkia juzi ni wa Wilaya ya Bahi, huku miundombinu ya barabara ikiharibiwa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Mwanahamisi Munkunda, alipokuwa akizungumza, baada ya ziara ya kukagua maeneo yaliyoathiriwa na mvua hizo.

Aidha, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari, huku akiwataka wazazi kuhakikisha watoto wanacheza kwenye maeneo salama badala ya kuogelea kwenye mito na madimbwi yaliyojaa maji.

Alisema kuna mito mingi ya maji kutoka mikoa jirani na wilaya inayoishia katika Wilaya ya Bahi, hivyo wananchi wachukue tahadhari kutokana na maji kuingia kwenye makazi yao.

Kimsingi, athari za mvua zinazoendelea kunyesha zinaweza kuwa kubwa kama wananchi hawatachukua hatua kama mamlaka husika Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) zinavyosisitiza wananchi kuchukua hatua.

Mamlaka hiyo imeshatabiri kuwa mvua zitaendelea kunyesha hadi Aprili, hivyo kutoa angalizo kwa wananchi kuchukua tahadhari, hivyo kwa upande watu tunapenda kusisitiza wananchi wasipuuze kuchukua tahadhari.

Tahadhari kubwa ni kuwa wanaoishi maeneo hatarishi kama ya mabondeni na mapitio yote ya maji waondoke kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kupata madhara yatokanayo na mafuriko.

Ikumbukwe kuwa moja ya athari za mabadiliko ya tabianchi ni mvua ambazo hazifuati msimu, na zinaponyesha zinakuwa na athari nyingi ikiwamo mafuriko na upepo.


Athari hizi za mabadiliko ya tabianchi zinayakumba na kuyaathiri maeneo mengi duniani, hivyo Tanzania hatuwezi kuwa kisiwa badala yake tuchukue tahadhari.

Tukumbuke kuwa serikali haina uwezo wa kuwasaidia watu wote wanaopata athari ya mvua hususan wale ambao wamekuwa wakikaidi maelekezo ya kuyahama maeneo hatarishi kwa muda mrefu.

Ni matumaini yetu kuwa wananchi watachukua hatua kutokana na taarifa pamoja na ushauri unaotolewa mara kwa mara na mamlaka husika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kama hunywi maji ya kutosha una dalili hizi

Na Sabato Kasika

**KUNA** mambo matano, yanayotajwa na wataalamu wa afya kwamba ni miongoni mwa dalili zinazoonyesha kuwa mtu hanywi maji ya kutosha, ambayo ni kupungua kwa kiwango cha mkojo na ngozi kuwa kavu sana.

Mengine ni kuumwa kichwa na mdomo kuwa mkavu na mkojo kuwa wa njano, hivyo mtu akiwa na hali ya aina hiyo, ajue kuwa kinachochangia ni kutokunywa maji ya kutosha.

Hivyo ndivyo anavyoesema, Dk. Tumaini Mgutu wa Kituo cha Afya cha Alexia kilichopo Kigamboni, jijini Dar es Salaam na kuwataka Watanzania kuwa na mazoea ya kunywa maji ya kutosha.

Dk. Mgutu, ambaye anasema ni mtaalamu wa magonjwa ya ndani ya mwili wa binadamu, anafafanua kuwa mtu akisumbuliwa na kichwa, atambue sababu kubwa inaweza kuwa ni upungufu wa maji.

Vilevile, akiwa na ukosefu wa mate, mdomo kuwa mkavu, mkojo kuwa na rangi ya njano ajue tatizo ni hilo, kwa vile rangi ya mkojo inatakiwa kuwa ya njano kwa mbali, lakini njano kupitiliza ni tatizo.

Anasema, mwili wa binadamu unaundwa na asilimia 70 ya maji, na kwamba ni muhimu kunywa maji ya kutosha, ili kuwezesha kufanya kazi inavyotakiwa na iwapo haupati maji ya kutosha ni tatizo.

"Kwa wastani, mtu anatakiwa kwenda haja ndogo mara sita hadi saba kwa siku, na kama anakwenda chini ya mara mbili kwa siku, basi ajue kuwa hunywi maji ya kutosha," anasema Dk. Mgutu.

Anafafanua kuwa kutokunywa maji ya kutosha kunaweza kusababisha madhara mbalimbali ya muda mfupi na muda mrefu, ikiwamo magonjwa ya shinikizo la damu, saratani na magonjwa ya figo.

"Baadhi ya watu wanadharau maji ya kunywa, wanaona kula ni muhimu kuliko kunywa maji, wanaona vinywaji vingine ndivyo bora kuliko maji, hawajui ni hasara kubwa kiasi gani wanajisababishia katika miili yao," anasema.

Anasema kujijenga kwa kinga za mwili hutegemea sana maji, katika mwili, hivyo ni vyema mtu kuhakikisha anaongeza kinga ya mwili wake kwa kunywa maji ya kutosha, hasa kabla ya kula kitu chochote.

Anasema iwapo mtu akiona ana ngozi kavu, atambue hana maji ya kutosha mwilini, kwa vile hata kiwango cha maji kwenye ngozi yake kinatokana na unywaji wake wa maji.

Aidha, mtu akiona anasumbuliwa na kichwa, atambue sababu kubwa inaweza kuwa ni upungufu wa maji na pia akiwa na ukosefu wa mate, na mdomo kuwa mkavu, vilevile chanzo chake ni upungufu wa maji.

"Kwa upande wa mkojo ni kwamba rangi yake inatakiwa iwe nyeupe au njano kwa mbali, kama ukiona rangi ya mkojo si ya kawaida kuwa njano kupitiliza, tambua una upungufu wa maji mwilini," anasema.

Pamoja na kuhamasisha watu kunywa maji, joto kali linatajwa kuchangia kupoteza maji kwa wingi mwilini, kama mtu hakunywa ya kutosha, wakati wa joto kali anaweza kukumbwa na upungufu wa maji.

Kuhara na kutapika pia hupoteza maji mengi mwilini, hivyo inashauriwa kunywa maji mara kwa mara, ili kuzuia upungufu wa maji na pia ishauriwa kutumia maji yaliyoongezwa chumvi na sukari wakati mtu anapohara na kutapika kwa wakati mmoja.

Aidha, unywaji wa pombe kupita kiasi nao unachangia kupunguza maji mwilini, kwa vile pombe inasababisha mtu kwenda haja ndogo mara kwa mara na kupoteza maji kwa wingi.

Hata hivyo, mtu anatakiwa kunywa maji kulingana na uzito wako na kwamba mwenye kilo 50 anatakiwa kunywa lita mbili, wakati mwenye kilo 65 anatakiwa kunywa maji lita tatu kwa siku moja.

Kwa mtu mwenye kilo 80 na kuendelea, anatakiwa kunywa maji lita nne kwa siku, na kwamba kukaa bila ya kunywa maji ni hatari kwa afya, lakini mtu anatakiwa aanze kunywa kiasi.

Wataalamu wa afya wanasema, sio lazima mtu aanze moja kwa moja kunywa lita moja ya maji, mbili au tatu kwa siku, bali aanze kiasi polepole na kuongeza idadi au chupa za maji na kufikia lengo lake kwa kuzingatia uzito wake.

# Babu miaka 89 arejeshewa eneo lake

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

DALALI wa Mahakama ya Ardhi na Nyumba wa Kampuni ya Mkassiwa Auction Mart Court Brocker wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Rashid Mkasiwa, amekabidhi eneo kwa Faustine Shagembe (89) lililokuwa limetwaliwa na Julius Zephania kwa amri ya Mahakama.

Mgogoro huo wa ardhi baina ya Shagembe, Zephania na wenzake umedumu kwa miaka kumi sasa.

Akizungumza na eneo la tukio na kushuhudia ubomoaji wa msingi wa nyumba, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyahanga, Felician Fabiai, alisema alifika eneo hilo baada ya kupata wito kutoka Mkassiwa Auction Mart Court Brocker ambao walipewa agizo na Mahakama kuvunja majengo au nyumba katika kesi ya msingi Na. 14 /2008 inayowahusu Shagembe (mlalamikaji) Zephania na wenzake (walalamikiwa).

Mtendaji huyo alisema kuwa hukumu ya Julai 27, 2018 iliwataka walalamikiwa hao kuondoa au kuvunja maendelezo katika ardhi hiyo, lakini walishindwa kutekeleza agizo la mahakama hadi ilipochukuliwa hatua hiyo ya kumtaka dalali wa mahakama kutekeleza agizo hilo.

Alisema baada ya kujiridhisha kwa kuona nyaraka ya mahakama, kama mlinzi wa amani katika kata hiyo, alisimamia zoezi la kukabidhiwa eneo lake mzee Shagembe ambaye ndiye mshindi wa tuzo.

Aidha, mtendaji alisema kuwa makabidhiano hayo yalifanyika Desemba 18, mwaka jana katika hali ya usalama, huku mshindwa tuzo Zephania, wenzake, jirani zake, askari Polisi wawili na viongozi wengine wa kata hiyo wakiwapo.

Alisema kuwa Zephania alishauriwa kulalamika endapo hajaridhika na hukumu hiyo.

Fabian alitumia fursa hiyo kuwasihi wananchi na wakazi wa Kata ya Nyahanga kuwa makini katika manunuzi ya viwanja kwa kujiridhisha zaidi kwa kufika katika Ofisi ya Idara ya Ardhi na Mipango Miji ili kupata ushauri wa kitaalamu, hali ambayo itapunguza migogoro ya ardhi katika maeneo yao.

Mkurugenzi wa Mkassiwa Auction Mart Court Brocker, Rashid Mkasiwa, akizungumza baada ya kuvunja msingi wa nyumba iliyokuwa imeanza kujengwa katika eneo hilo, alisema kuwa amepewa amri na Mahakama ya kuvunja na kubomoa chochote kilichojengwa katika kiwanja cha Shagembe.

"Nimetekeleza amri halali ya mahakama kuvunja msingi wa nyumba kwa amani na utulivu kutokana na ulinzi uliopo," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima (kulia), akikagua vitabu katika boksi moja kati ya maboksi 29 vya Historia, Hisabati, Uraia, Kemia na Biolojia, vilivyotolewa na Mwenyekiti wa Taasisi ya Wasira, Steven Wasira (wa pili kulia), kwa shule 29 za sekondari za serikali wakati wa uzinduzi wa taasisi hiyo, mkoani Mara juzi. **PICHA: ROSE JACOB**

# Mhasibu TPA matatani kosa lisilo na dhamana

**Na Hellen Mwango**

MHASIBU wa zamani wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Stephen Mtui, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 5.8.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi, Vicky Mwaikambo. Wakili wa Serikali, Faraji Nguka, alidai kuwa kati ya Julai 6, 2014 na Julai 8, 2014 katika eneo la bandari kavu AMI jijini Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alighushi nyaraka na risiti yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 2.6 kama malipo ya bandari ikionyesha kampuni ya Anchor Clearing and Forwarders kupitia benki ya CRDB kama tozo ya bandari, huku akijua si kweli

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa kati ya Julai, 2014 na Aprili 2015 eneo hilo jijini Dar es Salaam, mshtakiwa huyo akiwa mtumishi wa mamlaka ya Bandari aliiba zaidi ya Sh. bilioni 5.8 mali ya TPA.

Shtaka la nne, ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo kuisababishia mamlaka hiyo hasara, tarehe hiyo hiyo katika eneo la bandari kavu AMI jijini Dar es Salaam mshtakiwa huyo aliisababishia hasara ya zaidi ya Sh. 5.8 bilioni.

Upande huo wa Jamhuri ulidai katika shtaka la tano kuwa kati ya Julai, 2014 na Aprili 2015 katika eneo la AMI mshtakiwa huyo akiwa na wenzake walifanya miamala yenye thamani ya zaidi ya Sh. 5.8 bilioni wakati akijua ni zao la wizi.

Baada ya kusoma hati ya mashtaka, Nguka alidai kuwa upelelezi wa shauri hilo haujakamilika, hivyo aliiomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine.

Hakimu Mwaikambo alisema kutokana na shtaka linalomkabilili mshtakiwa huyo mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi hadi hapo Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) atakapotoa kibali cha kusikiliza shauri hilo.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Januari 20, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu, kutokana na makosa ya uhujumu uchumi kutokuwa na dhamana.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TANZANIA COMMUNICATIONS REGULATORY AUTHORITY

ISO 9001:2015 CERTIFIED

TCRA CREATING A LEVEL PLAYING FIELD

TAARIFA KWA UMMA

NDUGU WATANZANIA;

KAMA MNAVYOFAHAMU, MWISHO WA KUTUMIKA KWA LAINI ZA SIMU AMBAZO HAZIJASAJILIWA KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBUSHO CHA TAIFA **(NIDA)** NA KUTHIBITISHWA KWA ALAMA ZA VIDOLE NI **TAREHE 20 JANUARI, 2020.**

**HAKIKI TENA USAJILI WA LAINI ZAKO KWA KUPIGA NAMBA *106# NA UCHUKUE HATUA STAHIKI SASA.**

IKUMBUKWE KWAMBA UKOMO WA TAREHE 20.01.2020 UNAWAHUSU WALE TU AMBAO WANA LAINI ZA SIMU SASA (AMA KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU AU VIFAA VYAO VYA MAWASILIANO MENGINE) LAKINI HAWAJAZISAJILI KWA KUTUMIA NAMBA YA KITAMBULISHO CHA TAIFA **(NIDA)** NA KUTHIBITISHWA KWA ALAMA ZA VIDOLE.

1. KWA WATAKAOSITISHIWA HUDUMA ZA LAINI ZAO ZA SIMU TAREHE 20.01.2020 WANAWEZA PIA KUENDELEA NA UTARATIBU WA USAJILI KWA LENGO LA AMA KURUDISHA LAINI ZAO ZITAKAZOKUWA ZIMEFUNGWA AU KUPATA LAINI MPYA. **ZOEZI HILI NI ENDELEVU**.
2. KWA WATUMIAJI/WAOMBAJI WAPYA WA LAINI ZA SIMU WATAENDELEA KUSAJILIWA MUDA WOTE NA USAJILI HUO KWA KUTUMIA KITAMBULISHO CHA TAIFA NA KUHAKIKIWA KWA ALAMA ZA VIDOLE. **HUDUMA HIYO NI ENDELEVU PIA.**
3. KWA WANADIPLOMASIA AU TAASISI ZAO AMBAO HAWAJAKAMILISHA USAJILI WA LAINI ZAO ZA SIMU AU ZINAZOTUMIKA KWENYE VIFAA VYAO VYA MAWASILIANO WAENDELEE KUFUATA UTARATIBU WALIOWEKEWA.

**Imetolewa na Mkurugenzi Mkuu**
**TCRA**
**15 Januari, 2020**

# Bunge labaini Tazara kuelemewa madeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA



KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji Mitaji ya Umma (PIC), imesema kuwa Shirika la Reli la Tanzania na Zambia (Tazara) linakabiliwa na mzigo wa madeni makubwa, hali ambayo inasababisha kushindwa kukopesheka.

Kutokana na hali hiyo kamati hiyo imependekeza kuwa serikali za Tanzania na Zambia kukaa kwa pamoja ili kuona namna ya kulisaidia fedha shirika hilo kwa utaratibu mwingine ili kulinusuru.

Hayo yalielezwa jana na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Raphael Chegeni (pichani), alipokuwa akitoa maagizo yake kwa viongozi wa shirika hilo walioitwa mbele ya kamati yake.

Alisema kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na uongozi wa shirika hilo mbele ya kamati hiyo, hali inaonyesha dhahiri kuwa hivi sasa Tazara inajiendesha kwa hasara kutokana na mzigo mkubwa wa madeni iliyonayo.

"Hivi sasa kutokana na madeni yaliyopo Tazara haiwezi kukopesheka benki yoyote hivyo basi kutokana na hali hiyo, kamati inaona ni vizuri sasa serikali ya Tanzania pamoja na ile ya Zambia kukaa pamoja kuona ni jinsi gani wanaweza kulisaidia fedha shirika hili kwa namna nyingine ambayo siyo mkopo kwani halikopesheki tena shirika hili," alifafanua Chegeni.

Alisema ipo haja ya kufanyiwa marekebisho ya sheria inayosimamia uendeshaji wa shirika hilo kwani hivi sasa utendaji unafanyika katika mazingira ambayo kila mmoja hamwamini mwenzie.

"Huwezi kuingia ubia na mtu, wakati kila mmoja hamwamini mwenzie, hivyo basi ipo haja kwa menejimenti kulifanyia kazi suala hili la kisheria kwani Tazara tunahitaji sana ndiyo kiunganishi cha mataifa kusimu mwa Afrika hivyo lazima tuweke nguvu zetu katika kuhakikisha kuwa tunaliokoa katika hali yoyote ile," alisema Chegeni.

Pia alisema Tazara pamoja na kukabiliwa na mzigo wa madeni, bado inakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa mindombinu, mfumo mbovu wa mawasiliano na udhibiti mbovu wa mapato ambao unachangia kujiendesha kwa hasara.

Vilevile Dk. Chegeni aliutaka uongozi wa Tazara kubadilika kiutendaji kwa kubadili mitazamo waliyonayo hivi sasa katika uendeshaji wa shirika ili waongeze tija tofauti na ilivyo sasa.

Aliongeza kuwa pamoja na shirika hilo kuendesha kwa hasara, lazima uongozi uhakikishe kuwa unatimiza jukumu lake la kutoa gawio kwa serikali.

"Hili gawio mwisho ni Januri 23, lazima sisi kama kamati tupate 'commitment' yenu juu ya ulipaji wake kwani hili gawio ni pamoja na kwa mashirika yale ambayo mapato yake ni yale yasiyotokana na kodi," alisema. Awali mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, Richard Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, alihoji kuwa kwanini shirika hilo kwenye mfumo wa utawala mtendaji mkuu ni lazima awe kutoka nchini Zambia na Naibu wake kutoka Tanzania.

Mbogo alisema kwanini Tazara haioni kuwa ipo haja mtendaji mkuu awe anatoka kila nchi kwa vipindi tofauti kwa mujibu wa utaratibu utakaowekwa.

"Kila wakati lazima mtendaji mkuu atoke Zambia na Naibu Tanzania, Tazara hawaoni kuwa ipo haja ya hawa watendaji kuwapo utaratibu maalumu kuwa wanapokezana na siyo kama ilivyo sasa kila wakati ni kutoka Zambia tuu?" Alihoji Mbogo.

## OCD, ofisa ushirika waingia matatani fedha za wakulima

INATOKA UK. 2

Januari 11 mwaka huu, kilichojadili kujadili jambo hilo, Mkuu wa Wilaya aliagiza Takukuru kuwahoji watuhumiwa hao juu ya fedha hizo.

Dk. Chilongani alidai kuwa Januari 13, ofisa ushirika alirejesha fedha hizo kwenye ofisi za Takukuru wilaya baada ya kubanwa, lakini hakueleza sababu za kuwa nazo.

Akikabidhi fedha hizo jana kwa Mkuu huyo wa Wilaya ili zipelekwe kwa wakulima, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Simiyu, Joshua Msuya, alidai uchunguzi wa awali umeonyesha kuwapo kwa vitendo vya rushwa.

"Lengo letu la kwanza lilikuwa hizo pesa zipatikane na tuwapelekee wakulima walipwe na tumefanikiwa leo (jana) tutakabidhi pesa hizo kwako Mkuu wa Wilaya, na huo ni uchunguzi wetu wa awali," alidai.

Bosi huyo wa Takukuru mkoa alidai kazi ya uchunguzi bado inaendelea kwa watuhumiwa wote wakiwamo viongozi wa ushirika ambao wanadaiwa kutoa rushwa hiyo kwa kuwa sheria inasema anayetoa na kupokea, wote wana makosa.

Akipokea fedha hizo, Mkuu wa Wilaya, Dk. Chilongani, aliipongeza Takukuru kwa kazi kubwa ya kuhakikisha zinapatikana, huku akitaka uchunguzi uendelee kwa watuhumiwa wote ili wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Mkuu wa Wilaya huyo pia alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Fabian Manoza, kumsimamisha kazi mara moja Ofisa Ushirika (Budodi) kutokana na kukabiliwa na tuhuma hizo huku akitoa onyo kali kwa watu wanaochezea fedha za wakulima.

# Wingu latanda usajili laini za simu

INATOKA UK. 2

kuzimwa kwa laini zao.

**ARUSHA**

Jijini Arusha, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) imebainisha kuwa laini za simu 14,161 zimesajiliwa ndani ya siku tisa katika jiji hilo.

Mkuu wa TCRA Kanda ya Kaskazini, Imelda Salum, aliiambia Nipashe jana kuwa laini hizo zilisajiliwa kuanzia Januari 6 hadi 14 mwaka huu kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Arusha.

Aliyataja maeneo ambao usajili huo ulifanyika kuwa ni pamoja na Namanga, Ngaramtoni, Mto wa Mbu, Tengeru, Karatu, Ngorongoro na Wasso.

"Tulipoona siku zimeongezwa hadi Januari 20 mwaka huu, tuliamua kutawanyika maeneo ya wazi kama hapa jijini Arusha, tunaandikisha uwanja wa mpira wa Shekhe Amri Abeid ili wananchi wengi tuwafikie," alibainisha.

Alisema wataendelea na usajili kwa siku nne zilizobaki ili wananchi wapate haki yao ya mawasiliano.

**PWANI**

Mjini Kibaha mkoani Pwani jana kulishuhudiwa pia idadi kubwa ya wananchi kwenye ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) wakisubiri kupata namba.

Baadhi ya wananchi waliokutwa na Nipashe kwenye kituo hicho kilichoko Tumbi mjini Kibaha, walidai wanalazika kufika katika eneo saa 12 asubuhi ili kuwahi kupanga foleni.

"Kila ukija hapa foleni bado ni kubwa kila siku, sina uhakika kama nitasajili laini zangu kwa siku hizi tano zilizosalia, labda watu wa Nida wabadilishe utaratibu wa kutoa namba badala ya kukaa zaidi ya siku saba bila kupata namba," Ally Mohamed alilalama.

Mohamed alidai kuwapo kwa foleni ndefu ya wananchi wanaosubiri kupewa namba ya utambulisho wa taifa ni dalili kwamba wananchi wengi watakosa mawasiliano baada ya laini zisizosajili kuzimwa.

Nipashe ilipita kwa mawakala wa kampuni za mawasiliano ya simu ambao wanasajili laini za simu kwa alama za vidole na kukuta wakiwa na idadi ndogo ya wateja huku wakikosa hata mteja mmoja.

**RUVUMA**

Wilayani Songea mkoani Ruvuma, baadhi ya wananchi waliiambia Nipashe jana kuwa licha ya Rais Magufuli kuongeza muda wa kusajili laini kwa alama za vidole, bado Nida imeonyesha kuwa na matatizo ya kiutendaji kutokana na kutopatiwa namba za usajili kwa wakati.

Walidai kuwa baadhi yao wamekuwa wakitoka vijijini kwenda kwenye ofisi za Nida katika Manispaa ya Songea ili kupatiwa namba za vitambulisho zinazotumika kwenye usajili wa laini, lakini wanaambiwa hazijapatikana.

Martin Komba, mkazi wa Kijiji cha Mpitimbi wilayani Songea, akiwa kwenye ofisi za Nida mjini Songea, aliliambia gazeti hili jana kuwa ameshajiandikisha na kupigwa picha lakini hajapatiwa namba ya usajili na ameambiwa arudi Januari 30 mwaka huu ilhali usajili wa simu utafutwa Januari 20.

Alisema anaona usajili huo ni usumbufu kwa wananchi ambao wanaacha shughuli zao muhimu wakati huu wa msimu wa kilimo na kwenda mjini kufuatilia namba za Nida.

John Fransis, mkazi mwingine wa wilaya hiyo, aliipongeza serikali kwa kuchukua uamuzi wa kuongeza siku za kusajili laini, vinginevyo asingefanikiwa kusajili laini zake.

Wakala wa Kampuni wa Simu ya Mkononi ya Airtel, Songea Mjini, Amani Mbwambo, akizungumza na Nipashe jana mchana ofisini kwake, alisema wanaendelea kusajili laini na anaamini mpaka Januari 20 mwaka huu, wateja wengi watakuwa wamefanikiwa kusajili laini zao kwa alama za vidole.

Ofisa Masoko wa Kampuni ya Simu za Mkononi ya Vodacom Mkoa wa Ruvuma, Michel Kivuyo, alisema kampuni hiyo imejipanga kikamilifu kuhakikisha wateja wote wanaokidhi vigezo wanasajiliwa, lakini tatizo kubwa liko kupata namba za Nida.

**KATAVI**

Nida pia ilitupiwa lawama na baadhi ya wakazi wa Mkoa wa Katavi, waliodai kuwa bado kuna tatizo katika kupata namba za utambulisho wa kitaifa.

Walidai kuwa wengi wao wanapofika kwenye vituo vya Nida kufuatilia namba zao, wanaambiwa kuwa hawakidhi vigezo, baadhi yao wakidai walijaza fomu tangu Julai mwaka jana lakini hawajapata namba hadi sasa.

"Tulipofuatilia namba wakadai tulikosea kujaza fomu, tukajaza tena na kupitisha sehemu zote, tukairudisha wakakataa tena, wakasema hairuhusiwi kupiga picha mara mbili, tutatuma hizi namba," walilalamika.

Kaimu Ofisa Usajili wa Vitambulisho vya Taifa Mkoa wa Katavi, Mahona Karumbeta, alisema jana kuwa ugawaji wa namba za utambulisho wa kitaifa umekamilika kwa asilimia 88 mkoani humo.

"Hali siyo mbaya sana na wala siyo nzuri sana," alisema, "mpaka sasa tumetoa namba kwa asilimia 88, na tunaendelea kutoa huduma ya kusajili pia."

**SHINYANGA**

Wakati hali ikiwa hivyo Katavi, mkoani Shinyanga tatizo la kukatika kwa umeme limetajwa kuchangia kuchelewesha wananchi kupata namba za vitambulisho vya taifa.

Jana, Nipashe iliwakuta wananchi katika ofisi za Nida mjini Shinyanga wakiwa wamekaa kwenye makundi huku wengine wakilala jirani na ofisi hizo kutokana na umeme kukatika.

Mamea Hassani, mkazi wa Mwasele mjini Shinyanga, alidai alifika kwenye ofisi hizo saa tatu asubuhi, lakini hadi muda saa tisa alasiri hakupata namba ya kitambulisho cha Nida huku umeme nao ukikatika.

"Zoezi hili la upataji wa namba za vitambulisho vya Nida ni gumu. Tunamwomba Mheshimiwa Rais Magufuli aongeze tena muda, angalau hata wiki moja mbele, watu ni wengi sana na muda nao unazidi kuisha, hapa huduma zimesitishwa kwa saa nzima sasa kutokana na umeme kukatika," alilalamika.

Ofisa Uandikishaji wa Vitambulisho vya Nida mkoani Shinyanga, Nathani Njau, alikiri kuwapo kwa tatizo la umeme kukatika, lakini akasisitiza kuwa uandikishaji unaendelea vizuri kwa kuwa kwa siku wamekuwa wakiandikisha watu zaidi ya 500.

Mwishoni mwa mwaka jana, Rais Magufuli alisajili laini yake kwa alama za vidole na kuongeza siku 20 kutoka Januari Mosi hadi Januari 20 mwaka huu kwa wananchi kukamilisha usajili kwa mfumo huo.

**●Imeandikwa na Godfrey Mushi (MOSHI), Cynthia Mwilolezi (ARUSHA MJINI), Julieth Mkireri (KIBAHA), Gideoni Mwakanosya (SONGEA), Neema Hussein (KATAVI) na Marco Maduhu (SHINYANGA MJINI).**

## Wasafirishaji sasa kufuatiliwa saa 24

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi), imeanzisha utaratibu wa kufuatilia utendaji kazi wa mizani kwa saa 24 kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kamera za CCTV, ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi wa mizani hizo na kudhibiti vitendo vya rushwa.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Ujenzi, Elias Kwandikwa, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji ya wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu jijini, Dodoma.

"Mfumo huu umetuwezesha kugundua mwenendo mzima wa upimaji magari katika mizani kwani hata kama kuna vitendo vya rusha vimefanyika, basi mfumo unatusaidia kubaini vitendo hivi na inakuwa rahisi kuchukua hatua kwa yule aliyehusika," alisema Naibu Waziri Kwandika.

Aidha, amefafanua kupitia mfumo huo suala la utunzanji wa barabara kupitia mpango wa udhibiti magari yaliyozidisha uzito nalo ni la uhakika kwani magari yaliyozidisha uzito yanaweza kubainika na kuchukuliwa hatua.

"Mathalani, katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2019, jumla ya magari 3,080,285 yalipimwa ambapo kati ya hayo, magari 19,432 yalikuwa yamezidisha uzito wa zaidi ya asilimia tano ya uzito unaoruhusiwa na kutozwa tozo ya uharibifu wa barabara ambayo ni sawa na asilimia 0.63% ya magari yote yaliyopimwa," alisema Naibu Waziri.

Aliongeza kuwa wizara inaendelea kuelimisha wasafirishaji na wadau wengine kuhusu Sheria mpya ya Udhibiti Uzito wa Magari ya Afrika Mashariki ya mwaka 2016.

Kwandikwa alieleza kuwa katika kuhakikisha wakala unaendelea kusimamia kazi za udhibiti wa uzito wa magari, umeendelea kuweka mfumo wa kupima magari yakiwa kwenye mwendo ambapo kwa sasa mfumo huu tayari unafanya kazi katika vituo 13 na hivyo kupunguza msongamano wa magari katika mizani pamoja na muda wa kusafiri.

Alitaja baadhi ya vituo vya mizani vilivyofungwa mfumo huu ni pamoja na Njuki (Singida), Nala (Dodoma), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe).

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso, aliupongeza wakala huo kuendelea kutekeleza miradi yake ambayo ina tija kwa Taifa na kusisitiza wizara kuendelea kulipa madeni ya makandarasi ili kuwezesha miradi mingine ambayo imesimama kuendelea kutekelezwa.

"Naomba wizara mwendelee kulipa madeni ya makandarasi kwa kadri mnavyopata fedha kutoka Hazina, mkichelewa kulipa mnasababisha miradi kukwama na wananchi kukosa maendeleo," alisema.

Katika hatua nyingine, serikali kupitia wizara hiyo imeamua kununua gari maalum litakalogharimu kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya ukaguzi wa barabara.

Gari hilo ambalo litakuwa la kisasa litaweza kukagua mtandao wote wa barabara kuu hapa nchini ndani ya mwezi mmoja na kutoa majibu ya ubora na upungufu wa barabara kuanzia hatua za awali za ujenzi hadi mradi utakapokamilika.

# Bil. 117/- kwa majisafi wilaya 86

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, amesema serikali imepeleka Sh. bilioni 117 katika wilaya 86 na mikoa 17 kwa lengo la kuboresha na kuongeza huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama vijijini kwa kujenga vituo vipya vya maji na kufufua vya zamani.

Alisema kila wilaya imepatiwa Sh. bilioni 1.36 ambapo wamekabidhiwa Mameneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) ili kufikia malengo ya serikali iliyoahidi kwa wananchi ifikapo Desemba 2020 huduma ya upatikanaji maji kwa vijijini iwe kwa asilimia 85.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini Dar es Salaam wakati wa ziara ya kukagua maeneo yote yaliyohusisha ujenzi wa matangi na vituo vya kusukumia maji katika maeneo ya Bunju, Mabwepande, Salasala na Changanyikeni miradi inayoendeshwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa).

Akitoa taarifa hiyo baada ya kuhitimisha ziara yake, Prof. Mkumbo alisema kuwa hii ni mara ya kwanza halmashauri kupata fedha nyingi katika miradi ya maji kwa wakati mmoja hivyo amewataka wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri pamoja na viongozi wengine katika ngazi husika wasimamie utekelezaji wa miradi hiyo kikamilifu.

"Niwatake wakuu wa wilaya, wakurugenzi pamoja viongozi wengine watusaidie kusimamia utekelezaji wa miradi tuliopeleka kule kwa sababu Sh. bilioni 1.3 ni fedha nyingi na hii ni mara ya kwanza kwa baadhi ya halmashauri kupata fedha nyingi kwa wakati mmoja katika miradi ya maji," alisema Prof. Mkumbo.

Aliongeza kuwa pia, serikali imepeleka Sh. bilioni 25 Wizara ya Afya kwa ajili ya hospitali na Sh. bilioni 7 kwenye Wizara ya Elimu ili kuboresha usafi wa mazingira ikiwamo kujenga vyoo vipya katika wilaya na mikoa hiyo.

Alisema katika fedha hizo, serikali ilichukua mkopo wa Dola milioni 350 kutoka Benki ya Dunia kwa miaka mitano ijayo na kwa awamu ya kwanza fedha hizo zimetumika katika sekta ya maji.




Mwendesha guta akiwa ameshika mkono mmoja kwenye lori, lililokuwa kwenye mwendo kasi katika Barabara ya Morogoro, eneo la Magomeni Kagera, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Wazee watoa kilio cha dawa hospitalini

**Na Ndalike Sonda,**
KAHAMA

UMOJA wa wazee wilayani Kahama mkoani Shinyanga (UWAKA), umeiomba serikali kuzidi kuboresha huduma za afya kwa kuongeza upatikanaji wa dawa katika hospitali zote za serikali ili kuondoa usumbufu wa kuwataka wazee kwenda kununua dawa.

Umoja huo umesema kwamba wazee wamekuwa wakielekezwa kwenda kujinunulia dawa baada ya kupata vipimo hospitalini.

Katibu wa Uwaka, Paul Ntelya, aliambia Nipashe kuwa wanaipongeza serikali kwa kutenga dirisha la wazee katika hospitali za serikali, lakini kinachopaswa kufanyika kwa sasa ni kuboresha upatikanaji wa dawa ili kila mzee anayehitaji matibabu aweze kupata dawa.

Ntelya alisema ingawa wazee wamekuwa wakipewa kipaumbele kwenye matibabu, lakini bado huduma ya dawa imekuwa changamoto kwani suala la kuandikiwa kwenda kutafuta dawa nje ya hospitali linasababisha wazee wengi kutoendelea na dozi ya dawa kwa kuwa hawana uwezo wa kupata fedha za matibabu.

"Serikali yetu tunaiomba izidi kuongeza upatikanaji wa dawa ili wazee wawe wanapata huduma zote katika eneo la hospitali badala ya kwenda kununua kwenye maduka ya dawa, kwani wazee wengi hawana uwezo, hawana hata uhakika wa mlo iweje apate hela ya dawa?" Alihoji Ntelya.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. Lucas David, alisema upatikanaji wa dawa umeboreshwa ikilinganishwa na nyuma, baada ya hospitali hiyo kuanza kupokea dawa kila baada ya miezi miwili kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD), badala ya miezi mitatu.

Dk. David alisema halmashauri hiyo pia imeshawakatia bima za afya ya jamii (CHF) iliyoboreshwa wazee zaidi ya 2,000, ambao wanaendelea kupata huduma bure, huku akiwataka wananchi kuendelea kujiunga na CHF pamoja na Mfiko wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF).

Katika hatua nyingine umoja huo wa wazee wilayani Kahama, Uwaka, kupitia kwa katibu wake Ntelya umeiomba serikali kukamilisha azma yake ya kuanza kuwalipa pensheni wazee ili kuwasaidia kujikwamua kimaisha kwa kuwa walikuwa na mchango mkubwa katika taifa.

# 75% ya Watanzania kujumuishwa bima afya 2025

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga, amesema kuwa, mfuko huo ifikapo 2025 unataka zaidi asilimia 75 ya Watanzania wawe wamejumuishwa katika mfumo wa bima ya afya.

Ameyasema hayo jijini Arusha wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uhamasishaji wa wananchi kujiunga na NHIF kupitia vifurushi vipya.

"Tumeleta mfumo wa vifurushi ili kumwezesha Mtanzania mmoja mmoja kujiunga na bima ya afya na kuwa na uhakika wa matibabu wakati wowote," alisema Konga.

"Tunaamini mpaka kufika mwaka 2025 utakuwa unahudumia idadi kubwa ya wananchi kutokana na kuweka utaratibu rafiki wa kila kundi kuwa na fursa ya kujiunga na huduma za bima ya afya," alisema.

Aidha, Konga alisema kuwa mfuko umejipanga kuhakikisha unatoa huduma bora za matibabu kwa wanachama wake kwa kuboresha kitita cha mafao na kuwa na mtandao mpana wa vituo vya kutolea huduma.


Akizindua mpango huo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alisema kuwa pamoja na Serikali ya Awamu ya Tano kuboresha Mfumo wa Bima ya Afya pia imeendelea kuboresha miundombinu ya maeneo ya kutolea huduma ili mwananchi anapokuwa na kadi yake ya bima anakuwa na uhakika wa matibabu na yenye kiwango bora.

Alisema kuwa bima ya afya ni nyenzo muhimu kwa maisha ya kila Watanzania kwa kuwa inampa uhakika na kumwezesha kufanya kazi kwa kujiamini.

"Watu wanaopinga utaratibu huu wa vifurushi vya bima ya afya hawawatakii mema Watanzania, pindi unapopatwa na matatizo hawatakuja kukusaidia, tuwapuuze na tujiunge na mapango huu wa bima ya afya," alisema.

Aliwaagiza viongozi wa mkoa pamoja na viongozi wa dini kushirikiana kwa pamoja katika kuwahimiza na kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuwa na bima ya afya.

"Mpango huu wa vifurushi vya bima ya afya unakuwezesha kupata tiba popote pale nchini hivyo ni jambo muhimu sana kwa maendeleo yetu," alisema.



Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Simiyu, Joshua Msuya (kushoto), akikabidhi Sh. milioni mbili kwa Mkuu wa Wilaya ya Meatu, Dk. Joseph Chilongani, juzi. Fedha hizo zilirejeshwa na Ofisa Ushirika wa wilaya hiyo, ambaye alituhumiwa kuzipokea kama rushwa kutoka kwa viongozi wa Amcos wa Kijiji cha Mbushi. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Watoa huduma usajili simu watakiwa kuongeza nguvu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, amewaagiza watoa huduma za kusajili laini za simu kwa alama za vidole kuongeza nguvu katika eneo la Nyerere Square ili kupunguza foleni kubwa ya wananchi wanaopata huduma hiyo.

Agizo hilo alilitoa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya uongozi wa wilaya hiyo kufanikiwa kuwaunganisha watoa huduma za kusajili laini za simu kwenye eneo moja la wazi, ili wananchi wapate huduma kwa haraka kabla ya kufungwa kwa usajili huo Januari 20, mwaka huu.

Alisema kumekuwapo na mwitikio mkubwa wa wananchi kutokana na uongozi huo kutenga eneo hilo ambalo makampuni ya simu za mikononi, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), wote wapo hapo ili kufanikisha usajili huo.

Katambi aliwataka wahusika wa kutoa huduma ya utaratibu wa kupata vitambulisho vya Taifa hadi kusajili laini ya simu kwa njia ya vidole kuhakikisha wanaongeza nguvu ili kuwahudumia wananchi wanaojitokeza kupata huduma hiyo.

"Nashukuru wazo letu la kuwasaidia wananchi kupata huduma katika eneo moja la wazi limefanikiwa, lakini nawataka watoa huduma kuongeza nguvu kutoka na mwitikio mkubwa wa wananchi katika siku hii ya kwanza," alisema.

Aliwataja watoa huduma hao wanaotakiwa kuongeza nguvu kuwa ni Ofisi ya Nida, watoa huduma za simu za mkononi na Idara ya Uhamiaji.

Alisema lengo la kuanzisha eneo hilo la pamoja ni kuhakikisha wanapunguza mzunguko wa wananchi kutafuta huduma hiyo.

"Wananchi wapo hapo tangu asubuhi sikutegemea kama idadi itakuwa kubwa hivi, na serikali yetu tunawahakikishia usalama wakati wote na mtapata huduma kwa wakati," alisema.

Aidha, alisema wameweka askari Polisi wa kuwasaidia watu wenye ulemavu, wajawazito na wenye watoto wadogo pamoja na wazee ili kupewa kipaumbele katika kupata huduma.

Aliwataka wananchi wote ambao hawajasajili laini zao za simu kwa njia ya vidole na ambao hawajapata namba ya Nida kutumia fursa hiyo ya kufika eneo hilo.

Kwa upande wake, Ofisa Msajili Nida mkoa wa Dodoma, Khalid Mrisho, alisema ofisi hiyo inakabiliwa na changamoto ya idadi kubwa ya wananchi wapya waliojitokeza kwenye kujiandikisha kwa ajili ya usajili huo.

Mrisho alisema kwa sasa Nida wanatoa huduma katika maeneo matatu katikati ya mji wa Dodoma ili kuhakikisha wanakamilisha kabla ya kufungwa kwa usajili huo.

Mrisho alivitaja vituo hivyo kuwa ni jengo la Bima, eneo la Mji mpya na eneo la kituo kipya cha Nyerere Square ambapo watahakikisha wanafanyakazi kwa saa 24 kama agizo la Mkurugenzi Mkuu lilivyotolewa.

Alibainisha kuwa kuna muda wa kukusanya taarifa na kupiga picha na usiku wafanyakazi hao wanakuwa na kazi ya kuchakata taarifa walizokusanya.

# Waipa tano serikali kusogezewa huduma

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKAZI wa Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi, wameishukuru serikali kwa uamuzi wa kuwapelekea huduma mbalimbali, zikiwamo zinazohusiana na utoaji.

Wamesema hali hiyo imewapunguzia chngamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo nje ya maeneo yao.

Pongezi hizo walizitoa wakati wa uzinduzi wa majengo mawili ya serikali, Mahakama na Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) uliotekelezwa na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa.

Abdallah Juma, Mary David, Said Chinguile na Grace Yohana, wakizungumza kwa niaba ya wenzao, walisema tangu wilaya hiyo ianzishwe miaka 24 iliyopita, huduma za kutafuta haki kupitia vyombo vya sheria, walikuwa wakizifuata wilaya za Lindi na Nachingwea.

Walisema mtu alipokuwa na kesi mahakamani, alilazimika kupelekwa Lindi mjini zaidi ya Kilomita 100 au Nachingwea kilomita 65.

Walisema kwa umbali huo kuliwafanya baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo wakose haki zao kwa kushindwa kumudu gharama kwenda na kurudi Lindi au Nachingwea siku za kesi zao kusikilizwa, zikiwamo na gharama zingine za malazi na chakula.

"Wilaya yetu kujengewa jengo la Mahakama tumefarijika sana, kwani tumepata eneo la kukimbilia kutafuta haki zetu pale tutapodhulumiwa," alisema Said.

Akihutubia wananchi waliojitokeza kwenye uzinduzi huo, Majaliwa alisisitiza kuilinda miradi wanayopelekewa katika maeneo yao ili iweze kuwaletea maendeleo.

Pia aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuondoa hofu kwamba kujengwa kwa jengo la Mahakama hakuna maana ya kutaka kuwafunga watu wasio na hatia, bali ni kurahisisha upatikanaji wa huduma za utoaji haki kwa wananchi.

# TRA yadai kukwamishwa na Nida kutimiza malengo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Manyara, imesema suala la ucheleweshwaji wa vitambulisho vya taifa kwa wananchi linawaathiri hata wao kiutendaji.

Kaimu Meneja wa TRA Mkoa wa Manyara, Pius Mkonda, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake mjini hapa.

"Suala la Nida (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) linatuathiri hata sisi TRA kwa kuwa ili mtu apate TIN namba, ni lazima awe na namba ya Nida," alisema Mkonda.

Alisema jambo hilo linawakwamisha kuongeza wateja wapya, kutokana na watu wanaotaka kufungua biashara mpya kukosa namba za Nida.

"Hili suala linatuathiri kwa kiwango kikubwa maana ukitaka maziwa mengi ni lazima uwe na ng'ombe wengi, hivyo na sisi tunahitaji kuongeza wafanyabiashara wapya lakini kikwazo ni Nida," alisema.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari badala ya kuubiri kufuatwa waliko. "Kukwepa kodi si jambo la kufurahia. Naomba wafanyabiashara lipeni kodi kwa hiari badala ya kusubiri mpaka tuje mtaani. Hii haileti afya," alisisitiza. Mwishoni mwa mwaka jana, Ofisa Usajili wa Nida Mkoa wa Manyara, Emmanuel Joshua, akishirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), alisema Wilaya ya Babati usajili unakwenda vizuri na kwa Babati tu wameshatoa vitambulisho na namba za usajili kwa asilimia 94.

Naye Catherine Imani, mkazi wa Babati, alisema Nida wanawafanya wakwame kupata huduma nyingi za kijamii.

Kutokana na malalamiko hayo, Joseph Christian alishauri serikali kuongeza idadi ya watumishi Nida ili waongeze ufanisi wa kazi na kila Mtanzania apate kitambulisho siyo namba tu.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro (kushoto), akizungumza na kinamama wa Halmashauri ya Arusha juzi, kuhusu kampeni ya ujenzi wa madarasa. Hadi sasa vyumba vya madarasa 149 vimeshajengwa na kuvuka malengo ya vyumba 107.
**PICHA: WOINDE SHIZZA**

# RC aonya viongozi wanaouza makaburi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amewaonya wenyeviti wa vijiji na mitaa kuacha kutembea na mihuri mifukoni kwa ajili ya kuuza maeneo ya wazi na makaburi.

Onyo hilo alilitoa jana Mjini hapa alipokuwa akizungumza na wenyeviti wa vijiji na mitaa, watendaji wa kata, maofisa tarafa wa mkoa huo.

"Nawapa onyo la mwisho leo (jana) msirudie kuuza maeneo ya wazi kama ya shule, zahanati na makaburi. Kibaya zaidi mtu anawauzia zaidi ya mtu mmoja," alisema Mnyeti.

Mnyeti alisema kinachosikitisha zaidi baadhi ya viongozi hao wanauza hadi makaburi mpaka watu wanakosa mahali pa kuzika watu.

"Na wengine mnatembea na mihuri ili mkikutana na wateja muwauzie. Anayetakiwa kukaa na mhuri ni mtendaji wa kijiji au mtaa hivyo mnaotembea na mihuri mnavunja sheria," alisema.

Aliwataka kuwatumia vizuri watendaji wa vijiji na kuwaona kuwa wao ndio wanasheria wao au kamusi zao katika kutafsiri sheria, sera na miongozo mbalimbali ya serikali.

Aidha, aliwataka wenyeviti hao, kutumia mamlaka walionayo kuwasaidia wananchi na siyo kuwanyanyasa, huku akiwashangaa wenyeviti wenye tabia ya kulalamika wakati wao ndio wanajukumu la kutatua changamoto walizo nazo.

# DC aagiza wenyeviti kudhibiti magendo

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, amewaagiza wenyeviti na watendaji wa vijiji vilivyoko mpakani wilayani hapa, kudhibiti magendo yanayoingia nchini na yanayotoka kwenda Kenya.

Alitoa agizo hilo juzi kwenye semina ya kuwajengea uwezo viongozi hao iliyoandaliwa na Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, alipokuwa akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Longido.

"Wakati mwingine mimi na Katibu Tawala, Toba Nguvila, hatulali. tunapambana kudhibiti magendo yanayopita njia zisizo rasmi na tunayakamata lakini hamtupi ushirikiano," alisema.

Mwaisumbe alisema magendo mengi hayapiti barabarani bali njia zisizo rasmi (panya) hali ambayo ni hatari kwa Watanzania kwa kuwa magendo hayo huwafikia watumiaji wengi tofauti na mmoja anayevusha.

"Magendo yakiingia nchini ni hatari kwa taifa na wananchi wake. Nendeni mkawe mabalozi wazuri kukemea biashara ya magendo kwani yanapita katika maeneo yenu," alisema.

Kutokana na kukithiri kwa magendo hayo, Mwaisumbe alisema kwa sasa anajiandaa kufanya ziara kwenye vijiji vyote vilivyopakana na Kenya ili kuangalia na kukagua hali ya usalama ndani ya jamii hiyo kutokana na baadhi ya viongozi kutokuwa waaminifu na wazalendo kwa wananchi waliowapa dhamana.

Alisema sakata la zaidi ya ngamia 200 waliokutwa katika Kijiji cha Kimokuwa wakiwa wanatunzwa na raia wawili wa Somalia kinyume cha utaratibu, huku viongozi wa serikali za mitaa wakiwa wanafahamu jambo hilo. Alisema hali hiyo ni hatari kwa usalama wa nchi.

Baada ya kupata taarifa kuwapo kwa ngamia kutoka Kenya, wanaofugwa katika eneo la Tanzania kinyume cha sheria, alisema aliungana na kamati ya ulinzi na usalama na kukamata ngamia hao na raia hao.

Mwaisumbe alisema raia hao walifikishwa mahakamani na kwa kuwa hawakuwa na kibali cha kuishi nchini, mahakama ilitoa hukumu ya kifungo au faini, hivyo walilipa faini na kutakiwa kuondoka nchini.

Kwa mujibu wa Mwaisumbe, raia hao waliondoka na kwenda Somalia moja kwa moja badala ya Kenya.

"Tumekaa tunasubiri wenye ngamia wajitokeze hawajitokezi lakini taarifa zilizopo kuna kiongozi alikuwa anachukua fedha kwa wenye ngamia, akiwadanganya kuwa anaziwasilisha kwenye serikali ya kijiji, lakini wananchi hawana taarifa yoyote kuhusu ngamia hao," alisema.

Alisema kuwapo kwa ngamia hao, kunaleta shaka ya kiusalama kwa wananchi kwa kuwa kumekuwapo na taarifa ya kuwapo kwa kikosi cha kigaidi kwenye mlima uliopo mpakani, hivyo hata waliokuwa wanachunga ngamia hao, hakuna aliyefahamu kama ni wafuasi wa kikosi hicho.

## Atoa hadhari kutokea njaa

**Na Mwandishi Wetu**, MOSHI

WATANZANIA wametakiwa kuzitumia mvua zinazoendelea kunyesha ili kupata chakula cha kutosha kwa matumizi yao na ya taifa kwa ujumla.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mchungaji wa Assembeles of God Calvary, Saimon Sori, alipokuwa akizungunza na Nipashe ofisini kwake mjini hapa.

Alisema amelazimika kutoa tahadhari hiyo baada ya kupata maono kupitia ndoto mbalimbali zilizokuwa zikimtokea tangu Novemba, mwaka jana na kubaini kwamba zililenga kutoa tahadhari kuhusu janga la njaa ambalo linaweza kuikumba nchi mwaka 2021.

"Kuna ujumbe ambao Mungu ameweza kusema nami tangu Novemba, nilikuwa nimelala usiku, Mungu akaleta maono juu yangu akasema nami kuhusu taifa langu la Tanzania," alisema.

Kutokana na ndoto hizo, alisema ameamua kupeleka ujumbe huo kwa umma kupitia vyombo vya habari ili taifa lipate uelewa na pia tahadhari kuchukuliwa ili kuepuka baa la njaa.

"Kutokana na nafasi niliyo nayo kwa sasa si rahisi kukutana na viongozi wa serikali wa ngazi za juu ili kuwaelezea kuhusu hali hii ndiyo nikaona njia ya pekee ya kuwafikia wananchi na viongozi hao ni kwa njia ya vyombo vya habari ambavyo vinawafikia watu wengi kwa wakati mmoja," alisema.

Aidha, alitoa rai kwa viongozi wa serikali kuendelea kuwahamasisha wananchi kuendelea kuzalisha chakula kwa wingi wakati mvua zikiendelea na wakati huo huo wakihifadhi ili kukabiliana na hatari ya njaa iwapo itatokea.

# TRA kuwaburuza kortini wafanyabiashara

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kilimanjaro, inatarajia kuwafikisha mahakamani wateja 40 mkoani hapa kwa tuhuma za kukiuka matumizi ya risiti za kielektroniki (EFD).

Pia imewaonya wamiliki wa vituo vya mafuta kwa kushindwa kuwapa risiti wateja pindi wanapowapa huduma katika vituo vyao na badala yake huweka risiti hizo katika chombo cha kukusanyia taka.

Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake huku akisisitiza kuwa suala la utoaji wa risiti za EFD ni lazima kwa kila mmoja pindi anapofanya biashara.

Alisema kwa sasa mwanasheria wa mamlaka hiyo, anamalizia kuandaa mashauri hayo na muda wowote kuanzia sasa wafanyabiashara hao watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Mwangosi alisema kumekuwapo na tabia kwa baadhi ya vituo vya kuuzia mafuta kutowakabidhi risiti wateja wao pindi wanapoweka mafuta katika vyombo vyao vya moto.

Badala yake, alisema wafanyabiashara hao huzikusanya risiti hizo katika vyombo vya kuhifadhia uchafu na kusisitiza kuwa jambo hilo ni kosa na yeyote atakayebainika kufanya hivyo, atachukuliwa hatua ikiwamo kutozwa faini au kupelekwa katika vyombo vya sheria.

"Wamiliki wa vituo vya mafuta wamerahisishiwa kazi. Wanapotoa huduma ya mafuta na kurejesha pampu sehemu husika, hutoka risiti papo hapo, hivyo wafanyakazi wa vituo hivyo wana wajibu wa kuhakikisha mteja kabla hajaondoka wanamkabidhi risiti yake na si kuziweka katika chombo cha kukusanyia uchafu," alisema Mwangosi.

Meneja huyo pia aliwaonya wamiliki hao ambao wameweka vyombo vya kukusanyia uchafu kwa lengo la kuweka risiti hizo kuviondoa mara moja kabla ya adhabu haijawafikia.

Aidha, alisema kwa sasa mamlaka ina mpango wa kuhakikisha yeyote mwenye chombo cha moto pindi anapoweka mafuta lakini hachukui risiti, anachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo ulipaji wa faini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tiba wa Hospitali ya Rufani ya Kilutheri ya Haydom mkoani Manyara, Dk. Emanuel Nuwas, akitoa taarifa kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (hayupo pichani), wakati wa hafla ya uzinduzi wa vifaa tiba jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# NHIF yawatoa hofu wananchi vifurushi

**Na Mwandishi Wetu**

TAHARUKI iliyowakumba wananchi baada ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kutangaza vifurushi vipya, imepatiwa ufumbuzi baada ya mfuko huo kuanza kutoa elimu kwa jamii wakiwamo wanahabari wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Kongo, alisema jana katika kikao cha wanahabari jana mjini hapa kuwa wameshaanza kutoa elimu kwa jamii kupitia wanahabari ili kuhakikisha wananchi wanaelewa namna ya kujiunga vifurushi hivyo. Alisema wamezunguka mikoa mbalimbali kutoa elimu hiyo ili kuhakikisha Watanzania wote wanajiunga na mfuko huo na hatimaye kupata huduma za matibabu pindi wanapougua. Aliitaja baadhi ya mikoa ambayo mfuko umezunguka na kutoa elimu kuwa ni Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Lindi, Mtwara, Kigoma, Mwanza, Arusha Kilimanjaro.

"Baada ya kutanganza juu ya vifurushi, utafiti umebaini kuwa bado wananchi wengi hawajaelewa, hivyo tukalazimika kutoa elimu kwa jamii kwa kuwashirikisha wanahabari," alisema.

"Mfuko unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uelewa mdogo kwa wananchi. Bado hakuna sheria inayowabana wananchi kujiunga na bima ya afya, hivyo hakuna uhiari wa wanachama," aliongeza.

Akitoa mada chokozi katika mkutano huo, Hipoliti Lello, Meneja Masoko na Huduma kwa Wateja wa NHIF, alisema kwa sasa Tanzania kuna asilimia 66 ya wananchi ambao hawamo kwenye bima ya afya yoyote, hivyo ni hatari kwa usalama wao na taifa.

Lello alisema ili kufikia wananchi wote kupata bima hiyo, wameanzisha vifurushi vya aina 66 za gharama tofauti ili kuhakikisha kila mwananchi anajiunga kulingana na uhitaji wake. Pia alisema mfuko utahakikisha wanachama wanapata vipimo vya maabara na uchunguzi kama X-Ray, Echo na Ultrasound.

Mwanahabari Paul Wiliam, alisema mbali na kuwapo uelewa mdogo kwa wananchi, bado wananchi wamekuwa wakilalamikia ubora wa huduma zinazotolewa hasa katika hospitali mbalimbali.

"Ni kweli mmeleta vifurushi mbalimbali lakini bado wananchi wakifika katika baadhi ya hospitali kumekuwa na ubaguzi mkubwa wa utoaji wa huduma kwa kuwalinganisha na wanaotoa pesa taslimu huku baadhi ya hospitali zikilalamikia mfuko huo kutowalipa kwa wakati," alisema Sauda Shimbo. Sauda alisema ikiwa NHIF wamekuja na utaratibu huo, iko haja ya mfuko huo kujitathmini hasa katika utoaji wa huduma kwa wananchi ili waweze kupenda kujiunda na bima ya afya.

ama
ALHAMISI JANUARI 16, 2020
AFYA NA MAZINGIRA




## Kikombe, kifaa cha hedhi aina yake

Ukurasa 14



## Siku 3 Waziri Mbarawa Mbeya, Songwe zavuna tumaini la maji

Ukurasa 14



Ukurasa 17

## Rekodi yagunduliwa mti wa miaka 1,000



# OPERESHENI VYOO KAGERA

Ukurasa 18



Kinamama wakifunzwa kutumia kifaa hicho. **PICHA: MTANDAO**

# Kikombe, kifaa cha hedhi aina yake

**Nakuru, KENYA**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la mjini hapa, limezindua mpango wa kusambaza na kuhimiza matumizi ya vikombe maalum vitakavyotumika kwa kinamama wakati wa hedhi, kama njia ya kukabiliana na maradhi na kuwapunguzia gharama za kila mwezi.

Ni mradi unaoelezwa kuungwa mkono na serikali kama anavyosema mwakilishi wake Dk. Torome Kochei, kutoka Wizara ya Afya, anayeutaja kuwa mradi wa kipekee utakaowasaidia na hali zao kijinsia.

Anasema ni kifaa cha kipekee kinachozingatia usafi kwa wasiomudu mbadala, ikizingatiwa suala la hedhi kwa wenye kipato kidogo imekuwa tatizo kubwa kwa jamii nyingi nchini Kenya.

Mary Muthoni, ni miongoni mwa kinamama vijana walioshawishika kukitumia kifaa hicho, anakiri mwanzoni alikiona kifaa hicho 'jambo geni,' lakini sasa amebadili mtazamo wake.

Ni kifaa chenye muundo kama wa chombo cha kukinga mafuta katika chupa na kimetengenezwa kwa mpira laini, mtumiaji anahitajika kukisafisha bila kutumia dawa za kuua viini kila anapokitumia.

Mary anaeleza kuwa mwanamke anayeweza kukitumia hadi saa 12 kwa wakati mmoja, na salama kutumiwa usiku na mchana.

Shirika la Hope in Life kwa ushirikiano na wakfu wa Sulwe wameanzisha mradi wa kutoa mafunzo na kusambaza kifaa hicho cha hedhi kwa kinamama wachanga hasa wanaokabiliwa na changamoto za kifedha.

MAZINGIRA

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

# Siku 3 za Waziri Mbarawa Mbeya, Songwe zavuna tumaini la maji

## • Jicho la kiprofesa lanasa ufisadi



Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, akimtwisha ndoo ya maji mkazi wa wilayani Kyela, ikiwa ni ishara ya kuzindua mradi wa maji utakaowanufaisha wananchi wa vijiji vinane vya kata nne za wilaya hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

MJI ya Mbeya na Songwe nchini ina vyanzo vingi vya maji, lakini wananchi wake hawapati huduma ya maji ya bomba, kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na sababu mbalimbali.

Mojawapo ni kukosa ni baadhi ya makandarasi kuchelewa kukamilisha miradi wanayopewa na serikali na kuna miradi imechukua muda mrefu bila kukamilika, ikiwamo yenye zaidi ya miaka 10 tangu ilipoanza kujengwa.

Baadhi ya miradi ambayo inayotoa huduma, nayo inakabiliwa na tatizo la uchakavu, kutokana na kuwa muda mrefu baadhi iliwekwa tamgy zama za ukoloni na baadhi, inalaezwa ilijengwa kuzingatia idadi ya watu walioku wapo kipindi hicho, lakini sasa miundombinu inashindwa kukidhi mahitaji kutokana na ongezeko kubwa la watu.

**Prof. Mbarawa ziarani.**

Kati ya Desemba 10 na 13 mwaka jana, Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, alifanya ziara ya kufunga mwaka katika mikoa ya Mbeya na Songwe, alikokagua maendeleo ya utekelezaji miradi ya maji ya serikali.

Katika baadhi ya maeneo, alizindua miradi ya maji iliyokamilika na wananchi wakaanza kupata huduma hiyo muhimu, walikuwa walioikosa kwa muda mrefu.

Ziara hiyo iliwapa matumaini makubwa wananchi wa maeneo alikotembelea kupata huduma ya maji ya bomba, kutokana na maagizo na maoni aliyoyatoa wakati wa ukaguzi huo wa miradi.

**MKOANI SONGWE**

Prof. Mbarawa alianzia ziara katika Mkoa wa Songwe ambapo alianzia katika Wilaya ya Momba, alipokagua mradi mkubwa wa maji ya kisima katika Kata ya Ndalambo, unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA).

Huo ni mradi unaokusudiwa kuwanufaisha wananchi 11,000 wa kata hiyo na unatarajiwa kuongeza kiwango cha upatikanaji maji katika Wilaya ya Momba kwa kufikisha asilimia 48.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mbeya-WSSA, Mhandisi Ndele Mengo, hadi Desemba mradi ulishakamilika kwa asilimia 95 na maeneo yaliyobakia ni machache

> **Mpaka sasa tangu tumekabidhi mradi kwa Mbeya-WSSA, unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu tangu walipoanza kutekeleza. Hii ni hatua kubwa mno hata wataalamu wangu wa wizara ni mashahidi haijawahi kutokea mradi kutekelezwa kwa haraka hivyo," anasema Prof. Mbarawa.**

ambayo ndani ya muda mfupi ujao watakamilisha na wananchi kuanza kupata maji.

Mengo anasema, mtandao wa maji hayo wenye urefu wa kilomita 6.9 umeshakamilika, nyumba ya kuhifadhi mashine ya kusukuma maji inayotumia umeme imekamilika kwa asilimia 90 na tayari umeme tumeshaingiza.

"Mradi utakuwa na vituo nane na vyote vimeshaandaliwa kwa asilimia 100, urefu wa matangi mawili yenye urefu wa mita 50 m ambayo moja limekamilika kwa asilimia 98 na lingine asilimia 97, lakini tunaendelea kutekeleza kwa kasi ili tumalize mapema," anasema Mhandisi Mengo.

Prof. Mbarawa anasema, awali mradi ulikuwa unatekelezwa na makandarasi ambao kwa kiwango kikubwa walichangia kuchelewa kwa mradi huo na kuongeza gharama ambazo zilikuwa sio za msingi.

Anasema wakati wanatumika makandarasi mradi ulikuwa unagharimu Sh. milioni 577, lakini baada ya kuachana na makandarasi hao unatarajiwa kugharimu Sh. milioni 345 kutokana na kujengwa kwa kutumia mfumo wa akaunti ya dharura (Force Account).

"Mpaka sasa tangu tumekabidhi mradi kwa Mbeya-WSSA, unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu tangu walipoanza kutekeleza. Hii ni hatua kubwa mno hata wataalamu wangu wa wizara ni mashahidi haijawahi kutokea mradi kutekelezwa kwa haraka hivyo," anasema Prof. Mbarawa.

Waziri anadokeza, mbali na mradi kutekelezwa haraka, lakini ni wa uhakika kutokana na mabomba yanayotumika kuwa ya viwango vinavyotakiwa kutokana na kuchukuliwa moja kwa moja kiwandani.

Anasema makandarasi waliotekeleza mradi huo walimu walishafutiwa usajili na kwamba walikuwa wanatekeleza mradi mwingine katika makao makuu ya wilaya ya Momba, ambako serikali pia itatekeleza kwa utaratibu huo uliotumika huko Ndalambo.

**Mjini Tunduma**

Baada ya kutoka Momba, Prof.

**Inaendelea Uk. 15**

MAZINGIRA

Inatoka Uk. 14

# Siku 3 Waziri Mbarawa Mbeya, Songwe zavuna tumaini la maji

Mbarawa alielekea kutembelea miradi ya visima vitano virefu vya maji katika Mamlaka ya Mji wa Tunduma, ambavyo vimekamilika na tayari wananchi wanapata maji.

Visima alivyotembelea Prof. Mbarawa, vinazalisha maji yenye ujazo wa zaidi ya lita 30,000 kwa siku na kwa mujibu wa wataalamu, vimesaidia kupunguza tatizo la maji katika mji kwa kiwango kikubwa.

Meneja wa Mbeya - WSSA, Mhandisi Mengo anasema kutokana na idadi ya wakazi wa mji huo, bado wanahitaji kutafuta vyanzo vingine vitakavyowezesha kufikisha asilimia 85 ya kiwango cha upatikanaji huduma hiyo. Meneja wa Mamlaka ya Maji Mijini na Vijijini (Ruwasa) Mkoa wa Songwe, Charles Pande, anasema tayari wameanza kufanya upembuzi wa chanzo kipya cha maji ya Mseleleko kutoka wilayani Ileje kwenda mji huo wa Tunduma.

Pande anasema, chanzo hicho kitasafirisha maji kwa zaidi ya kilomita 50 na endapo watafanikiwa kukikamilisha, kitamaliza kabisa tatizo la maji mjini Tunduma na vijiji vitakavyopitiwa na bomba, huku kukiwapo ziada.

"Kile chanzo ni cha uhakika na kina maji ya kutosha, ikitokea tukakikamilisha vizuri, basi tatizo la maji katika Mji wa Tunduma itakuwa ni historia," anasema Meneja Pande.

Baada ya maelezo hayo, Waziri Mbarawa aliitaka mamlaka kuharakisha upembuzi huo, ili fedha za utekelezaji zitolewe mapema na wananchi waondolewe tatizo lililopo.

"Lengo la serikali ni 'kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani'. Sasa naamini kabisa visima tulivyochimba kwenye mji huu havitoshelezi mahitaji, hivyo mnatakiwa mharakishe upembuzi ili tuanze utekelezaji," anasema Prof. Mbarawa.

Maelekezo hayo ya waziri yalionyesha kuongezea nguvu Ruwasa kwenye utekelezaji wa mradi huo, kuwapa matumaini wananchi kupata huduma ya maji.

**Wilaya Mbozi**

Baada ya kutoka Mji wa Tunduma, safari ya Waziri Mbarawa ilielekea chanzo cha maji cha Vwawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, ambacho kinatarajiwa kuwahudumia wananchi wa Mji wa Vwawa.

Ni mradi uliozinduliwa na Rais Dk. John Magufuli alipokuwa ziarani mkoani Songwe, uliokuwa bado haujaanza kupeleka maji kwa wananchi, lakini waziri akawapa wananchi matumaini ya kuanza kupata huduma kuanzia mwezi huu.

Aahidi maji hayo kuanza kusambazwa kwenye makazi ya wananchi mwezi Januari na alizitaka mamlaka zinazohusika kuanza kuweka baadhi ya miundombinu muhimu.



Waziri Prof. Makame Mbarawa, akizungumza na wananchi wa Mji wa Lwangwa katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe kuhusu tatizo la maji linalowakabili.

> **Lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wa maeneo ya miji na wilaya wanapata maji kwa asilimia 90 na wa maeneo ya vijijini wawe wanapata maji kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2020," alisema Prof. Mbarawa.**

"Endeleeni kuwafungia wananchi dira za maji ili watakapokuwa wanalipia wawe wanaelewa vizuri matumizi ya maji, hii inasaidia kupunguza malalamiko yasiyokuwa na maana," anasema Prof Mbarawa.

Matumaini ya wananchi kuwa kilio chao cha muda mrefu kutopata huduma ya maji kwa ufanisi, kikapata nuru ya kuanza kufurahia huduma hiyo. Aliwataka waendelee kuvuta subira.

**Wilaya Kyela**

Baada ya kumaliza ziara yake mkoani Songwe, Waziri Prof. Mbarawa, aliingia katika mkoa wa Mbeya, alianzia katika Wilaya ya Kyela, ambako alileta neema kwa wananchi kwa kuzindua mradi wa maji wa Kapapa Group ulioanza kutekelezwa muda mrefu.

Ni mradi unaoanzia katika chanzo kilichopo Busokelo wilayani Rungwe na unahudumia wananchi zaidi ya 13,000 wa vijiji nane kutoka katika kata nne za Ipinda, Mwaya, Talatala na Ikama, ambako kwa muda mrefu walikuwa hawapati huduma hiyo.

Kwa mujibu wa Prof. Mbarawa mradi huo umeigharimu serikali Sh. bilioni 3.55 na kutokana na mkandarasi wa awali kuchelewa kuukamilisha waliamua kusitisha mkataba na wakaikabidhi Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) ambayo iliukamilisha ndani ya muda mfupi.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha wananchi wa maeneo ya miji na wilaya wanapata maji kwa asilimia 90 na wa maeneo ya vijijini wawe wanapata maji kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2020," alisema Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa mbali na kuzindua neema hiyo kwa wakazi wa kata hizo nne, pia aliwashauri wananchi hao kuunda kamati za watumia maji kwa ajili ya kusimamia mradi huo ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato na kufanyia marekebisho miundombinu.

Hata hivyo, aliwashauri kuendelea kutunza vyanzo vya maji ili kuhakikisha wanaendelea kupata maji katika kipindi chote cha mwaka na kuepuka kuyachafua maji hayo.

**Halmashauri Busokelo**

Akiwa katika Bonde la Mwakaleli, katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, Waziri Mbarawa alikerwa kutoka jijini Dar es Salaam kucheleweshwa mradi wa maji wa bonde hilo kwa zaidi ya miaka 10.

Mradi huo unadaiwa kuwa ulianza kujengwa tangu mwaka 2008, lakini mpaka sasa wananchi bado hawajaanza kunufaika huku kukiwa na ubabaishaji wa mkandarasi katika kuutekeleza.

Mbali na kuchelewesha mradi huo, pia Waziri Prof. Mbarawa, alibaini ubadhirifu mkubwa wa fedha zilizotengwa kuujenga mradi huo, hivyo akaiagiza Polisi kuchukua hatua dhidi mhandisi huyo wa maji wa kampuni hiyo.

Pia, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) kuuchunguza mradi mzima, kwa maelezo baada ya kupitia mpango kazi mzima, alibaini dalili za ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma.

"Mradi mzima unagharimu Sh. bilioni sita na mpaka sasa wameshalipwa bilioni tatu, lakini hakuna kilichofanyika hapa. Nimepitia mpango kazi wao, unaonyesha hiki kibanda cha mabati wamekijenga kwa Sh. milioni 100," analalamika Prof. Mbarawa.

Aidha, kutokana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA) kufanya vizuri kwenye miradi ambayo, ilipewa itekeleze, na Waziri Prof. Mbarawa, aliiagiza kuvunja mkataba wa mkandarasi huyo, ili itekeleze yenyewe.

Anasema, mradi utakapokamilika utawanufaisha wananchi wa vijiji 18 vya Halmashauri za Rungwe na Busokelo, ambao wameikosa huduma ya maji kwa muda mrefu.

AFYA

# DARASA KAMILI...

- Alishangaa sana VVU, mwenza hana na alipovuta hisia 'wa miaka miwili'...
- Mtoto 'salama salmini' kama baba
- Yu tayari kulea...ila 'nabaki kando'
- Siku moja mwambukizaji aliyeyuka



Naomi Ireri, katika picha za harakati zake kufunguka kuhusu vita ya maambukizi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

NI kisa kinachosikitisha, lakini kuna funzo ndani yake kwamba kuishi na virusi vinavyosababisha Ukimwi si mwisho wa safari ya maisha hapa duniani.

Maambukizi ya virusi vya Ukimwi bado yanaongezeka kwa kasi kubwa, lakini ndani ya jamii hatari hiyo bado imekuwa ngumu kwao kuitambua kutokana na ukimya uliotawala kuzungumzia ugonjwa huo.

Kuna watu wengi ikiwamo katika jamii ya Kiafrika wanaouona ugonjwa huo kama jambo la siri, hivyo inakuwa vigumu kuzungumza hadharani kwa kuhofia kutengwa na unyanyapaliwa.

Licha ya serikali pamoja na wadau, kupitia matendo, sera, sheria na kampeni zake, kuhakikisha ukimya unatoweka, bado ni mtihani mkubwa, jamii inaona ni vigumu kufanya hivyo kutokana na 'unyeti' wake.

> **Anasimulia mkasa: "Nilipoenda kufanyiwa vipimo vya damu, wahudumu wa afya walichukua muda kabla ya kunipa majibu yangu na hapo nikaanza kuwa na wasiwasi kwanini matokeo yangu yalichukua muda?"**

**MKASA WA NAOMI**

Kwa Naomi Ireri (41), anayeishi na virusi vya Ukimwi, mkazi wa nchini Kenya ana simulizi kubwa inayombebesha sifa kwa ujasiri wake wa kujitoa hadharani, baada ya kuamua kusimulia jinsi alivyoambukizwa virusi vya Ukimwi.

Kitendo cha Naomi kuwa wazi na hali yake, amepata mialiko mingi katika vituo vya habari nchini mwake na hata kuibua mijadala kwenye mitandao ya kijamii.

Mama huyo mwenye mtoto wa miaka saba hivi sasa, anasema kwamba, alijitambua kuhusu uhalisia wa hali yake, wakati alipokuwa na mimba ya miezi mitano na anahudhuria huduma za kliniki.

Anasimulia mkasa: "Nilipoenda kufanyiwa vipimo vya damu, wahudumu wa afya walichukua muda kabla ya kunipa majibu yangu na hapo nikaanza kuwa na wasiwasi kwanini matokeo yangu yalichukua muda?"

Naomi anaendelea kwamba, baada ya muda kupita aliitwa na kuulizwa iwapo alikuwa amepimwa na kujulishwa kuhusu virusi vya Ukimwi. Jibu lake lilikuwa fupi tu, nalo ni hapana."

Anasimulia kwamba, ilipofika hatua akatambulishwa rasmi kwamba amepata maambukizo ya virusi hivyo, alishtuka sana na kujawa na hofu, asijue la kufanya kwa wakati huo.

Naomi anasimulia kwamba kilichomjia akilini mwake wakati huo ni kwamba, baba ya mtoto wake, kwa maana aliyempa mimba hiyo ndiye aliyemwambukiza.

Haraka aliamua kumpigia simu huku akilia na kumweleza kwa lugha anayoikumbuka katika simulizi yake: "Umefaulu kuniambukiza virusi."

Hata hivyo, mpenzi wake alikanusha kuwa hakumwambukiza, haraka akimjibu yuko tayari kupimwa wakiwa pamoja na waliporejea hospitalini hapo na kumpima tena, majibu yalionyesha Naomi alikuwa na virusi, lakini mpenzi wake hakuwa navyo.

"Nilishangaa sana ni vipi mimi nilikuwa na virusi na mpenzi wangu hana?"

''Hapo ndipo nilianza kurejesha akili yangu nyuma, ili kukumbuka mahusiano mengine ya kimapenzi niliyokuwa nayo."

Anasema ni tafakari ya kina iliyomfikisha katika hatua ya kukumbuka mwanamume mmoja ambaye alishiriki naye ngono mara mmoja tu, tena ilikuwa miaka miwili kabla ya kukutana na mpenzi wake wa sasa.

Naomi anaendelea kusimulia kwamba, kumbukumbu zinamjia kuwa aliambukizwa Ukimwi mwaka 2010, lakini hadi inafikia anafahamu suala hilo, ni mwaka 2012.

Uhakika ni kwamba alikutana na mpenzi wake ambaye ni baba wa mtoto wake akiwa tayari ameambukizwa, ila hakufahamu wakati huo katika mazingira ya upekee katika hilo hawakuambukizana virusi vya ugonjwa huo.

**ILIKUWAJE**

Anasema ndoto yake ya kupata mpenzi ambaye angefunga naye ndoa, iliyeyuka mara alipokutana na mwanaume mmoja mwaka wa 2010.

Walipokutana ghafla mahaba mazito yalimwelemea, katika kipindi cha wiki moja, mapenzi yalikuwa yamenoga hadi wakaamua washiriki ngono.

Pia anasema mtu huyo alikuwa amemwahidi ndoa na mambo mengine mengi.

Ilianza kwa ahadi baada ya wiki moja, waliandaa siku na wakati wa kukutana na alitumai penzi lake na mwanaume huyo lingenoga na hata wawe mume na mke.

Anasema, walikutana kama walivyokuwa wamepanga na kushiriki naye mapenzi kwa usiku huo, baada ya hapo hakumuona tena. Mwanamume huyo hakupokea simu zake na kila mara alizima simu yake, ikiwa ni dalili za kukwepana.

"Nilisononeka sana kwa kuwa sikuweza kumfikia mwanaume huyo ambaye nilikuwa nimeanza kumpenda, ila sikujua nyumbani kwake, wala sehemu ya kumuona na wala sikufahamu jamaa yake," anasema Naomi katika hali ya majonzi.

Baada ya muda, Naomi anasema aliamua kuendelea na maisha ya kila siku, hata akajikuta anaingia katika mchakato wa uhusiano mwingine wa kimapenzi na mwanaume tofauti, ambaye sasa ni baba wa mtoto wake aliyeingia katika historia mpya ya kimaisha.

Naomi anasimulia, pindi aliposhika mimba tu, ndipo matukio ya usiku mmoja yalianza kumjia na kumkumbuka mwanaume huyo asiyemtambua vyema.

Tangu alipofahamu hali yake, baba wa mtoto wake pia alijiweka pembeni na kuvunja uchumba wao, lakini akaahidi atamtunza mtoto akiwa mbali na wao.

Naomi anasema ni jambo lililomfanya ajute sana, lakini anarudi katika ukweli wa kuamua kuangalia maisha yake kama kielelezo cha jamii, kwa wale wanaoharakisha penzi na baadaye kuwatokea puani.



Naomi Ireri

**VIPI KUTOAMBUKIZANA?**

Wataalamu wa afya wana maoni kuwa, maumbile ya mwanaume ni vigumu kupata maambukizi kwa sababu inakuwa ngumu kupata michubuko wakati wa tendo hilo.

Pia, inawezekana wapo wanaume wenye kinga dhidi ya virusi vya Ukimwi au chembechembe zao za kinga hazina mapokezi au receptors vya virusi vya Ukimwi. Inaelezwa kitaalamu, virusi vya Ukimwi vinaingia kwenye chembechembe za kinga kupitia vipokezi mithili ya 'ufunguo na kitasa' au 'nati na boriti.'

Dk. Mathew Dolan wa Marekani, anasema uwezo wa kuzuia maambukizi ya virusi wakaati mwingine hutokea kwa njia mbalimbali na katika makundi mbalimbali ya kijamii akitoa mfano Bara Ulaya na Asia.

Pia, kuna daktari mhusika na tiba hiyi nchini, wanaofafanua wenza wengi wa aina hiyo wanapofika hospitalini na kinamama ndiyo wanaathirika zaidi kwa mujibu wa takwimu za hospitali kubwa aliko jijini Dar es Salaam.

Anasema, ili kirusi kifanye kazi mwilini, ni lazima kinase 'cd4 receptors' inayoshambuliwa na kusababisha kinga ya mwili kushuka na iwapo mtu hana mirija ya mapokezi katika kinga yake, vijidudu hivyo hukosa chakula na vinapotea.

***Makala hii imeandaliwa kwa msaada wa taarifa mbalimbali, zikiwamo za mtandao.***



Moja ya jamii ya mti mkongwe, ambao sasa una miaka 600. Inauwezo wa kuishi miaka 1,000. **PICHA: MTANDAO**

## Rekodi yagunduliwa mti wa miaka 1,000

- Inafuata wa miaka 4,800 • China, Marekani watafiti

**Na Mwandishi Wetu**

MTI unaodumu hadi wastani wa miaka 1,000 na kushangaza watu, sasa wanasayansi wamegundua na kuibuka na majibu yake kulikoni.

Ni utafiti ulioubua siri kuwapo aina ya miti yenye kemikali zinazodhibiti magonjwa na hata athari za ukame unakausha mimea, ikiwa ni tofuati na aina ya miti ambayo vinasaba vyake ni tatizo kuhimili hayo.

Siri ya uwezo wake kusimamia afya yake ni kwamba, ina kama mfumo wa vinasaba ambao havisumbuliwi na ukomo wa umri wa mmea.

Mtafiti Richard Dixon, kutoka Chuo Kikuu cha North Texas, Marekani anasema katika utafiti wao walijaribu kuusambaratisha kwa majaribio na wakagundua kuna namna ya kujihami kuendeleza uhai wake, jambo ambalo ni nadra kwa mimea mingine.

Mimea hiyo inaelezwa kuwa na baadhi ya tabia kama vile; inakua taratibu kuelekea ukubwa wake, ukiwa na rangi za njano na unapatikana zaidi katika ardhi ya China, ambako sasa unatunzwa kwa upekee kwa maana ya mimea adimu.

Watafiti walioshirikiana kutoka China na Marekani, waligundua baadhi ya miti hiyo walioitafiti ina umri kati ya miaka 15 na 667 katika uchambuzi wa kisayansi kuanzia mbegu zao, chembe hai na majani. Walikusanya kwa jumla miti 'mizee' na 'vijana' wakaona yote inatema kemikali za kujihami na kuwezesha kujipa uhai zaidi dhidi ya misukosuko ya kiafya na ukame.

Utafiti wa vinasaba inaonyesha kuna uhusiano kati ya kutofikia ukomo wa mabadiliko ya makuzi katika umri fulani, kama ilivyo kwa mimea mingine, wanyama, hata binadamu.

Dk. Dixon anasema wanachokigundua kwa sasa, kinafanana kwa karibu na miti mingine yenye umri mrefu, kwamba kinachowasimamia ni mazingira ya kiafya katika mtazamo wa namna hiyo

"Ni matumaini yetu kwamba utafiti huu utawahamasisha wengine kuzama zaidi kuhusu picha muhimu kwa umri huo wa mti," anasema.

Bingwa mwingine mtaaluma, Mark Gush, akichangia kuhusu kazi hiyo ya kisayansi, anasema mti ulioishi mikaa mingi zaidi duniani unaitwa Bristlecone pine (Pinus longaeva) -ulikadiriwa kuwa na umri miaka 4,800.

"Uliondoa kupata chakula wakati wote, mwanga na maji bado uwezo wa kufikia umri kama huo unadhaniwa kuhusishwa na kasi (ndogo) ya ukuaji, inavyojilinda na mambo kadhaa yanayofuatia kama magonjwa, hali ya hewa na hatari nyiginezo," anasema.

Uingereza, ni moja ya nchi ambayo katika sera zake, inaamini katika upandaji miti mchanganyiko kwa manufaa ya mazingira, hali ya hewa na mahitaji mengineyo inaitumia kuifuatilia kiyasansi.

Suala la msitu nchini Tanzania nako inapewa umuhimu mkubwa, kama kuwa na asasi, idara na taasisi kama Tafori, sheria na mahitaji mengi yanayoipa umuhimu mimea.

Pia kuna baadhi ya maeneo ambayo kuna hifadhi ya misitu, ikiwamo mimea na aina ya miti maaluma iliyotengwa na hata baadhi iko hatarini kutoweka, mfano hai ni katika Msitu wa Kisarawe, Mkoa wa Pwani.

***KWA MUJIBU WA JARIDA LA KISAYANSI***

AFYA

# OPERESHENI VYOO KAGERA

- Mafanikio yaonekana, tatizo ubora
- Halmashauri Bukoba yashika mkia
- DC Afande awaanika wasio navyo
- Umaskini & uelewa bado shida kuu
- Kujisaidia porini ‘baibai’ taratibu

**Na Lilian Lugakingira,**

**MISSENYI**

HIVI sasa kunasikika kila upande, kampeni na operesheni vyoo ndio dai muhimu la maendeleo na ustawi wa umma. Sehemu nyingi kuna kampeni kubwa, kama ilivyowahi kuripotiwa na Nipashe mkoani Shinyanga na wilaya zake.

Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera, kuna jitihada zinaendelea kuhakikisha kaya zote wilayani humu zinakuwa na vyoo.

Nia ya msukumo huo ni kutaka kuepusha madhara yatokanayo na kutokuwa na vyoo, yakiwamo magonjwa ya mlipuko ambayo yanachangia udumavu kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.



Choo cha Zahanati ya Ishozi, Missenyi kilivyoathiriwa na tetemeko lililotokea mkoani Kagera.

**MRATIBU LISHE**

Mratibu wa Lishe wa Wilaya hiyo Zainath Hassan, anasema kuwa Missenyi ina kaya 43,053 na kuwa hata kama kaya zote zina vyoo, vyoo bora ni 39,608 na visivyo bora ni 3,445.

Zainath anasema kwamba waliamua kupambana na kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo, kuepusha jamii kukumbwa na magonjwa ya kuharisha, kuhara damu, kipindupindu, minyoo ya tumbo, homa ya tumbo, magonjwa ya macho na polio.

Miongoni mwa jitihada wanazozifanya anasema ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa vyoo, kufanya mashindano na kutoa zawadi kwa waliofanya vizuri.

“Tunafanya mashindano ya kaya kwa kata na tunatoa zawadi kwa mshindi, kwa hiyo kata inayoshindwa awamu inayofuata inajitahidi kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo ili ishinde, pia tunatumia sheria ndogo za halmashauri kukabiliana na tatizo la vyoo,” anasema.

Anasema, pamoja na mambo mengine pia ukosefu wa vyoo unaathiri afya za watoto, huku akifatanua: “Mfano kinyesi kuzagaa ovyo kinachafua mazingira, na mtoto kila anachookota anaweka mdomoni.”

> **“Missenyi pia kuna tatizo la baadhi ya makazi kujaa maji na udongo, kichanga unaosababisha vyoo kubomoka, lakini pia kuna tatizo la baadhi ya wanajamii kuhama hasa wafugaji,” anasema Zainath.**

Zainath anawahimizwa kunawa mikono kila wanapotoka chooni na kuwasafisha watoto mikono kwa sabuni, ili kuepuka kula uchafu.

“Wasipofanya hivyo watoto watapata minyoo, wataharisha na lishe itapungua,” anasema.

Jitihada zinazofanyika kwa lengo la kuhakikisha wanaepuka magonjwa ya mlipuko, Wilaya ya Missenyi ina watoto 710 wanaosumbuliwa na magonjwa yanayohofiwa kutokana na tatizo la vyoo.

Zainath anasema, wanaendelea na kampeni ya usafi wa mazingira katika vijiji 77 kwa kuhamasisha jamii kujenga vyoo bora na anasema: “Tutashindanisha vijiji kwa vijiji na kutoa zawadi kwa washindi, pia tutafanya ukaguzi na kutumia sheria ndogo za vijiji maana kila kijiji kina sheria zake.”

Anataja jitihada nyingine kuwa ni kufanya mikutano ya kuhamasisha wananchi kujenga na kutumia vyoo bora, kuchukua hatua kali kwa watakaokaidi na kutoa vipindi katika redio kuhusu umuhimu wa kuwa na choo bora na namna ya kukitumia.

“World Vision watafanya mikutano na kutoa vyoo vya mfano 63 ambavyo watavigawa katika shule za msingi na Kituo cha Afya Bunazi,” anasema Zainath.

**MBINU KUU**

Anasema, serikali kupitia mpango wa kampeni za kitaifa za usafi wa mazingira, inaendesha mashindano na halmashauri hiyo imeshika nafasi ya tatu kitaifa.

Zainath anataja baadhi ya njia wanazotumia kufikisha ujumbe kwa jamii ni mikutano, kutoa vyoo vya mfano, kufanya mashindano, kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara na kutumia vyombo vya habari.

Anataja changamoto zao ni ufinyu wa bajeti unaokwamisha baadhi ya miradi ya usafi wa mazingira kutotekelezwa na uwezo mdogo wa kiuchumi kwa baadhi ya wana kaya unaokwamisha ujenzi wa vyoo bora.

“Missenyi pia kuna tatizo la baadhi ya makazi kujaa maji na udongo, kichanga unaosababisha vyoo kubomoka, lakini pia kuna tatizo la baadhi ya wanajamii kuhama hasa wafugaji,” anasema Zainath.

Kwa mujibu wa mratibu lishe huyo, mipango ya baadaye iliyopo katika kufanikisha ujenzi wa vyoo bora, ni kuboresha na kukarabati vyoo vya jumuiya, mfano katika vituo vya usafiri, akitaja baadhi maarufu, Mutukula na Soko la Bunazi.

Zainath anahidi wataendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ili kuhakikisha elimu inawafikia walengwa ipasavyo.

“Kuna mipango ya muda mrefu ikiwamo kuhamasisha wananchi kutumia mabampa na vyoo vya ‘Smart Toilet’ ambavyo viko kama plastiki na ni rahisi kuvisafisha,” anasema mratibu lishe huyo.

**USHINDANI**

Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, imepanda kutoka kuwa na asilimia 37 ya kaya zenye vyoo bora mwaka 2015 na kufikia asilimia 92 kwa mwaka 2019.

Anatoa wito kwa jamii kuendelea kutambua kuwa matumizi ya vyoo ni muhimu, maana yanaweza kuimarisha afya za umma na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao vizuri, lengo ni kuinua uchumi wa mwananchi na taifa kwa ujumla.

Nipashe ilitembelea kijiji cha Bugorora na kupata maoni ya wakazi na viongozi wao kuhusu umuhimu wa kutumia vyoo bora, mkazi mmojawapo, John Kalikawe wa kijiji hicho, anakiri zamani hakuona umuhimu wa choo, lakini baada ya elimu, sasa anazingatia.

“Kwa sasa nina choo hata kama si bora, lakini kinanisaidia kutunza mazingira na kuepuka kukumbwa na magonjwa ya mlipuko,” anasema.

Anasema, zamani alipohitaji kujisaidia alichimba shimo shambani alilolifukia baada ya kutumia, hali iliyosababisha kinyesi kusambaa shambani, hasa msimu wa mvua.

“Nina mpango wa kujenga choo bora, naendelea kujituma ili nipate fedha kwa ajili ya kujenga choo hicho, maana nimekwishaona umuhimu wake baada ya kupata elimu kupitia kwa mwenyekiti na mhudumu wa afya ngazi ya jamii,” anasema.

**MHUDUMU AFYA**

Odiro Adrian, mhudumu afya ngazi ya jamii katika kijiji cha Bugorora, anasema wanapotembelea kaya miongoni, mwa masuala wanayozingatia na kuyapa kipaumbele, ni kuweka uchafu mbali na watoto.

Anasema, uchafu ikiwamo kinyesi unapozagaa, kuna hatari mtoto anaweza kushika na kula au kuweka vidole vichafu mdomoni, endapo hatagundulika haraka na kusafishwa kwa sabuni.

Odiro anasema, kijijini Bugororoa hadi sasa wamepiga hatua, familia zote hadi mwaka huu zina vyoo, ingawa baadhi si bora, hali inayosababisha wakati wa mvua baadhi hutitia na kusababisha kinyesi kusombwa na maji, kisha kinazagaa ovyo.

“Hali hii inahatarisha afya za wananchi, hasa watoto. Kinachofanyika sasa ni kuendelea kutoa elimu, ili angalau wajenge vyoo imara kidogo ili kuepusha kutitia,” anasema Odiro.

Anasema tatizo linalochangia baadhi ya wananchi kushindwa kujenga vyoo bora, ni hali ngumu kiuchumi na Odiro anfafanua: “Mwaka jana kulikuwa na kaya nne

INAENDELEA UK.19

AFYA

INATOKA UK.18

# OPERESHENI VYOO KAGERA



Daudi Kyeya, Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Kajunguti, wilayani Missenyi, akimwonyesha Balozi Dk. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge hali mbaya ya choo, mwaka juzi.

hazikuwa na vyoo kabisa, lakini kwa mwaka huu zimejenga vyoo hata kama si bora."

Pia, anasimulia ulipofayika mkutano wa hadhara wa kijiji hicho uliohudhuriwa na Mkuu wa Wilaya, Kanali Denice Mwila, alizitaja hadharani kaya zisizo na vyoo na baada ya huo mkutano waliona aibu, walienda kujenga vyoo.

"Kuna familia nyingine utakuta wanaishi katika nyumba iliyojengwa kwa udongo na kuezekwa kwa nyasi. Unawezaje kumwambia atafute matofali na mabati kujenga choo bora?" Anaeleza kwa kuacha tafakari ya kutafakari.

Anasema, watu wa namna hiyo huambiwa wajenge choo kulingana na uwezo wao, kwa kutumia mabanzi ambayo hutakiwa kuzibwa vizuri isiwepo nafasi ya wazi.

"Inabidi kuachwa tundu dogo kwa ajili ya kupitisha haja ambalo hushauriwa kutengeneza mfuniko, ili kutoruhusu wadudu kama inzi kuingia na kubeba uchafu na kuusambaza," anasema.

Odiro watu wanashauriwa kuweka kidumu chirizi na sabuni, ili wanapotoka chooni, wanawa mikono kwa sabuni na mtu asiposafisha mikono vizuri, anaposhika vyombo au kuandaa chakula cha mtoto, anaweza kumlisha uchafu na kuathiri afya yake.

Anasema kuwa baada ya elimu hiyo, watu wanatumiaji vyoo vya wastani, angalau kwa kutumia 'mabampa' ambayo yanauzwa kwa bei rahisi akitaja wastani wa Sh. 10,000.

**MTENDAJI KIJIJI**

Herman Clonery, ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Bugorora, anayesema kijiji chake kina jumla ya kaya 568 na anafafanua:"Kaya 98 zina vyoo bora, kaya 470 hazina vyoo bora na hakuna kaya hata moja isiyo na choo."

Clonery anasema wanaendelea kufanya mikutano ya kuhamasisha wananchi, ili kuhakikisha kaya zote zinakuwa na choo bora.

"Kwa kushirikiana na wahudumu wa afya ngazi ya jamii, wenyeviti wa vitongoji na viongozi wengine wa kijiji, huwa tunaweka mikakati na maazimio kupitia halmashauri ya kijiji, mfano kufanya ukaguzi na kupanga tarehe ya lini tupite kukagua," anasema.

Anasema muda waliopanga ukifika huwa wanaenda kukagua, pia kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutunza usafi wa mazingira, unaojumuisha vyoo na uchimbaji mashimo ya kuhifadhia uchafu.

Anasema kijiji cha Bugorora, hakina sheria za kuhifadhi mazingira, lakini kupitia mikutano wanayoifanya wanaweka maazimio yanayotumika kama sheria, kutekeleza yaliyoazimiwa.

"Kwa wanaokaidi wanawajibishwa kwa mujibu sheria ndogo za uhifadhi mazingira zilizotungwa na halmashauri," anasema Ofisa Mtendaji huyo.

**OFISA AFYA**

Nelson Rumbeli, Ofisa Afya Mkoa wa Kagera, anasema asilimia

> "Ili kufikia lengo hilo tunaendelea kuhamasisha jamii kupitia viongozi wa dini wa serikali na vyombo vya habari. Pia, tutafanya ukaguzi wa 'nyumba kwa nyumba' kwenye makazi ya watu na taasisi, ili kuhakikisha zinaboresha vyoo" anasema.

99.7 ya kaya zote 600,000 mkoani Kagera zina vyoo, na asilimia 0.3 tu ndizo hazina vyoo kabisa.

Rumbeli, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba inaongoza kwa uchache wa vyoo bora ambavyo ni asilimia 36 ya vyoo vyote, ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo yenye asilimia 39.2 na Ngara, asilimia 47.2.

Aidha, anasema, Halmashauri zenye vyoo bora, Missenyi inaongoza kwa asilimia 92.4, ikifuatiwa na Manispaa ya Bukoba yenye asilimia 84.5 na Karagwe asilimia 74.3.

Rumbeli anasema, kuwapo vyoo bora katika kaya kimkoa ni wastani wa asilimia 58.9 na takwimu hizo ni kwa mujibu wa taarifa ya kuanzia Julai hadi Septemba mwaka jana na lengo lililopo, ifikapo Juni 2020, mkoa unalenga kufikia asilimia 75 ya kaya zenye vyoo bora.

"Ili kufikia lengo hilo tunaendelea kuhamasisha jamii kupitia viongozi wa dini wa serikali na vyombo vya habari. Pia, tutafanya ukaguzi wa 'nyumba kwa nyumba' kwenye makazi ya watu na taasisi, ili kuhakikisha zinaboresha vyoo" anasema.

Anasema mkakati ni kufanyika ukaguzi kwa kufuata sheria ndogo za mamlaka za serikali za mitaa katika halmashauri husika.

"Wakati tunafanya ukaguzi tutaongozwa na Sheria ya Afya kwa Umma ya Mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2012," anasema.

Rumbeli anasema, hadi sasa serikali imetoa fedha shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya uboreshaji vyoo na kuwezesha upatikanaji majisafi na salama, kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mkoani Kagera, kunaelezwa kaya zenye vyoo bora zimeongezeka kutoka asilimia 45 mwaka 2018 hadi asilimia 58.9 mwaka jana.

"Namshukuru Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, Katibu Tawala wa Mkoa, Profesa Faustine Kamuzora, wakuu wote wa wilaya na wakurugenzi, ambao kwa jitihada zao wamewezesha kuongezeka kwa kaya zenye vyoo," anasema.



Balozi wa kampeni ya kujenga vyoo, msanii wa Mrisho Mpoto, akiwa ameketi na wanafunzi wa Karagwe, katika moja ya kampeni za 'nyumba ni choo.' **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

AFYA

# Dk. Ndugulile na siri ya kukwepa viriba tumbo

Na Sabato Kasika



SUALA la lishe bora linatajwa kuwa bado ni tatizo kwa baadhi ya Watanzania kufuatia asilimia 30 kudumaa, huku asilimia tano ya watu wazima, hasa kinababa wakiwa na tatizo la viribatumbo.

Ni kauli ya Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, mwaka jana, alipotembelea mabanda ya vyakula vya asili katika Tamasha la Utamaduni ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Jamafest), Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam.

Anasema, Watanzania wengi hawajui kupika, kwa vile wanatumia mafuta mengi katika vyakula, wanakula vyakula vyenye, sukari nyingi na kusababisha watoto wao kudumaa, kutokana na kushindwa kupata lishe inayostahili.

Dk. Ndugulile anaitaja mikoa inayolima vyakula vingi ikiwamo Mbeya na Songwe, kwamba inaongoza kwa watoto kudumaa kutokana na kushindwa kupangilia chakula.

"Vyakula vingi vinatakiwa kupikwa kwa kuchemshwa na sio kujaza mafuta kama watu walivyozoea katika familia yako, pia utumiaji wa nazi nao unachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la viribatumbo na udumavu kwa watoto," anasema.

Dk. Ndugulile anasema matatizo hayo yanaweza kuondoka, endapo watu watazingatia lishe bora, kufanya mazoezi na kupunguza unywaji wa pombe kupita kiasi

Hivyo, chakula chenye virutubisho mbalimbali ni muhimu kwa afya bora na ndicho Watanzania wanatakiwa kukitumia ili kuwa na afya bora na jambo la msingi ni kuzingatia ushauri wa wataalamu wa afya.

Aaeleza kuwa mtu kuwa mnene siyo lishe nzuri, bali unaofaa na mtindo bora wa maisha ni unaozingatia ulaji chakula unaotokana na makundi matano na kufanya mazoezi.

Msisitizo huu unakolezwa na Ofisa Lishe, Mtafiti Mwandamizi kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Margareth Rwenyagira na kutaja makundi hayo kuwa ni matunda, mboga jamii ya kunde na asili ya wanyama.

Vilevile kundi la nafaka, mizizi na ndizi mbichi pamoja na kundi la mafuta, sukari na asali, ambalo linasisitizwa kuliwa kiasi kidogo kwa vile chakula kilichopikwa kwa mafuta mengi na sukari nyingi vinaongeza uzito kwa haraka.

Vyakula vilivyowekwa mafuta mengi na sukari nyingi, humweka mtu, katika hatari ya kupata magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, shinikizo la juu la damu, magonjwa ya moyo na baadhi ya saratani.



Dk Faustine Ndugulile
Naibu Waziri wa Afya

**"Hivyo baada ya kuwapima na kuwapa elimu wameonyesha kuelewa na kufurahia juu ya njia nzuri za kupunguza uzito kwa kuzingatia kanuni za ulaji unaofaa na mtindo bora wa maisha," anasema Rwenyagira.**

Rwenyagira anasema, jamii inapaswa kupata elimu na ushauri juu ya ulaji unaofaa na mtindo bora wa maisha, ili kuepuka kukumbwa na magonjwa, kwa sababu tu kutoelewa ulaji unaotakiwa.

Kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kitaifa jijini Mwanza, Weyamgira anasema: "Watu walikuwa hawajui umuhimu wa kula matunda na mboga kwa wingi.

"Hivyo baada ya kuwapima na kuwapa elimu wameonyesha kuelewa na kufurahia juu ya njia nzuri za kupunguza uzito kwa kuzingatia kanuni za ulaji unaofaa na mtindo bora wa maisha," anasema Rwenyagira.


Ulaji unaofaa kwa ajili ya kuendelea kuwa na afya bora hutegemea kula chakula cha kutosha na mchanganyiko wa vyakula vyenye virutubishi na unasisitizwa pia na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Anasema, lishe bora ni msingi wa maendeleo, na kwamba bila ya Watanzania kuwa na lishe bora, afya bora, nchi haiwezi kufikia lengo la uchumi wa viwanda unaokusudiwa.

Waziri Mkuu alikuwa akifungua mkutano wa sita wa wadau wa lishe nchini, Oktoba mwaka jana, jijini Dodoma na kusema, licha ya umuhimu wa lishe katika jamii, bado kuna tatizo kwa watu wengi.

Kutokana na umuhimu hilo, anasema kuwa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu wa 2020 zitakuwa na ujumbe wa lishe bora, ili kila utakapotoka uwamulike watu na kuwahamasisha juu ya kuzingatia suala la lishe.

Kiongozi huyo anaamini kwamba elimu itawafikia watu wengi na nchi itapiga hatua katika suala la lishe bora, na hatimaye kuondokana na matatizo mbalimbali yanayotokana na lishe duni.





# Naibu Waziri apiga jeki ujenzi madarasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, ameungana na wananchi wa Kata ya Utengule – Usongwe katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, kujenga vyumba tisa vya madarasa.

Vyumba hivyo vinahitajika kwa ajili ya wanafunzi 400 wa kidato cha kwanza waliokosa nafasi.

Dk. Ndugulile aliungana na wananchi hao kujenga vyumba hivyo juzi baada ya kupata taarifa kutoka kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuwa wananchi hao wamejitolea kwa zaidi ya wiki mbili kujenga vyumba hivyo kwa nguvu zao.

Mbali na kushirikiana na wananchi hao siku nzima kujenga vyumba hivyo, pia aliwachangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya kukamilisha mradi huo mapema na wanafunzi ambao wanatakiwa kusoma shuleni hapo waanze masomo haraka.

Alisema wananchi wa kata hiyo ni wa mfano nchi nzima katika kushiriki shughuli za maendeleo na akasisitiza kuwa wanatekeleza kwa vitendo mwongozo wa elimu unaowataka wananchi kushiriki kwenye ujenzi wa miundombinu ya shule. "Katika ziara zangu zote ni mara ya kwanza kuona wananchi wanajitokeza kwenye shughuli za maendeleo kama ninyi. Hii sasa na mimi naahirisha shughuli zangu zote nashinda nanyi siku nzima hapa tukijenga," alisema Dk. Ndugulile.

Alisema wananchi wa maeneo mengine nchini wanatakiwa kuiga mfano wa wakazi wa Mji wa Mbalizi kwa maelezo kuwa baadhi ya maeneo wananchi hawashiriki shughuli hizo na badala yake wanabaki wanalalamika.

Aliwataka wasiishie kujitolea kwenye ujenzi wa vyumba hivyo pekee bali washiriki na kwenye shughuli zingine ikiwamo ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alimhakikishia Naibu Waziri huyo kuwa kwenye ujenzi madarasa hayo uadilifu katika usimamizi wa raslimali ni mkubwa kutokana na wananchi kushirikishwa kwenye ulinzi.

Alisema mbali na mifuko hiyo waliyopewa, pia kuna wadau wengine waliochangia akiwamo Mbunge wa Jimbo hilo, Oran Njeza, ambaye alichangia mifuko 100, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, mifuko 10 na wafanyabiashara wa mji huo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kwa sasa wameanza ujenzi wa vyumba vitatu baada ya vingine sita kufikia hatua ya kuezeka ili kukamilisha idadi ya vyumba tisa vinavyotakiwa na kwamba wananchi wanashiriki kwa asilimia 100.

"Wananchi hawa wanachangia fedha na nguvu zao hapa. Sasa hawawezi wakaruhusu mtu afanye hujuma hapa, hivyo nikuhakikishie ndani ya siku tatu hii mifuko uliyotupatia itakuwa imekwisha na kama utatamani kutuongezea tunakukaribisha," alisema Kisemba. Aliwaomba wadau wengine kuendelea kuchangia ujenzi wa vyumba hivyo ili vikamilike mapema na wanafunzi waanze kusoma mapema ili wasipishane.

Nao baadhi ya wananchi wa kata hiyo walimshukuru Naibu Waziri kwa mchango wake na kwamba mchango huo unawafariji na kuwatia nguvu ya kuendelea kujitolea.

Mmoja wa wananchi hao, Rebeca Kyoma, alisema baada ya kuanza wenyewe kushiriki kwenye mradi huo, viongozi wengi wamejitokeza na kuwatia moyo.

Alisema hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwaahidi kuchangia bando 35 za mabati kwa ajili ya kuezeka vyumba hivyo huku Benki ya NMB pia ikitaka kuezeka.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi, akiwa ameongozana na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, kukagua vyumba vya madarasa vinavyojengwa wilayani humo, jana, kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao wamekosa nafasi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Machinga wapewa mchongo biashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wadogo wa Jiji la Mbeya maarufu kwa jina la 'machinga', wametakiwa kuchangamkia fursa za biashara katika eneo la uwanja wa ndege wa zamani baada ya serikali kuliboresha eneo hilo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Saad Mtambule, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu kuanza kwa soko hilo ambalo ni kwa ajili ya wafanyabiashara hao ambao waliliomba kwa Rais John Magufuli alipokuwa ziarani jijini hapa.

Alisema kwa sasa zimeandaliwa meza zaidi ya 300 kwa ajili ya biashara hiyo na kwamba mnada utakuwa unafanyika siku mbili kwa wiki ambazo ni Jumatano na Jumamosi.

"Tumeshaandaa mazingira yote yako vizuri, sasa tunawashauri machinga wote kuchangamkia biashara katika eneo letu hilo ambalo tulipewa kwa ajili ya shughuli hiyo," alisema Mtambule.

Alisisitiza kuwa meza hizo zilikuwa zinagawiwa kwa watu wenye vitambulisho vya mjasiriamali vilivyotolewa na Rais Magufuli na hivyo wafanyabiashara wakubwa hawana nafasi katika eneo hilo na badala yake wanatakiwa wabaki kwenye maeneo yao rasmi.

Pia alisema halmashauri haitakuwa inakusanya ushuru katika eneo hilo kwa mfanyabiashara mwenye kitambulisho cha mjasiriamali hivyo kila mwenye meza anatakiwa awe huru kufanya

# DC aonya wazazi wasiopeleka watoto kujiunga na sekondari

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya imewatahadharisha wazazi ambao hawatawapeleka shuleni watoto waliofaulu mitihani ya darasa la saba na kuanza kidato cha kwanza kuwa watachukuliwa hatua za kisheria.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi, wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya iliyokuwa na lengo la kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba sita vya madarasa vinavyotakiwa kwa ajili ya watoto hao.

Mahundi alisema baadhi ya wazazi katika wilaya hiyo wana tabia ya kutowapeleka watoto shuleni na badala yake kuwaozesha wakiwa na umri mdogo na kwa watoto wa kiume wanaajiriwa kwenye shughuli ngumu za mashambani na migodini.

Alisema katika wilaya hiyo watoto waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza ni wengi, lakini ambao tayari wameripoti ni wachache na kwamba kwa sasa serikali imetoa muda wa wazazi kuwape watoto wao kwa hiari.

Kwa mujibu wa Mahundi, endapo itabainika kuwa mwamko bado ni mdogo msako utaanza mitaani ili wazazi watakaokamatwa hawajawapeleka watoto wao waanze kuchukuliwa hatua.

"Kuna baadhi ya wazazi sasa hivi wanawaandaa watoto wao kuwaozesha. Sasa wewe jaribu uone, tumeshawapatia maelekezo viongozi wa vijiji ili waendelee kuhamasisha kabla hatujafikia kuanza msako," alisema Mahundi.

Aliwataka wazazi kuendelea kuhamasishana kuwapeleka watoto wao shuleni ili kukwepa kikombe cha kuchukuliwa hatua za kisheria na kwamba wasikubali kuona mtoto hata mmoja ambaye anashindwa kwenda shule.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Cuthbert Mwinuka, alisema wanafunzi waliokosa vyumba vya madarasa ni 261 na vyumba vinavyohitajika ni sita ambavyo tayari vinaendelea kujengwa.

Alisema vyumba hivyo vinajengwa kwa ushirikiano kati ya serikali na wananchi na kwamba mpaka kufikia Januari 30, mwaka huu, vyote vitakuwa vimekamilika na kuwa tayari kuanza kutumika.

Mwinuka alisema ili kukamilisha vyumba hivyo, Halmashauri ya Wilaya imechangia mifuko 543 ya saruji, mabando 30 ya mabati na mbao 750, vifaa ambavyo vimegawanywa kwenye shule zenye ambazo vyumba hivyo vinajengwa.

Alisema vyumba hivyo vinajengwa katika shule za sekondari za Isangawana, Lupa, Mtande na Sangambi na kwamba kati ya shule hizo, ni Isangawana pekee ndiyo ilikuwa na upungufu wa vyumba vitatu.





# Serikali yajipanga kutokomeza sumu kuvu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imejipanga kudhibiti sumu kuvu hususan kwenye mazao ya mahindi na karanga kutokana na kusababisha vifo kwa baadhi ya mikoa na wilaya.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigumwe, alisema hayo juzi alipokuwa akitia saini mkataba wa zaidi ya Sh. milioni 800 katika jitihada za serikali kudhibiti sumu kuvu katika mikoa ambayo inakabiliwa na tatizo hilo.

Mtigumwe alisema tayari serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo.

"Serikali tayari tuko katika hatua mbalimbali za kukabiliana na suala hilo tunaamini litakwisha," alisema Mtigumwe.

Alisema hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa wakulima na wafanyabiashara ya uhifadhi wa mazao ili kusaidia kupunguza tatizo hilo.

Mtigumwe aliongeza kuwa wakulima wengi wamekuwa wamekosa uelewa jinsi ya kuhifadhi mazao baada ya mavuno.

"Tumegundua elimu inahitajika kwa wakulima ya namna ya kuhifadhi mazao naamini mwaka huu tutafanikisha hilo, " alisema.

Mtigumwe alisema kupitia mradi huo wanatarajia kujenga maghala ya kuhifadhi mazao mkoani Dodoma.

Kadhalika, alisema wametia saini mikataba ya aina tano ya kusaidia upembuzi yakinifu na utunzaji wa nafaka kama mahindi na karanga pamoja na maabara ya kilimo.

Naye Mratibu wa Mradi wa Tanipac unaojihusisha na kukabiliana na sumu kuvu, Clepin Josephat, alisema wametia saini mkataba huo kwa ajili ya kudhibiti tatizo hilo katika mikoa 10 ambayo iko hatarini kuathiriwa.

Alifafanua uamuzi huo umetokana na baadhi ya wilaya kuathiriwa na sumu kuvu na kusababisha baadhi ya watu kufariki.

Josephat aliitaja mikoa ambayo imeathiriwa ni Dodoma, Morogoro, Simiyu, Tabora, Kigoma, Mwanza, Manyara, Geita, Mtwara na Ruvuma.

Alisema mwaka 2016, baadhi ya watu walifariki dunia kutokana kuathiriwa na sumu kuvu, hivyo mradi huo wanaamini utasaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia mikoa hiyo kukumbwa na athari hizo.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya, akizungumza na wajasiriamali kwenye mafunzo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TFS kutoa elimu matumizi ya ardhi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Misitu Tanzania (TFS), umejipanga kushirikiana na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, kutoa elimu katika vijiji 150 vilivyo karibu na hifadhi ili kutambua mipaka baina ya eneo la hifadhi na kilimo.

Hayo yalielezwa jana na Kamishna Mhifadhi Misitu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alipokuwa akizungumza kuhusu mikakati uliowekwa na TFS mwaka huu katika kudhibiti ukataji ovyo wa misitu.

Alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kupunguza migogoro kwa wananchi wasio na uelewa juu ya mipaka ya hifadhi ya misitu na maeneo yanayostahili kutumika kwa kilimo kwa jamii inayozunguka.

"Mwaka huu tumejipanga kuhakikisha tunaelimisha wananchi hasa wa vijiji kuhusu umuhimu wa hifadhi za misitu na kujua mipaka kwenye maeneo yao ya kilimo na hifadhi za misitu," alisema Prof. Silayo.

Alisema mwaka jana walitoa elimu kwa vijiji 90 ambavyo wamepata matokeo chanya kutokana na wananchi wengi kuelewa na kuacha kufanya shughuli za kilimo katika maeneo ya hifadhi. "Mkakati wa kutumia elimu unasaidia kwa kiasi kikubwa, hivyo tunaendelea nao mwaka huu ili kuhakikisha kila kijiji kilicho karibu na hifadhi ya misitu, wananchi wanakuwa na elimu ya utunzaji wa hifadhi ya misitu na ardhi," alisema.

Kamishna huyo alisema lengo ni kuona hifadhi zilizoko maeneo ya jirani na vijiji zinakuwa salama kwa ajili ya kuleta maendeleo katika eneo husika na taifa kwa ujumla.

Kuhusiana na kuimarisha ulinzi, Prof. Silayo alisema kuna boti kubwa tano zenye uwezo wa kwenda kina kirefu cha maji kwa ajili ya kukabiliana na wahalifu wa hifadhi za misitu pale wanapobainika na kutaka kutoroka.

Alisema boti hizo zinafanya kazi katika maji ya bahari kuu kwenye mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga pamoja na zile zinazofanya kazi katika Ziwa Victoria.

"TFS imejipanga kuendeleza mkakati wa kulinda hifadhi za misitu zisiharibiwe na wahalifu," alisema Prof. Silayo.

Pia alisema TFS imeimarisha usafiri katika wilaya mbalimbali kwa watumishi ili kuhakikisha misitu na hifadhi zake zinakuwa salama.

## Watakiwa kuchangamkia fursa za uchaguzi mkuu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalang'anya, amewataka wananchi wa Dodoma kuchangamkia fursa za ujasiriamali ikiwamo kutengeneza bidhaa kwa ajili ya uchaguzi mkuu mwaka huu ili kujikwamua kiuchumi.

Nabalang'anya alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wakazi wa Dodoma waliojitokeza kwenye mafunzo ya ujasiriamali yaliyoandaliwa na Jiji la Dodoma kwa kushirikiana na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde.

Alisema kila mwananchi akitumia fursa zilizopo kwenye ujasiriamali umaskini utakuwa historia kwake.

"Umaskini tunajitakia, kila mmoja akitumia fursa zilizopo hakuna mtu atakayelalamika maisha magumu. Kila mmoja ajitume afanye kazi za kuimwingizia kipato," alisema.

Alisema si wakati tena wa kulalamika na kuinyooshea serikali kwa madai kuwa vyuma vimekaza bali kila mmoja ajitume na kutumia vizuri fursa za mafunzo ya ujasiriamali zinapopatikana.

"Sasa tunaingia kwenye mwaka wa uchaguzi ni wakati wa wajasiriamali kutumia fursa ya kutengeneza vitambaa, vikoi, mashati na vitu vingine vyenye nembo ya vyama ili kujiingizia kipato," alisema.

Alisema ujio wa makao makuu unakwenda sambamba na ongezeko la watu ni vyema kama wananchi wa Dodoma wakajipanga ili kuzalisha bidhaa za kutosha na kusisitiza kwamba ni vizuri kujipanga kufanya biashara zenye mafanikio ili kujiimarisha kiuchumi.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Saravai Izina, aliwataka wajasiriamali kujitambua pia akiwahamasisha kujiepusha na matapeli wanaoandaa mafunzo kwa ajili ya kujinufaisha matumbo yao.

"Kazania kidogo ulicho nacho utatoka lakini huwezi kufanikiwa bila kubadilika. Tunafikiria raha zaidi kuliko kipato zaidi. Kwenye biashara unatakiwa umsikilize mteja zaidi kuliko kujifikiria wewe zaidi," alisema.

Katika mafunzo hayo, wajasiriamali walifundishwa kutengeneza bidhaa mbalimbali kama sabuni za aina tofauti, shampoo, mishumaa, chaki na mafuta ya mgando ya kujipaka.



# Sirro ajitosa malalamiko ya wastaafu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, ameahidi kuyapatia ufumbuzi malalamiko ya askari polisi wastaafu kuhusu malipo yao na pensheni. Sirro alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokutana na askari wastaafu wa jeshi hilo wakiwamo maofisa ambao walistaafu kazi, lakini wamedai kuwapo kwa mapunjo ya fedha walizolipwa.

Kutokana na malalamiko hayo, alisema atatuma timu ya wataalamu kutoka Idara ya Fedha makao makuu, Dar es Salaam kuja Zanzibar na kufuatilia suala hilo kwa makini na kutambua kasoro zilizopo. Alisema mfanyakazi yoyote anapostaafu, matarajio yake ni kupata fedha zinazostahiki kwa ajili ya kufanya kazi zake zingine ambazo zinatokana na jasho lake.

"Nitatuma timu ya wataalamu wa fedha kutoka makao makuu kufuatilia suala hili. Watakaa Zanzibar kwa wiki moja kufuatilia kasoro zote zilizojitokeza," alisema. Baadhi ya askari wastaafu wa Polisi Zanzibar walifurahishwa na kauli ya mkuu huyo juu ya kufuatilia malalamiko yao haraka na kuyapatia ufumbuzi.

"Huo ndio uwajibikaji wa kiongozi aliyekabidhiwa majukumu ya kuongoza taasisi kama Jeshi la Polisi na kuyafanyia kazi," alisema Amour Abdalla ambaye alikuwa ofisa wa jeshi hilo aliyestaafu miaka mitatu iliopita.

Malalamiko makubwa ya askari wastaafu ni kupunjwa mafao ikiwamo viinua mgongo kutokana na madai kwamba wamelipwa tofauti na wenzao wa Tanzania Bara waliostaafu pamoja.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ali Ame (kulia), akizungumza na wananchi wakati akikabidhi mabomba ya kusambazia majisafi na salama kwa wakazi wa Kijiji cha Moga, Jimbo la Mkwajuni. Mabomba hayo yaliyotolewa na mwakilishi wa jimbo hilo, Ussi Yahya (kushoto). **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Asisitiza uzalishaji bidhaa zenye ubora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Taasisi ya Ubora na Viwango Zanzibar (ZBS), Khatib Mwadini, amewataka wafanyabiashara kuhakikisha wanazalisha bidhaa zenye ubora ili kunusuru afya za wananchi.

Akizungumza juzi na wananchi na wafanyabiashara katika Maonyesho ya Biashara ya Miaka 56 ya Mapinduzi huko Maisara mjini Zanzibar, alisema iwapo watazalisha bidhaa zenye ubora, zitakuwa na ushindani mkubwa wa soko la ndani na nje.

Mwadini alisema taasisi hiyo itahakikisha afya za watumiaji wa bidhaa zinakuwa salama na kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara.

Pia alisema watahakikisha wanalinda usalama wa afya za wananchi ili kuimarisha uchumi wa nchi na kwamba afya zikiimarika watafanya kazi zao kwa ufanisi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ubora na viwango vya bidhaa unasaidia uimarishaji wa maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja na taifa kwa ujumla.

Aidha, alisema taasisi hiyo ina maabara za kupimia ubora wa bidhaa na hivi karibuni walizuia mafuta ya dizeli ambayo yalikuwa chini ya kiwango.

Pia alisema wana maabara ya kupima ubora wa chakula pamoja na vifaa vya umeme ili kulinda usalama wa wananchi.

# Walalamikia ukosefu huduma za afya Mkwajuni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wa Kijiji cha Mbuyu Maji Jimbo la Mkwajuni wameiomba Wizara ya Afya Zanzibar kuharakisha utoaji wa huduma za afya katika kijiji hicho.

Wakizungumza jana na waandishi wa habari kijijini hapo, wananchi hao walisema ujenzi wa kituo hicho umekamilika lakini wanashangazwa kwa kuchelewa kuanza kufanya kazi.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake, Jabu Makame, alisema hatua hiyo inasababisha kinamama na watoto kupata usumbufu mkubwa kutokana na kutembea masafa marefu kufuata huduma za afya.

Kuanza kutoa huduma kituoni hapo, alisema kutawarahisishia kupata huduma za afya bila usumbufu na kufanya kazi zao zengine za kujitafutia kipato.

Wananchi hao walimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa jitihada zake za kuwajali na kuagiza kujengwa mara moja kituo cha afya kijijini hapo.

"Mwaka 2017, Dk. Shein alifika kijijini hapa kwa kweli hali ilikuwa mbaya, hatuna shule, barabara wala kituo cha afya. Tunashukuru kwa sasa shule tayari watoto wetu wanasoma na kituo cha afya kimeshamalizika kujengwa lakini bado hakijaanza kutoa huduma," alisema Juma Ali, mkazi wa kijiji hicho.

Naye Mwakilishi wa Mkwajuni, Ussi Yahya, alisema atawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini A Unguja kuhakikisha kituo hicho kinafanya kazi.

"Hivi sasa huduma za afya katika ngazi za msingi zimegatuliwa na wenye dhamana na kituo hiki ni halmashauri," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuendelea kuwa na subira kwa sababu bado kituo hicho hakijapata huduma ya majisafi na salama.

Mwakilishi huyo alisema bila huduma ya majisafi na salama, huduma zitakazotolewa zinaweza kusababisha athari kwa wananchi.

Mjumbe wa Kamati ya Fedha ya Halmashauri Wilaya ya Kaskazini A Unguja, Fadhil Babla, alisema halmashauri iko katika hatua za mwisho kuhakikisha kituo hicho kinafunguliwa na kuanza kutoa huduma.

"Mwanzoni mwa mwaka huu, kituo kitafunguliwa wananchi wa kijiji cha Mbuyu Maji wasiwe na wasiwasi," alisema.

# Waziri ataka maadili shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amewataka wazazi na walimu kuwafunza watoto maadili mema, ili wawe watoto wema watakaosaidia kuleta maendeleo baadaye.

Akizungumza katika ufunguzi wa majengo ya madarasa sita na ukumbi wa mitihani katika Shule ya Sekondari Msuka, alisema ipo haja kwa wazazi kushirikiana na walimu katika kumjenga mtoto kimaadili bora.

Alieleza kuwa iwapo watoto watakulia katika maadili mema watapatikana vijana wakakamavu na wenye kuleta maendeleo endelevu katika nchi.

"Watoto utakapowajenga kimaadili mapema, wataepuka kujiingiza katika makundi maovu kama watumiaji wa dawa za kulevya, wizi na udhalilishaji, hivyo tutapata vijana imara hapo baadaye," alisema.

Aliwashukuru wananchi wa Msuka kwa ushirikiano wao na kuwataka wazidishe juhudi, ili kupelekewa maendeleo zaidi ambayo yatawasaidia katika shughuli zao za kila siku ikiwe za kiuchumi.

"Hizi ni juhudi za serikali katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma hivyo," alisema.

Aliwaomba wanafunzi wa shule hiyo kusoma kwa bidii ili wafaulu vizuri. "Serikali inatoa elimu bila malipo kwa wanafunzi kuanzia maandalizi hadi sekondari, lengo ni kuhakikisha watoto wote wanapata elimu, hivyo msome kwa bidii, kwani pia serikali inatoa mkopo wa elimu ya juu," alieleza waziri huyo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Omar Khamis Othman, aliwataka walimu kuwashughulikia watoto kwa nguvu zote, ili waepukane na vitendo vya udhalilishaji.

"Matendo ya udhalilishaji yameenea kila sehemu, watoto wanabakwa na kulawitiwa, hivyo muwe makini na muwasomeshe kwa bidii, ili waweze kufaulu," alisema.

Akisoma taarifa ya kitaalamu Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Zanzibar, Madina Mjaka Mwinyi, alisema ujenzi huo umegharimu Sh. 134, 216,190 mpaka kukamilika kwake.

Alisema ujenzi wa mabanda hayo utasaidia kupunguza msongomano wa wanafunzi katika darasa moja, na kuleta faraja kwa wanafunzi.

"Wanafunzi ilikuwa wanakuja mikondo miwili kutokana na ufinyu wa madarasa, lakini kwa sasa watapunguza shida hiyo," alisema.

Akitaja changamoto katika shule hiyo alisema ni ukosefu wa majisafi salama, ukosefu wa vyoo, uhaba wa walimu na nyumba za walimu, jambo ambalo linazorotesha utendaji katika shule hiyo.

Aliishukuru serikali chini ya Rais wa Dk. Ali Mohamed Shein kwa maendeleo makubwa aliyoyafanya katika kuboresha elimu.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, aliahidi kuitatua changamoto ya vyoo kwa kusaidia saruji, matofali na mawe.

# Barabara yakwamisha mifuko mawe dhahabu

**Na Shaban Njia,**

ZAIDI ya mifuko ya mawe ya dhahabu 10,000 kutoka mgodi wa Pamoja Mining Gold Rush uliopo katika Kijiji cha Wisolele Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, yamekwama kusafirishwa kwenda kwenye uzalishaji kutokana na ubovu wa barabara.

Barabara hiyo imeharibika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika Halmashauri ya Msalala, na inaunganisha vijiji vya Wisolele, Mwazimba, Bukandwe, Nyangarata, Mwakitolio hadi barabara kuu inayotoka Kata ya Segese kwenda Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Hamisi Mabubu, Mwenyekiti wa Mgodi huo, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari maeneo ya mgodi huo ambapo alisema mpaka sasa wanashindwa kuendelea na uzalishaji baada ya mawe yaliyopo kushindwa kusafirishwa.

Aidha, Mabubu alisema kwa sasa biashara ya mawe ya dhahabu imeshindikana kutokana na ukosefu wa barabara yenye uhakika inayokwenda katika Kijiji cha Wisolele ambako ndipo kwenye mgodi huo kutokana na hujaa maji na kusababisha magari yanayobeba mawe hayo kushindwa kufika mgodini.

"Mawe haya mnayoyaona hapa imeshindikana kuyasafirisha baada ya barabara tunayotumia kuwa mbovu na, magari makubwa kushindwa kufika hapa...mawe tunayouza tunatoa gawio kwa serikali ya kijiji kiasi cha Sh. 1,500,000 sawa na mifuko 500 ya mawe haya," alisema Mabubu. Aliongeza: "Licha ya gawio ambalo tunatoa kwenye serikali ya kijiji, bado tunatoa huduma za kimaendeleo kwenye jamii zinazozunguka mgodi hasa kwenye sekta ya elimu, afya, maji pamoja na ugawaji wa zana za kilimo na pembejeo kwa wazee wenye umri wa kuanzia miaka 60." Mabubu alisema kuwa, mgodi wa Pamoja Miningi Gold Rush una maduara 180 kati ya hayo 80 yanatoa dhahabu na mpaka sasa wameshatoa gawio au kodi kwenye serikali ya kijiji zaidi ya Sh. milioni 23, na wameshatenga Sh. milioni nne kwa ajili ya ujenzi wa choo katika Zahanati ya Wisolele.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Msalala, Dk. Ntanwa Kilagwile, alisema halmashauri ina mitambo ya ukarabati wa barabara na kuutaka uongozi wa Mgodi huo kuandika barua ya kuomba msaada wa mitambo hiyo ili kutatua changamoto hiyo.

Pia Dk. Kilagwile alisema, suala la ukarabati wa miundombinu ya barabara jukumu hilo limebaki kwa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (Tarura), lakini halmashauri kwa kuwa inatambua mchango wa wachimbaji wadogo, itahakikisha inashirikiana nao kutatua changamoto inayowakabili.



Mwakilishi wa Balozi wa Norway nchini, Gwen Bwerge ambaye ni Mkurugenzi Mkazi wa NCA Tanzania, akizungumza na wananchi wa Mbulu, baada ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (hayupo pichani), kuzindua vifaa tiba vipya vya Hospitali ya Rufani ya Kilutheri ya Haydom iliyoko Mkoa wa Manyara jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Ndugulile ahimiza wananchi ushiriki maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amewataka wananchi wa Mji wa Mbalizi mkoani Mbeya kujikita kaatika kushiriki katika shughuli za maendeleo ili kutatua changamoto zinazowakabili.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo mjini Mbalizi mkoani Mbeya alipokuwa akishiriki katika ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa ya Shule ya Sekondari Utengule Usongwe kukabiliana na changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Alisema kuwa serikali inaendelea kuamsha ari ya wananchi katika kushiriki shughuli za maendeleo na kuwaunga mkono pale wanapoanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo yao.

"Wizara hii inahusika na masuala yote ya maendeleo, na kazi yetu kubwa ni kuamsha ari ya wananchi katika kujitolea na kushiriki katika shughuli za maendeleo," alisema Dk. Ndugulile.

Dk. Ndugulile alisema kuwa serikali inataka kuona wananchi wanafanya kazi wanajishughulisha na shughuli za maendeleo kwa kuchangia katika miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Mkuu wa Shule hiyo, Benedict Mahenge, aliishukuru serikali, wananchi na wadau walijitolea katika kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo kwani itasaidia kupunguza adha ya wanafunzi kukaa wengi katika darasa moja.

Aidha, Ofisa Elimu Kata ya Utengule Usongwe, George Mtawa, alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa tisa umetokana na kuwa na idadi kubwa ya shule za msingi na ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba, hivyo wananchi waliamua kuanza ujenzi huo ili kuondokana na changamoto ya watoto kukosa madarasa ya kusomea.

Naye Diwani wa Kata ya Utengule Usongwe, Elia Mkono, alisema kuwa wananchi wa kata hiyo wameamua kujenga vyumba vya madarasa hayo ili kuhakikisha watoto 981 wanapata madarasa ya kuanza kidato cha kwanza katika shule hiyo.

# Walimu wahofia maisha yao Kenya

**NAIROBI, Kenya**

WALIMU nchini Kenya wanaofundisha eneo la Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo wanaendelea kuhofia usalama wao.

Hatua hiyo imekuja baada ya wiki iliyopita kundi la kigaidi la Al Shabab kuwashambulia na kuwaua wenzao wanne katika Jimbo la Garissa.

Chama cha kutetea maslahi ya Walimu nchini humo (KNUT) kinataka hatua za dharura na za makusudi kuchukuliwa na serikali ili kuwahakikishia usalama wa walimu hao.

Shambulizi katika Shule ya Kamuthe, limezua hasira na wasiwasi miongoni mwa walimu katika eneo hilo linalopakana na nchi ya Somalia.

Robert Kivuti mfanyakazi katika shule hiyo, alifanikiwa kujificha baada ya kutokea kwa shambulizi hilo, na kueleza kuwa anahofia usalama wake.

"Serikali lazima imefanye jambo ili kutulinda. Ukweli, kuendelea kufunza katika mazingira haya, inakuwa ngumu," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu nchini humo KNUT, Wilson Sossion, anaitaka serikali kuwahakikishia usalama walimu hao la sivyo watachukua hatua.

"Haitoshi tu kusema pole na kutuma risala za rambirambi. Serikali ihakikishe kuwa, walimu wetu wanakuwa salama. Hatuwezi kuendelea kuwa darasani," alisema Sossion.

Alisema kupata tatizo la suala hilo, wanafunzi wanaomaliza sekondari katika eneo hilo lenye idadi kubwa ya Waislamu wenye asili ya Somalia, waruhusiwe kujifunza katika shule hizo za serikali, kwa sababu Al Shabab imekuwa ikiwalenga wageni.

"Wanafunzi wanaomaliza shule za sekondari wanaweza kupewa mafunzo ili wajifunze katika maeneo yao, hili litasaidia kumaliza tatizo hili," alisema Sossion.

Utafiti unaonyesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, asilimia 70 ya walimu, madaktari na wafanyakazi wengine ambao sio wenyeji wa eneo la Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo wameacha kazi.

**RFI**

# Waziri ataja mbinu kuwakabili Al Shabab

**NAIROBI, Kenya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani nchini Kenya, Dk. Fred Matiang'i, amedokeza njia mpya za idara ya ulinzi ambazo wakuu wa usalama nchini humo watatumia na maofisa wa ulinzi katika kukabili tishio la usalama.

Akizungumza katika kikao kikuu cha usalama mjini Mombasa, Matiang'i alisema vitengo mbalimbali vya usalama vilivyoko katika makao makuu ya usalama jijini Nairobi vitagawanywa katika makundi madogo ambavyo maofisa wake watakuwa wakizuru kila jimbo angalau mara mbili kwa mwaka.

Alisema maofisa hao watakuwa wakijumuika na maofisa wa mashinani kufahamu na kupata suluhisho katika kukabili changamoto mbalimbali zinazosababisha tishio la usalama nchini Kenya.

Matiang'i amesema: "Punde baada ya kikao hiki nitawaamrisha maofisa wakuu katika makao makuu ya usalama nchini kujigawanya katika makundi madogo mawili au matatu na wawe wakitembelea kila kaunti mara mbili kwa mwaka ama zaidi na kufanya kazi na maofisa wa usalama katika jimbo ili kujua ni shida gani wanazozipitia na nikupitia njia hiyo ndio tutaweza kujua kinachoendelea kwenye mashina."

Kenya kuna vitengo mbalimbali vya usalama, lakini taifa hilo limekuwa likikabiliwa mara kwa mara na wanamgambo wa Al Shabab na pia makundi ya wahuni katika sehemu mbali mbali za taifa hilo.

Hali hiyo imemlazimu Matiang'i kusema kuwa wanataka vitengo hivyo kuwa pamoja katika kufanya kazi ikiwa ni kushirikiana katika kupeana taarifa za kijasusi, utumiaji wa vifaa sawa na kuweka malengo na mipango ya kila mwaka ya kukabiliana na ukosefu wa usalama.

Katika kikao hicho Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Dk. Karanja Kibicho, alisema kikosi cha pamoja cha idara za usalama kimetayarishwa kwa ajili ya kukabiliana na usalama wa ndani sawa na wahalifu wanaoingia kupitia mipakani.

Baadhi ya mataifa ya Ulaya yamewatahadharisha wananchi wake kutozuru katika majimbo ya Lamu ambayo imekuwa ikishambuliwa mara kwa mara na kundi la kigaidi la Al Shabab ambalo lina maficho ya kambi zake ndani ya msitu mkubwa wa Boni ulioko katika jimbo hilo.

Mwaka 2014 Al Shabab waliua watu wapatao 60 katika eneo la Mpeketoni, Lamu jambo lililolazimisha serikali kupeleka Jeshi la Kenya ndani ya msitu wa Boni kuwaondoa wanamgambo hao lakini hadi sasa msitu huo bado ni makao ya Al Shabab.

***DW***



Kiongozi wa baraza la mpito nchini Sudan, Luteni Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, akizungumza na vyombo vya habari baada ya vikosi vya jeshi la nchi hiyo kuzuia mapinduzi. **PICHA: XINHUA**

# Jeshi Sudan lazima jaribio la mapinduzi

**KHARTOUM, Sudan**

JESHI la Sudan limezima jaribio la uasi lililotekelezwa na kikosi maalumu cha usalama wa taifa ambacho awali kilikuwa kitiifu kwa aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Omar al-Bashir.

Mapambano hayo yalianza juzi katika Jiji la Khartoum na kwamba milio ya milipuko ilisikika na kulazimisha uwanja wa ndege jijini humo kufungwa kwa muda.

Serikali inadai kuwa uasi huo umechochewa na malipo ya mafao, kitengo hicho cha usalama wa taifa kwa sasa kinavunjwa.

Wanajeshi wawili waliuawa na wengine wanne kujeruhiwa kwenye uasi huo.

Kiongozi mwandamizi wa baraza huru linaloongoza Sudan kwa sasa, Jenerali Mohammed Hamdan Dagalo, amemtuhumu mkuu wa zamani wa usalama wa taifa, Salah Gosh kuchochea uasi huo.

Dagalo alisema hachukulii jambo hilo kama jaribio la mapinduzi, lakini alisema jambo hilo halivumiliki.

Hadi kufikia jana asubuhi jeshi lilikuwa likiyashikilia makao makuu ya kikosi hicho.

Katika hotuba yake aliyoitoa jana, kiongozi wa baraza hilo, Luteni Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, alitangaza kuwa mapambano yameisha.

Alisema makao makuu yote yapo chini ya jeshi, na anga la nchi hiyo limefunguliwa.

Wakati huohuo, kumekuwa na wasiwasi juu ya uwezekano wa baadhi ya viongozi waliokuwa na ushawishi wakati wa Bashir kujaribu kutaka mabadiliko ya kisiasa yanayoendelea kushuhudiwa nchini humo kwa sasa.

Bashir ambaye alikaa madarakani kwa mkono wa chuma kwa miaka 30 alipinduliwa Aprili mwaka jana baada ya kutokea kwa maandamano ya umma.

Askari kutoka kitengo cha usalama wa taifa waliweka picha za video kwenye mitandao zikionesha wenzao wakifyatua risasi hewani usiku kama alama ya uasi na kuonesha nguvu zao.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kulikuwa na mapambano katika Wilaya ya Kaskazini Khartoum, na jengo la usalama karibu na uwanja wa ndege.

Vyanzo ndani ya jeshi vinaeleza kuwa vikosi vya serikali kwa sasa vimerejesha hali ya utulivu katika maeneo ambayo waasi walikuwa wakishambulia baada ya kufanya mazungumzo nao.

Kundi kubwa la waandamanaji wa nchi hiyo wametoa wito wa kukomeshwa kwa operesheni hizo zisizokuwa na msingi ambazo zinawatia hofu wananchi.

Waandamanaji zaidi ya 170 waliuawa mwaka jana nchini Sudan, na kikosi hicho cha usalama wa taifa kipo lawamani kwa kutekeleza sehemu kubwa ya mauaji hayo.

***BBC***

# Ahukumiwa miaka 13 jela kunajisi, kutorosha mtoto

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

SHEHA Bakar Khamis, mkazi wa Mitondooni Kambini, Wilaya ya Wete kisiwani Pemba, amehukumiwa kwenda jela miaka 13 na fidia ya Sh. 400,000, baada ya kupatikana na kosa la kumtorosha na kumnajisi mtoto mwenye umri wa miaka sita.

Hakimu wa Mahakama ya Mkoa Wete, Abdalla Yahya Shamhun, alitoa hukumu hiyo baada ya kumaliza kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili na kuona kuwa hakuna chembe ya shaka kwa upande wa mlalamikaji.

Alisema mashahidi wanane walisikilizwa mahakamani hapo, akiwamo daktari ambaye alithibitisha kuwa mtoto huyo alifanyiwa kitendo hicho.

Hakimu alisema mshtakiwa ana makosa mawili, kosa la kwanza ni la kumtorosha mtoto huyo ambapo atatumikia adhabu ya miaka mitatu jela na kosa la pili ni la kunajisi mtoto huyo, hivyo mahakama kumhukumu kwenda jela miaka 10 na kulipa fidia ya Sh. 400,000.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo, Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Pemba, Ali Amour Makame, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili liwe fundisho kwake na kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Ilidaiwa mtuhumiwa alitenda makosa mawili, ambapo kosa la kwanza alilitenda kati ya Mei 1 mwaka 2019 na Mei 2, 2019 eneo la Kiuyu Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa bila ya halali na bila ya ridhaa ya wazazi wake, alimtorosha mtoto mwenye umri wa miaka sita kutoka nyumbani kwao na kumpeleka kwenye Bonde la Kwanyange Mitondooni.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 113 (1) (2) cha Sheria ya Adhabu Namba 6 ya Mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

Kosa la pili kwa mshtakiwa huyo ilidaiwa alilitenda kati ya tarehe hizo kwenye Bonde la Kwanyange Mitondooni Wilaya ya Wete ambapo bila ya halali alimnajisi mtoto huyo. Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume cha kifungu cha 115 (1) cha Sheria ya Adhabu Namba 6 ya Mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.




Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Walemavu, Anthony Mavunde, akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kampuni ya Bakhresa Group kushirikiana na serikali kuwawezesha vijana kunufaika na fursa zitokanazo na mnyororo wa thamani wa viwanda vya kampuni hiyo. Kulia ni Mkurugenzi wa Uhusiano wa Bakhresa Group, Huseni Sufiani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri apiga 'stop' kukamatwa ovyo wafanyabiashara madini

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

NAIBU Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, amepiga marufuku kukamatwa wafanyabiashara waliohifadhi madini maeneo wanayotaka kwa mujibu wa sheria.

Sambamba na hilo, amesema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 Mkoa wa Arusha ulikusanya zaidi ya Sh. bilioni 30 zinazotokana na madini ya vito.

Akizungumza jana jijini hapa wakati akifungua mkutano wa mabalozi wa China nchini na Tanzania nchini China pamoja na wafanyabiashara wa madini nchini, Nyongo alisema sheria inaruhusu wafanyabiashara kukaa na madini ili mradi wafuate sheria.

"Lakini siku za karibuni kumezuka tabia ya kusumbua wafanyabiashara waliofuata sheria za kukaa na madini kwa kulipa kodi zote wanazotakiwa ili wakauze mahali popote wanakotaka lakini wanasumbuliwa kwa kukamatwa na vyombo vya ulinzi," alisema.

Alisema ili kuondoa mkanganyiko huo, wizara imejipanga kuelimisha wadau wa madini vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama kuhusu sheria za madini ikiwamo inayoruhusu wafanyabiashara kushikilia madini kabla ya kuuza kwenye masoko.

Pia aliwaomba mabalozi hao kushawishi wawekezaji kuja kuwekeza nchini kwenye madini ili kuongeza thamani ya rasilimali hizo chini ya gramu mbili ambayo yanaruhusiwa kwenda nje ya nchi bila kuongezwa thamani.

"Kama mna teknolojia ya kuongeza thamani madini haya tunawaalika mje kuwekeza ili tusiyatoe nje bila kuongeza thamani," alisema.

Mkuu wa Mkoa Arusha, Mrisho Gambo, alisema wameleta mkutano huo ili kuongeza fursa kwa wafanyabiashara katika kupanua wigo wa soko la madini.

Alisema Tanzania ina madini mengi lakini mchango wake kwa pato la taifa ni asilimia 5.07 tofauti na pato la utalii asilimia 17 na asilimia 25 katika kuingizia taifa fedha za kigeni.

"Mchango huu hautoshi, hivyo tumeamua kutumia mkutano huu ili tuongeze fursa katika madini na kukuza zaidi pato la sekta hii," alisema.

Kuhusu ukusanyaji wa madini, alisema yanatokana na soko la madini Namanga kukusanya Sh. bilioni 1.7 ya madini ya vito na soko la Arusha walikusanya Sh. bilioni 34.46 katika kipindi cha Juni hadi Desemba, mwaka jana.

Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, aliomba wafanyabiashara kutumia fursa ya mkutano huo kuongeza mapato ya madini kutoka Sh. bilioni 500 ya sasa hadi kufikia Sh. trilioni moja.

# RC apinga Ewura uuzaji petroli, dizeli

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amewataka wenyeviti wa vijiji na mitaa kuwaruhusu wananchi kuuza nishati ya mafuta na kutokubaliana na mamlaka zinazowawekea zuio wakati huduma hiyo inahitajika.

Mnyeti aliwapa rungu hilo wenyeviti jana mjini hapa wakati akizungumza na wenyeviti hao wa mkoa mzima, watendaji wa kata, maofisa tarafa na watendaji wa vijiji na mitaa katika mkutano wake wa kutoa maelekezo ya serikali.

"Waacheni watu wafanye biashara zao za kuuza mafuta maana mtu hawezi kufuata petroli, dizeli au mafuta ya taa nusu lita zaidi ya kilometa 200 kwa watu wa vijijini," alisema Mnyeti.

Aidha, alisema mamlaka zinazokuja kwenye maeneo yao kuwakamata wauzaji wa nishati hiyo wenyeviti wasiwasikilize na akawaambia atakayewasumbua wamwambie aende kumuuliza mkuu wa mkoa.

Mnyeti alisema Tanzania haijaendelea mpaka kufikia hatua ya kuwa na kituo cha mafuta kila kijiji au mtaa, hivyo akawataka wenyeviti hao kuwapuuza na kutokuwapa nafasi ya kuweka zuio la uuzwaji wa mafuta.

Pia aliwataka viongozi hao kuandaa vijana wa kuwadhibiti watu wanaokuja wakijifanya Ewura au Ewura (Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Nishati na Maji) wenyewe kwa lengo la kuvuruga masuala ya maendeleo na wengine kujifanya wanajua.

Kiongozi huyo wa mkoa alisema waachwe wananchi wauze mafuta hata kama wanaowazuia wanadai yatawalipukia na kusisitiza kuwa hata wao wanajua kuwa yanalipuka, hivyo wataweka tahadhari wakishindwa watakaokufa ni watoto wao, hivyo wasibughudhiwe.

"Mimi hapa kwangu mkoani anayejifanya anajua ni Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Wengine wakija hapa wanajitambulisha hapa halafu mimi ndio nawaruhusu kufanya wanachotaka," alisema.

"Mimi hapa kila mtu lazima apige hodi kwa sababu huu mkoa una mwenyewe si mtu kuja tu na kati ya mikoa ambayo ina wenyewe ni huu," alifafanua.

"Akija mgeni akamruhusu aende wilaya fulani akaenda akaharibu, japo huyo mtu namfukuza," aliongeza.

Mnyeti aliwataka viongozi hao wa vijiji kusimama imara katika kusimamia maendeleo na kutetea haki za wananchi siyo kuwaonea maana uongozi ni kuwatumikia wananchi.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Getasam, wilayani Hanang, Hussein Ako, alimshukuru Mnyeti kwa kuwakutanisha na akaunga mkono maelekezo aliyoyatoa.

Alitumia fursa hiyo kuiomba serikali ya awamu ya tano iwakumbuke viongozi hao kwa kuwalipa hata Sh. 1,000 kwa siku maana kazi wanayofanya ni kubwa na wanateseka bila kulipwa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**WAHUDUMU WA HOTELI WANAHITAJIKA** Hoteli ndogo Bagamoyo inatafuta wahudumu, wapishi, usafi, bartender wenye vyeti. Kwa mawasiliano zaidi **Piga 0757 129 546.**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 16/2020**

Ombi la **SAID WALLACE MKUDE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **WALLACE MKUDE MZESE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/01/2020

215586402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LONAGRO TANZANIA LTD** inatangaza kupotea kwa kadiya Gari aina ya **FORD LANGER** yenye namba ya usajili **T656 CKR** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyot e atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/OST/232588/2019**

115586202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FARM CONCERN INTERNATIONAL LTD** inatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya **TRACTOR** yenye namba ya usajili **T590 DQQ** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Yeyot e atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/CHA/RB/389003/2019**

115586102

## KUPOTEA KWA CHETI



**VENANCE JAMES** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha sita chenye **index namba S.1688/0508** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BAHARI BEACH SEKONDARI mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/1577/2019.**

115585402

## PROSHARE CAPITAL LTD

Kutangazwa magari yanauzwa;

1. **MAGESA WILLIAM KARUBI**
   - TOYOTA NOAH T 117 DER
2. **HENRY VICTOR NTAMWEMBE**
   - TOYOTA BREVIS T 579 DEG
3. **DANIEL REUBEN MAKO**
   - SCANIA T 185 DGK
4. **FRANK JULIUS KILAWA**
   - TOYOTA HARRIER T 708 DHB
5. **STEPHEN HERBERT KIJAZI**
   - HILUX SURF T 294 BKL

115585902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 06/2020**

Ombi la PIUS IBRAHIM BONZO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu IBRAHIM PIUS BONZO.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/01/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/01/2020

215586502


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

Uza, Chenye
Thamani Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SARRI: SINA TATIZO NA DYBALA

**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri amebainisha kwamba hakuna tatizo lolote kati yake yeye na Paulo Dybala baada ya fowadi huyo kuonyesha kukasirika wakati akitolewa nje kwenye ushindi wa Jumapili wa mabao 2-1 dhidi ya AS Roma.

Dybala alitoa krosi ya bao la kwanza lililofungwa na Merih Demiral na akapata penalti dakika ya 10 iliyopigwa na kufungwa na Cristiano Ronaldo, lakini alikasirika wakati alipotolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Gonzalo Higuain huku zikiwa zimesalia dakika 20 mpira kumalizika.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumatano wa Coppa Italia dhidi ya Udinese, Sarri alisema hakukuwa na haja ya kusafisha hali ya hewa kuhusu jambo hilo.

"Nazungumza na Dybala kila siku, pia kwa sababu nampenda. Hakuna haja ya kuzungumzia kile kilichotokea," alisema.

"Miongoni mwa mambo mengine, wenzangu waliniambia aliuliza tu kwanini alitolewa, haimaanishi chochote kibaya kwa upande wangu binafsi.

"Tuna bahati kuwa na washambuliaji imara, hakuna tatizo au chochote kibaya, mambo yalikuwa poa."

## SOLSKJAER HAJUI CHOCHOTE KUHUSU FERNANDES

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United inatajwa kwamba inakaribia kumsajili nyota wa Sporting CP, Bruno Fernandes, lakini kocha, Ole Gunnar Solskjaer amedai hana habari hizo.

Nahodha huyo wa Sporting, Fernandes ametajwa kwamba alikuwa anawaniwa na United wakati wa maandalizi ya msimu huu, lakini usajili huo haukufanikiwa na akasaini mkataba mpya Novemba mwaka jana.

Lakini habari zake bado hazijapoa kuhusu uvumi wa kusajiliwa mwezi huu, United imeripotiwa kuwa mstari wa mbele kwenye mbio za kumwania Fernandes, ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Ureno.

Sporting imedai United wanaonekana wanaweza kulipa euro milioni 70 kwa ajili ya kiungo huyo mshambuliaji, huku habari nyingine zikisema kwamba, Marcos Rojo anaweza kurudi Sporting ikiwa ni sehemu ya dili hilo.

Lakini Solskjaer amesisitiza hakuna chochote kimya kinachozungumza na vyombo vya habari wakati na mkutano wake na waandishi wa habari juzi.

"Sijapata taarifa yoyote ya usajili," alisema Solskjaer wakati alipoulizwa kama anaweza kutoa lolote linaloendelea kuhusu Fernandes.

"Kama tukipata kitu ambacho tunaweza kuzungumza na kuwaambia, tutasema, lakini sijapata habari yoyote kwa sasa."

# KOCHA MPYA BARCA ATOA MSIMAMO KWA MESSI



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Quique Setien amesisitiza hataogopa kuwa na msimamo kwa Lionel Messi na nyota wengi wa Barcelona, ingawa anaamini mahusiano yao yatakuwa mazuri tu.

Setien aliteuliwa kuwa kocha mpya wa Barca Jumatatu wiki hii baada ya klabu hiyo kuamua kuachana na Ernesto Valverde licha ya timu kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Inaonekana kama kazi kubwa kwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 61, ambaye kazi yake ya hivi karibuni ilikuwa kule Real Betis, na aliachana nayo mwishoni mwa msimu uliopita.

Hata hivyo, Setien hana shaka na safu yake ya ushambuliaji, ingawa akabainisha kwa mara ya kwanza itakuwa ngumu.

"Nimezungumza na wachezaji na kuonyesha msimamo wangu," alisema Setien akiwaambia waandishi wa habari.

"Sijamzungumzia Messi pekee, bali na wachezaji wengine, ambao nimekuwa nafurahia kuwangalia wakiwa na timu hii na kwenye televisheni.

"Wamenifanya nifurahie soka, nimekuwa nawaangalia kila mchezo na kila siku wanayocheza."

HABARI MICHEZO



# MOURINHO:

## ERIKSEN ATAONDOKA KWA MAFANIKIO

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, amesema, Christian Eriksen anatakiwa "kunyanyua kichwa juu" kama anaondoka Spurs wakati uvumi wa kuhusishwa kujiunga na Inter Milan ukizidi kupamba moto.

Miamba wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Inter wameripotiwa kufanya mazungumzo na Tottenham kwa ajili ya kumsajili Eriksen kwenda pale San Siro kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo la Januari hii.

Eriksen, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, anaonekana kutaka changamoto mpya, akiwa amejiunga na Spurs akitokea Ajax mwaka 2013.

Alipoulizwa kuhusu Eriksen baada ya kuzomewa na mashabiki wa Tottenham wakati wa mchezo wa ushindi wa raundi ya tatu wa Kombe la FA dhidi ya Middlesbrough, Mourinho aliwaambia waandishi wa habari: "Alicheza vizuri. Alicheza vizuri sana, na hivyo ndivyo nilivyokuwa natarajia kutoka kwake.

"Kama akifanya uamuzi wa kuondoka, nafikiri anatakiwa kuondoka huku kichwa chake kikiwa juu, kwani amejitoa kila kitu kwa timu kama ambavyo mchezaji anatakiwa kufanya.

"Mashabiki, mara zote ni wa kuwaheshimu, tunatakiwa kuwaheshimu, lakini kijana alifanya kazi nzuri kwa upande wetu."

Wakati majaliwa ya Eriksen yakionekana yanafikia mwisho hapo Tottenham, kiungo wa Benfica, Gedson Fernandes ameripotiwa anakaribia kutua hapo kwa mkopo kutoka kwa miamba hao wa Ureno.

# TUCHEL

## afurahia 'pea' ya Mbappe, Icardi

**PARIS, Ufaransa**

UPATINA wa Kylian Mbappe na Mauro Icardi unamkumbusha Kocha wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel zama za nyota huyo wa Ufaransa alizofurahia wakati akiwa na Radamel Falcao pale Monaco.

Mbappe amefunga mabao 19 kwenye mechi 21 alizoichezea PSG msimu huu, huku Icardi akiwa amefunga mabao 17 katika mechi 20 tangu alipojiunga kwa mkopo akitokea Inter Milan.

Wote wawili hakuna aliyefunga Jumapili wakati wakitoka sare ya 3-3 dhidi ya Monaco, lakini Tuchel amesifia ushirikiano wao.

Mbappe alichomoza kwenye soka la Ufaransa na Ulaya wakati akicheza pamoja na Falcao kule Monaco ambapo waliipiku PSG na kushinda taji la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, msimu wa mwaka 2016-17, pamoja na kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuifunga Borussia Dortmund iliyokuwa chini ya Tuchel.

"Ndio, ni kama inafanana kwa sababu Falcao anafanana na Mauro, anapenda zaidi kucheza namba tisa, na anaweza kucheza peke yake," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani akiwaambia waandishi wa habari.

"Kylian ana kasi zaidi, anakwenda kwa kasi zaidi akiwa kwenye winga. Ni muunganiko mzuri, ni nzuri kwa upande wao, wanapenda kucheza pamoja na hatari wakiwa pamoja.

"Ni vizuri kwa sababu mara zote tuna wachezaji wawili mbele na ni ngumu kuwazuia."

# LUKAKU AELEZEA FURAHA YAKE INTER

**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku amesema kuondoka kwake Manchester United na kutua Inter lilikuwa chaguo zuri zaidi baada ya mshambuliaji huyo kuendeleza rekodi ya kufunga mabao wakati akifunga mara mbili kwenye Kombe la Italia.

Lukaku alifunga mabao mawili Jumanne kwenye ushindi wa magoli 4-1 dhidi ya Cagliari na kufikisha mabao 18 aliyofunga kwenye mashindano yote tangu aanze kuichezea Inter mwanzoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgili alianza kufunga bao la kwanza sekunde ya 21, huku pia akiifungia Inter kwa kichwa bao la tatu kipindi cha pili mchezo uliopigwa uwanja wa San Siro, ambapo Nerazzurri hao walifuzu robo fainali.

"Lazima niwashukuru wachezaji wenzangu, kocha, wafanyakazi wote na mashabiki. Kila mmoja amenisaidia mimi kuanzia siku ya kwanza," alisema Lukaku, ambaye alifunga mabao sita katika mechi nne zilizopita akiiambia Rai.

"Inter lilikuwa chaguo langu sahihi. Naweza kukua hapa na naweza kutoa mchango wangu mkubwa. Malengo yangu ni kuisaidia timu na najua mashabiki wanapenda hilo.

"Kwa uhakika kufunga ndio kazi na malengo yangu, sijifikirii tu mimi menyewe, lakini pia timu yangu. Nipo hapa kupata mafanikio na natumaini nitashinda kitu fulani hapa."

Kocha wa Inter, Antonio Conte, ambaye alitaka kumsajili Lukaku wakati alipokuwa pale Chelsea kabla ya kumpata msimu huu, alisema: "Mnajua kwamba sipendi kuzungumza sana kuhusu mchezaji mmoja mmoja. Romelu anatupa kile tunachotakiwa kukipata na anaendelea kuimarika."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# PSG NAYO YAJITOSA KUMWANIA ERIKSEN

●●●Ni baada ya Spurs kukataa ofa iliyowasilishwa na Inter Milan ili kunasa saini...

**PARIS, Ufaransa**

MABINGWA wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris Saint-Germain wanajiandaa kuingia kwenye vita ya kuwania saini ya Christian Eriksen wa Tottenham ambaye alikuwa anakaribia kujiunga na Inter Milan.

Kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Denmark anajiandaa kuondoka katika klabu hiyo ya London Kaskazini mwezi huu, baada ya mkataba wake na Spurs kubakisha miezi sita.

Tayari ofa ya pauni milioni 10.5 iliyotolewa na Inter ili kumnasa mchezaji huyo imekataliwa na klabu hiyo ya Ligi Kuu England, ambayo iko tayari kumuuza kwa dau la pauni milioni 20.

Hata hivyo, kwa mujibu wa gazeti la The Mirror, Paris Saint-Germain iko tayari kupambana na vigogo hao wa Ligi Kuu Italia maarufu Serie A ili kumsajili kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27.

Taarifa zinasema kuwa mabingwa hao wa Ligue 1 walikuwa wakifuatilia kwa karibu mazungumzo kati ya timu hizo mbili na ikapata nguvu ya kuanza mchakato wa kumwania nyota huyo ambaye hakuna klabu nyingine zinazohitaji saini yake.

Akiwa amebakisha miezi sita katika mkataba wake, mabingwa hao wa Ufaransa wanaruhusiwa kufanya mazungumzo moja kwa moja na Eriksen.

Nyota huyo wa zamani wa Ajax amefungua milango kwa timu mbalimbali kumwania baada ya kukataa kusaini mkataba mpya na Spurs na kuonyesha nia ya kuondoka klabuni hapo.

Katika majira ya joto mwaka jana, kiungo huyo aliweka wazi anahitaji "kupata uzoefu mpya", ingawa matarajio yake hayakukamilika baada ya kushindwa kuihama klabu hiyo mpaka dirisha la usajili lilipofungwa.

Eriksen alikuwa katika kikosi cha mechi ya marudiano ya Kombe la FA wakati Spurs ilipopata ushindi dhidi ya Middlesbrough.

Baada ya mchezo huo, Jose Mourinho alisema Eriksen alicheza vizuri.

"Alicheza vizuri sana, alicheza kwa weledi wa kiwango cha juu kama tulivyotarajia kuona kutoka kwake.

Kama atafanya uamuzi wa kuondoka, nafikiri ataondoka huku akiwa anajivunia mafanikio, kama ametuonyesha na kutupatia kila kitu, ndivyo alivyotakiwa kuifanyia timu yake."

## KWA UFUPI

**LEICESTER YAMTAKA SHAW**

LEICESTER City imeanza mawasiliano na Manchester United kuhusu uwezekano wa kumsajili beki, Luke Shaw endapo itamkosa beki wake wa kushoto, Ben Chilwell (23), ambaye anawindwa na Chelsea. ***(Mail)***

**FERNANDES, SPURS SAFI**

SPURS iko karibu kukamilisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Benfica na Timu ya Taifa ya Ureno, Gedson Fernandes (21). Usajili huo ukikamilisha utakuwa ni wa kwanza kwa Jose Mourinho, nyota huyo tayari alitua London Jumatatu kufanya vipimo vya afya. ***(Evening Standard)***

**PSG WAMFUATA CAVANI**

MKURUGENZI Mtendaji wa Atletico Madrid, Miguel Angel Gil Marin, ametua jijini Paris kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa PSG na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani (32). ***(Marca)***

**LACAZETTE NJIA PANDA**

HATIMA ya straika wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Alexandre Lacazette (28) kutua Atletico Madrid utafanyika endapo mchakato wa kumnasa Edinson Cavani utakwama. ***(Sky Sports)***

**SOLSKJAER KUNEEMEKA**

MANCHESTER United italazimika kumlipa Kocha Ole Gunnar Solskjaer pauni milioni tano, endapo itafanya uamuzi wa kumtimua kazi. ***(Sun)***

**GIROUD ANUKIA MILAN**

MCHAKATO wa usajili wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud kuelekea Inter Milan unakaribia kukamilika huku Chelsea ikitaka kulipwa pauni milioni sita ili kumtoa nyota huyo mwenye umri wa miaka 33. ***(Star)***

**KESSIE AKARIBIA ARSENAL**

ARSENAL imeanza maandalizi ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Franck Kessie, ambaye ana umri wa miaka 23 kutoka AC Milan. ***(Corriere dello Sport, via Metro)***

**GUIMARAES ATUA SOKONI**

RAIS wa Athletico Paranaense, Mario Celso Petraglia analalamika kuhusu mchakato wa Arsenal wa kuwania saini ya kiungo Mbrazil, Bruno Guimaraes (22). ***(Evening Standard)***

**CHONG KUTUA MILAN**

WAKALA wa winga wa Timu ya Taifa ya Uholanzi na Manchester United, Tahith Chong, ambaye anajiandaa kuondoka Old Trafford, ameonekana katika picha akiwa Inter Milan. ***(Mirror)***

**HUDDERSFIELD YAMNASA KING**

KIUNGO wa Leicester City na Timu ya Taifa ya Wales, Andy King (31), amekubali kujiunga na Huddersfield Town ambayo inashiriki Ligi ya Championship. ***(Mail)***

**JONJOE MAMBO SAFI**

KLABU ya Bundesliga, Schalke inataka kumsajili beki wa kulia wa Everton, Jonjoe Kenny (22), baada ya mchezaji huyo raia wa England kuonyesha kiwango kizuri alipokuwa akiitumikia klabu hiyo ya Ujerumani kwa mkopo. ***(Mail)***

**VELA KUMKARIBISHA HERNANDEZ**

NYOTA wa Los Angeles FC, Carlos Vela anatarajia kumkaribisha mchezaji mwenzake wa zamani wa Sevilla, Javier Hernandez (31) katika timu hiyo baada ya kumalizika kuwatumikia mahasimu wao, LA Galaxy. ***(ESPN)***

HABARI MICHEZO

# MOLINGA, BALINYA WATEMWA RASMI, MORISSON KIMEELEWEKA

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI uongozi wa Yanga umetangaza kuwaacha wachezaji wake watano baada ya dirisha dogo la usajili kufungwa rasmi jana usiku akiwamo mshambuliaji, David Molinga 'Falcao', imempa mkataba wa miaka miwili straika mpya, Benard Morisson, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliwataja wachezaji wengine walioachwa na klabu hiyo ni pamoja na Mganda Juma Balinya, Issa Bigirimana, Sadney Irikhoub na Mustapha Selemani.

Bumbuli alisema wachezaji wengine ambao wametolewa kwa mkopo ni Mwarami Issa na Cleofas Sospeter ambao wamepelekwa Singida United wakati Saidi Mussa na Said Kassimu wamechukuliwa na Lipuli FC.

Kiongozi huyo alisema baada ya kukamilisha usajili wa dirisha dogo kwa kusajili nyota wapya, wanaamini watafanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya Kombe la FA nchini.

"Mpaka sasa tayari tumekamilisha usajili wa wachezaji ambao tulikuwa tunawahitaji katika usajili wa dirisha dogo, naamini msimu huu tutaleta mapinduzi ya hali ya juu," alisema Bumbuli.

Aliongeza pia tayari wameshakamilisha usajili wa straika wao mpya raia wa Ghana, Bernard Morisson ambaye wanaamini ataongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji ya timu hiyo.

"Napenda kuwatangazia rasmi kuwa tumemaliza usajili wetu na mpaka sasa tayari tumemkabidhi mwalimu kikosi kizima, kazi inabaki kwake, kiujumla kikosi cha kwanza kimekamilika," Bumbuli alisema.

Aliongeza kuwa uongozi wa klabu hiyo pia umekiimarisha kikosi cha Yanga Princess kwa kusajili wachezaji wapya wanne na baadhi kuwatoa kwa mkopo ili kwenda kukuza viwango vyao.



Wachezaji wa timu ya kikapu ya Benki ya DTB wakiwa katika mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na Ligi ya Mkoa wa Dar es Salaam maarufu RBA katika msimu wa 2020. DTB ndiyo taasisi pekee inayoshiriki katika ligi hiyo ikiwa na lengo la kufufua kuhamasisha taasisi nyingine kujitokeza kuendeleza mchezo huo hapa nchini.

# Mashabiki waitwa 'kuisapoti' Tanzanite

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), Bakari Shime akisema maandalizi ya kikosi chake kuelekea mchezo dhidi ya Uganda utakaochezwa Jumapili yako vizuri, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), linawaomba mashabiki kujitokeza kwa wingi.

Tanzanite inaikaribisha Uganda katika mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia (U-20), ambazo zitafanyika baadaye Novemba mwaka huu huko Panama na Costarica.

"Wachezaji wako vizuri, tumejipanga kuhakikisha tunafanya vizuri katika mashindano haya, malengo yetu ni kushiriki fainali hizo kubwa, tunataka kuweka rekodi ya kuiwakilisha Tanzania katika michuano hii mwaka huu," Shime alisema.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), Amina Karuma, alisema maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yamekamilika na benchi la ufundi limefanya kazi mapungufu yaliyobainika katika mechi zilizopita.

Alisema pia wanatoa mialiko kwa shule mbalimbali ili kuruhusu wanafunzi kuhudhuria mechi hiyo ili kuongeza hamasa wakati kiingilio cha juu katika mechi hiyo ni Sh. 5,000 kwa eneo la VIP A wakati VIP B ni Sh. 1,000 huku eneo la mzunguko ikiwa ni bure.

# Harmonize balozi mpya wa Sayona

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Rajabu Abdul maarufu Harmonize, ameteuliwa rasmi kuwa balozi wa heshima wa bidhaa za Sayona, imeelezwa jana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini, Pawan Patel, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vinywaji ya Sayona, alisema kuwa wamefurahi kuingia makubaliano na msanii huyo na wanaamini atasaidia kuzinyanyua bidhaa za kampuni hiyo.

Patel alisema wamemteua msanii huyo kwa sababu ni mpambanaji na amedhamiria kuupeleka muziki huo wa Tanzania katika hadhi ya kimataifa.

"Tunajisika fahari kuwa na Harmonize kama balozi wa heshima wa bidhaa yetu. Ni miongoni mwa vijana wapambanaji, mwenye msaada kwa Watanzania wengi, anayefanya kazi kwa bidii, lakini pia amekuwa na chachu ya kuupeleka muziki wa Tanzania mbali zaidi. Hili ni jambo ambalo linaunga mkono malengo na maono yetu ya kuwa kinara katika biashara ya vinywaji baridi barani Afrika," alisema kiongozi huyo katika uzinduzi wa kinywaji cha Twist.

Kwa upande wa Harmonize, alisema ni jambo la faraja kufanya kazi na Sayona na huu ni mwanzo wa ushirikiano mzuri kati yake na kampuni hiyo.

"Twist ni kinywaji kizuri chenye ladha ya kipekee. Nimekuwa nikikitumia mara kwa mara na nimekuwa sehemu ya ubunifu huu mpya wa bidhaa hii, nina hakika Watanzania watafurahia bidhaa hii na matumizi yake yatafika nje ya Tanzania," alisema msanii huyo.

Aliongeza wateja wa vinywaji vya Sayona, sasa watakuwa na fahari ya kuchagua zaidi baada ya kampuni inayotengeneza vinywaji baridi kuboresha na kuzindua upya kinywaji hicho cha TWIST.



# Goba Marathon kufanyika Feb. 2

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya michezo ya Goba (GRR), ya jijini Dar es Salaam imetangaza kuandaa mbio za marathon zitakazofanyika Februari 2, mwaka huu zikiwa na lengo la kuchangia na kuboresha vituo vya afya na kukuza vipaji vya wachezaji vijana.

Akizungumza jijini jana, Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Revocatus Kahendaguza, alisema wameamua kuandaa mbio hizo ambazo zitajulikana kama Goba Hills Marathon ili kuimarisha afya pamoja na mahusiano ya wanachama wake.

"Klabu yetu mpaka sasa imefanikiwa kuendesha mbio fupi 11 maarufu kama 'fun runs' kwenye maeneo tofauti hapa jijini Dar es Salaam. Lakini mwaka huu tumeona ni vema kutanua wigo wetu na kuandaa marathon kamili kwa kuanzia na mwaka huu," Kahendaguza alisema.

Aliongeza kuwa kwa kutambua michezo ni ajira, klabu yao imedhamiria kutumia sehemu ya mapato yatakayotokana na mbio hizi kuwaendeleza wachezaji chipukizi na kutunisha mfuko kwa kujenga kituo.

"Tunaamini kupitia mbio hizi, vijana watapata sehemu nzuri na salama ya kuonyesha na kuendeleza vipaji vyao. Vile vile, klabu yetu imelenga kuboresha baadhi ya vituo vya kwenye maeneo yetu ikiwa ni moja ya juhudi za kuunga mkono sera ya afya ya serikali yetu," alisema Kahendaguza.

Aliongeza kutakuwa na mbio za kilometa 42, nusu marathoni (kilomita 21.1,), kilomita 10 na kilometa tano huku akitaja ada kwa wanariadha watakaoshiriki mbio za marathoni ni Sh. 25,000 na washiriki wanaweza kujiandikisha kupitia mtandao wa gobaruners.fasthub.co.tz.

Michezo
Alhamisi Januari 16, 2020
Nipashe



## PSG nayo yajitosa kumwania Eriksen

HABARI UK 30




Mshambuliaji wa Yanga, Patrick Sibomana (kulia), akijaribu kumtoka beki wa Kagera Sugar, Eric Kyaruzi katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam jana. Yanga ilifungwa mabao 3-0. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# YANGA HALI TETE

## ●●●Ni baada ya Maxime kumkaribisha Kocha Mbelgiji katika Ligi Kuu kwa kichapo cha 3-0, huku...

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa zamani wa Simba na Yanga, Yusuph Mhilu na Peter Mwalyanzi wanaochezea Kagera Sugar, waliongoza mauaji dhidi ya Yanga iliyokubali kichapo cha mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana.

Mhilu ambaye aliwahi kuichezea Yanga na Mwalyanzi aliyewahi kuichezea Simba walikuwa mwiba mchungu na kusababisha majonzi kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo waliojitokeza kushuhudia mchezo, huku wakiwa na furaha kwa kutoka sare dhidi ya Simba.

Pia walikuwa na furaha nyingine ya kuona watani zao hao wamefungwa bao 1-0 dhidi ya Mtibwa Sugar katika fainali ya Kombe la Mapinduzi Visiwani Zanzibar, ambayo wao walitolewa katika hatua ya nusu fainali.

Matokeo hayo yameifanya Kagera Sugar kufikisha pointi 27 baada ya kucheza mechi 17 na kupaa hadi nafasi ya nne huku Yanga iliyoshuka dimbani mara 13 ikibakia na pointi 24 na kuteremka nafasi kwenye katika msimamo wa ligi hiyo.

Kipigo hiko ni kikubwa kwa Yanga msimu huu, lakini ni cha pili baada ya kufungwa bao 1-0 katika mechi ya ufunguzi wa pazia la ligi na 'Maafande' wa Ruvu Shooting.

Shughuli ilianza dakika ya sita tu, pale Abdallah Seseme alipokosa bao la wazi, alipowekewa krosi safi kutoka kwa Yushuph Mhilu, shuti lake likapaa juu ya lango.

Dakika moja baadaye Yanga ilijibu shambulizi, baada ya Mohamed Issa 'Banka' kuwekewa pande maridadi na Haruna Niyonzima, lakini akapiga shuti lililotoka pembeni kidogo ya lango.

Kagera Sugar ilihesabu bao dakika ya 13 lililofungwa na Mhilu. Bao hilo lilitokana na makosa ya beki wa Yanga, Kelvin Yondani alipokosea kuokoa krosi ya mfungaji huyo iliyokuwa ikienda kwa Kelvin Sabato, lakini katika harakati za kuhakikisha mpira haumfikii, akaugonga na kuurudisha tena kwa Mhilu aliyeachia kombora kali lililokwenda moja kwa moja wavuni na kumwacha kipa Farouk Shikalo akiruka baada ya mpira kumpita.

Straika aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo, Ditram Nchimbi alikosa bao la wazi dakika ya 31, baada ya mpira wa kurushwa wa Abdul-Aziz Makame kutua mguuni mwake, lakini mpira ukapaa juu ya lango la Kagera Sugar.

Banka alizawadiwa kadi nyekundu dakika moja kabla ya kwenda mapumziko, alipomvuta Sabato aliyekuwa anaelekea langoni kuifungia timu yake iliyoko chini ya Mecky Maxime bao lingine.

Awali mchezaji huyo alikuwa ameonyesha kadi ya njano iliyotokana na kumfanyia madhambi Seseme.

Kucheza pungufu kulionekana kuwaathiri zaidi Yanga kipindi cha pili, dakika ya 66, Ally Ramadhani aliiandikia Kagera Sugar bao la pili kutokana na makosa ya Niyonzima aliyetaka kupiga chenga ya kisigino, lakini ukaporwa na kumfikia mfungaji ambaye alipiga shuti lililomgonga Lamine Moro na kujaa wavuni.

Wakati wachezaji wa Yanga wakipigana kufa na kupona kutaka kusawazisha mabao hayo kama ilivyokuwa Januari 4, mwaka huu dhidi ya watani zao, walijisahau na kupanda mbele.

Hiyo ilimpa nafasi beki wa zamani wa Yanga, David Luhende kuambaa na mpira upande wa kushoto na kupiga krosi iliyomkuta Mwalyanzi na kuujaza wavuni kwa kichwa.

## Simba yaipania Mbao Kirumba

**Na Somoe Ng'itu**

VITA inaendelea! Ni maneno ya Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbao FC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Simba itashuka dimbani leo ikiwa na 'maumivu' ya kupoteza mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar dhidi ya Mtibwa Sugar, iliyochezwa mapema wiki hii kwa kufungwa bao 1-0.

Matola aliliambia gazeti hili wamejipanga kupambana ili kupata ushindi na kuwafurahisha mashabiki wa Simba, lakini wanajua wazi mechi hiyo ni ngumu.

Kiungo huyo wa zamani wa Simba alisema wanahitaji kuendelea na kasi ya ushindi ili kujiimarisha kileleni na kujiweka katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo wanaoushikilia.

"Haikuwa malengo yetu kupoteza mchezo wa fainali, imetuuma kufungwa, lakini sasa nguvu zote tumeziweka kwenye Ligi Kuu Bara, tunajua ligi ina ushindani na kila timu inahitaji kupata ushindi ili kujiweka nafasi bora, tutaahidi tutapata matokeo mazuri," alisema Matola.

Nahodha wa Simba, John Bocco alisema wamerejea katika Ligi Kuu na nguvu mpya na wamejiandaa kuwapa furaha mashabiki na wapenzi wa klabu hiyo.

"Mpira umebadilika, kila timu inahitaji ushindi, tunajua nao wamejipanga, lakini sisi pia hatutaki kupoteza mchezo, tuko vizuri na tumekuja hapa kwa jukumu moja la kusaka ushindi," Bocco alisema.

Simba ambao wana pointi 35 ndiyo vinara wa ligi hiyo wakiwa wamecheza mechi 14 wakati Mbao FC yenye pointi 18 na imeshuka dimbani mara 16 iko katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ligi hiyo yenye timu 20 itaendelea tena Jumamosi kwa Alliance FC kuwakaribisha mabingwa watetezi Simba kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, wakati Azam FC itavaana na Yanga kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >